ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	N/ Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28. Mhe. Ali Mzee Ali	Uteuzi wa Rais
29.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
30.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
31.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
32.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake

39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
51.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
53.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
55.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
57.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
58. Mhe. Mussa Khamis Silima	Jimbo la Uzini
59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
61.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
62.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
63.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
65.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
66.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
67.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
68.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
69.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
72.Mhe. Salum Amour Mtondoo	Jimbo la Bububu
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75 Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim **Katibu wa Baraza la Wawalishi**

Kikao cha Thalathini na Moja – Tarehe 28 Julai, 2011

(Kikao Kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 211

Ujenzi wa Barabara ya Wete – Konde

Mhe. Jaku Hashim Ayoub Kny Suleiman Hemed Khamis - Aliuliza:

Shughuli za ujenzi wa barabara ya Wete – Konde ulianza mnamo mwezi wa Septemba mwaka 2009. Kuanzia kipindi hicho ujenzi uliendelea vyema na tunategemea kumalizwa wakati wowote kwa kuwa kilichobaki ni utiaji wa lami baada ya kupungua kwa mvua za masika.

(a) Je, Mhe. Waziri ni lini hasa Wizara yako inategemea kukabidhi rasmi barabara hiyo.
(b) Wakati wa ujenzi wa barabara hiyo ni nyumba ngapi zilizoathirika.
(c) Kwa jumla ni kiasi gani cha fedha kinachohitajika cha kugharamia malipo ya fidia ya nyumba hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:

Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 211 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kujibu Mhe. Mwakilishi suala lake, naomba kutoa maelezo mafupi, yafuatayo:

Mhe. Spika, Mradi wa barabara 3 za Kaskazini Pemba, unahusisha barabara za Chake–Wete, Wete-Gando na Wete-Konde. Mradi huo unafadhiliwa kwa pamoja kati ya mfuko *wa SAUDI ARABIA SAUDI FUND* na *BADEA* na SMZ. Mradi huu unategemewa kugharimu jumla ya 29 billioni za Kitanzania. Katika utekelezaji huo, awamu ya kwanza inazihusisha barabara za Wete-Konde na Wete-Gando. Hivyo basi mnamo mwezi wa Septemba 2009, utekelezaji wa

mradi huo ulianza na ulitarajiwa kuchukua muda wa miezi 29 kukamilika kwake yaani mnamo mwezi Januari 2012. Mhe. Spika, mradi huu umekumbana na changamoto mbali mbali ambazo zinaweza kuathiri muda wa utekelezaji wa mradi huo. Miongoni mwa changamoto hizo ni fidia, eneo la kufanyia kazi, mvua, malipo n.k.

Baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, mategemeo yetu mradi ulipangwa kukamilika mwezi Januari, 2012. Hata hivyo, napenda nikiri kutokana na changamoto nilizozieleza kwa uwezekano mkubwa wa muda huo kuengezwa.

Hata hivyo, Wizara yangu itajitahidi kumtaka mkandarasi anaharakisha muda pamoja na changamoto hizo tulizozieleza.

(b) Mhe. Spika, katika ujenzi wa barabara hizo jumla ya nyumba 241 zilikisiwa kubomolewa ili kupisha ujenzi wa barabara hizo. Hata hivyo, idadi ya nyumba hizo zimeengezeka kutokana na kuwepo kwa idadi kubwa ya nyumba zilizoathirika katika harakati za ujenzi huo. Wizara yangu inaendelea kuratibu na zoezi zima litakapokamilika tutaendelea taratibu za kulipa fidia kwa wamiliki wa nyumba hizo.

(c) Mhe. Spika, gharama ya awali ilikuwa ni jumla ya 670,890,000/= hata hivyo kiasi cha shilingi 375 Mill, zimeshalipwa kwa upande Wete-Konde. Mchanganuo wa gharama hizo kwa upande na Wete-Gando, ni takriban 2,000,000,000/= zinahitajika kwa ajili ya kulipa fidia.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri kama utakumbuka katika majibu yako siku zote unapokuwa unajibu, siku zote unasema wizara yako iko katika jitihada, hebu twambie hizo hitihada zako lini zitamalizika na huku wakati wananchi wa konge wakiwa wanateseka kwa usafiri huu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, katika majibu yetu tumeeleza kwamba, tulikuwa tukidaiwa shilingi milioni 670 hadi muda huu, tumeshalipa shilingi milioni 375 naamini hizi ni jitihada za kuonesha kwamba serikali iko *serious* kikwazo ni upatikanaji wa fedha. Lakini kadiri tutakavyopata fedha ndivyo tutakavyoweza kutekeleza wajibu wetu wa kulipa fidia.

Nam. 230

Ujenzi wa Hoteli Maeneo ya Mji Mkongwe

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Kumekuwepo na kasi ya ujenzi wa hoteli ndani ya Mji Mkongwe bila ya kujali kuwa hapo nyuma tayari kulipigwa marufuku ya ujenzi wa hoteli katika eneo hilo.

(a) Je, marufuku hayo sasa imeondoshwa.
(b) Kuna sababu zipi za msingi zilizopelekea marufuku hayo kuondoshwa.
(c) Serikali haioni kwamba idadi kubwa ya hoteli katika sehemu hiyo ni kuhatarisha maisha ya watoto wetu.
(d) Je, kuzigeuza nyumba za Mji Mkongwe kuwa hoteli hakuathiri utunzaji wa Mji Mkongwe.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 230 lenye kifungu (a), (b), (c) na (d) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali kwa Maana ya Baraza la Mapinduzi haijapiga marufuku ujenzi wa hoteli katika eneo la Mji Mkongwe Serikali inachokifanya ni *control* idadi ya maombi yanayoletwa Mji Mkongwe kwa ajili ya kujenga hoteli.

(b) Serikali ihaijapiga marufuku.

(c) Serikali haioni kwamba kutakuwa na matatizo ya maisha ya watoto kama zikijengwa hoteli Mji Mkongwe kwa idadi ile inayoruhusiwa na serikali.

(d) Kuzigeuza nyumba za Mji Mkongwe kuwa hoteli kunategemea maombi na ile namna ya ujenzi wa hoteli zenyewe, kama ujenzi huo hautobadilisha aina ya nyumba hizo za Mji Mkongwe ujenzi huo hautaathiri urithi wa Mji Mkongwe.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa maana hiyo unachotaka kunambia Mhe. Waziri tutaendelea kuwa nyumba zenye mahoteli katika Mji Mkongwe.
Kama tutaendelea huoni athari itazidi tena kwa watoto vile vile, ikiwemo kuvuta unga, ulevi na mavazi ya nguo mbovu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaa, Maji na Nishati: Mhe. Spika, nilipokuwa najibu swali mama nilisema:

(a) Ujenzi wa hoteli haukupigwa marufuku ila tunaudhibiti kwa namna ya maombi yanavyokuja na muombaji mwenyewe.

(b) Kwa maana hiyo ya (a) hakutakuwa na uharibifu wa watoto wanaoishi Mji Mkongwe. Suala la kuvuta unga na kulewa na kuvaa nguo zilizokuwa sio za heshima limeenea kila hapali nchi hii hata ng'ambu kuna aina hiyo ya uvutaji unga ya kuvaa nguo zisizokuwa za heshima. Kwa hivyo suala hilo halipo Mji Mkongwe peke yake na haliletwi na ujenzi wa hoteli.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Raisi Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa Mwaka 2011/2012

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kwanza kabisa asubuhi ya leo kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Fedha.

Mhe. Spika, nianze kama ilivyokuwa kawaida yetu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uhai na uzima tukiendelea na kazi zetu hapa za kujadili masuala yanayowagusa wananchi wetu.

Mhe. Spika, naomba nianze kwa kusemka kwamba wizara hii tunayoizungumza ni wizara muhimu sana katika kusimamia utendaji wa shughuli za serikali katika nchi yetu. Kwa sababu hiyo ni vizuri sana au ni muhimu sana waziri wetu anayesimamia masuala haya akawa na nguvu kamili ya kuweza kuuzimamia uchumi wetu.

Mhe. Spika, pahala popote duniani Waziri wa Fedha ndiye anayeratib masuala mazima ya uchumi wanchi. Kwa hivyo ni muhimu sana kuweza kuwa na nguvu

za ku- *determine fiscal and monetary policies* katika nchi, (sera za uchumi na fedha). Lakini kwetu sisi bahati mbaya Mhe. Spika, kutokana na mfumo wetu wa muungano uliokuwepo Waziri wetu wa Fedha hana madaraka hayo, au labda tuseme hayakutimia vizuri.

Mchango wangu wa kwanza Mhe. Spika, nilikuwa nataka kuomba kwamba waziri akija hapa atusaidie. Ni madaraka yetu ya msingi ambayo tunayakosa kutokana na mfumo wetu ulivyo ambao unamnyima yeye fursa ya kusimamia kikamilifu uchumi wetu.

Mhe. Spika, niliwahi kuchangia katika michango yangu ya nyuma katika kikao hiki kwamba taasisi mbili kubwa za fedha zinazosimamia uchumi wetu katika jamuhuri ya muungano ni Benki Kuu ya Tanzania (*BoT*) ambayo inasimamia masuala ya sarafu na mabenki. Lakini pia kuna hawa *TRA* ambayo pia inasimamia masuala mazima ya kodi.

Mhe. Spika, ukivitizama vyombo hivi, utendaji wake wa kazi hauonekani kwamba unazingatia kwamba vinasimamia chumi mbili tafauti. Kwa vyovyote vile uchumi wa kisiwa na uchumi wa nchi kubwa kama ilivyo Tanganyika au Tanzania Bara hauwezi kuwa sawa. Kwa vyovyote vile zile njia za kutegemea kukuza uchumi haziwezi kuwa sawa. Tulitegemea jambo lile serikali itakaa itafanya maamuzi yake lizingatie hilo. Lakini sio tu kwamba halizingatiwi.

Kwa maoni yangu Mhe. Spika, ule muundo wake hauruhusu hata kuzingatiwa. Nasema hivyo kwa sababu ikitizama bodi zile zinazosimamia vyombo hivi Wazanzibari ni wachache sana. Niliwahi kutoa mfano uliotolewa Bungeni kwamba kulitolewa kitabu katika hiki kikao cha Bunge kinachoendelea cha BOT kile chenye viongozi na Maafisa wa ngazi za juu wa Benki ile jumla yao ni 80 Mzanzibari alikuwa ni mmoja tu. Lakini na *TRA* nina hakika tukenda kutizama bodi pengine kama kuna Mzanzibari pengine ni wawili.

Mhe. Spika, kaka hali kama hiyo hawa wengine hawawezi kutambua vizuri uchumi wa kisiwa *(Island Economy)* kwa hivyo sidhani kama wanaweza wakatusaidia katika kupanga sera zao za uchumi na fedha katika nchi na masuala mazima ya kodi kwamba wataweza kutizama kwa ukamilifu vipi kuwa na sera ambazo zitavua uchumi wa Zanzibar. Nitoe mfano Mhe. Spika, wakati fulani nchi yetu ilikuwa inafikiria kuanzisha mfumo wa *Offshore Companies* na *Offshore Bank*.

Mhe. Spika, wakati ule aliyekuwa Waziri wetu wa Fedha hapa Zanzibar Mhe. Amina Salum Ali alishatayarisha mswada ambao kuwa ulikuwa uwasilishwe kikako kilichofanyika Pemba nakumbuka cha Baraza la Wawakilishi. Lakini

aliyekuwa Waziri wa Fedha wa Jamuhuri ya Muungano Marehemu Kigoma Ali Malima akaja akauzuia Mswada ule kwa kusema kwamba madaraka haya hayapo kwa Waziri wa Fedha wa Zanzibar.

Mhe. Spika, vitu kama hivi pengine kwa uchumi wetu wa kisiwa *offshore Companies* na *offshore Bank* ingekuwa ni kitu sahihi kabisa, lakini unakuta huna madaraka hayo. Tunazungumzia hapa mara nyingi kila tunapoijadili wizara hii masuala mazima ya kodi kwa mfano Mhe. Spika, katika suala hili la ku - *determine* viwango vidogo vya ushuru kwa upande wa Zanzibar ili kuvutia biashara ya mpito hapa. Kwa sababu sisi kama ni kisiwa uchumi wetu ungetegemea kwa kiasi kikubwa biashara ya mpito. Sisi hatuzalishi kiasi kikubwa Mhe. Spika. Waziri wetu wa Fedha hana madara ya mwisho wa kuamua viwango vya ushuru hapa.

Mhe. Spika, unakuta zile nyenzo kuu *instrument* za kusimamia uchumi wetu Waziri wetu wa fedha hana. Utayakuta kila pahala, ukiangalia ille orodha ya yale mambo ya Muungano yaliyokuwepo katika nyongeza ya kwanza pale mengi ni mambo yanayogusa uchumi. Wakati uendeshaji wa uchumi wenyewe si suala la muungano. Ni kama vile dereva umepewa gari, umepewa usukani, umepewa na *break*, lakini *klatch* na gia hui-*control* wewe, huwezi kuendesha gari Mhe. Spika. Ndiyo ilivyo kwa Mhe. Waziri wetu wa Fedha wa Zanzibar.

Nilikuwa nasema hili hebu akija Waziri wetu wa Fedha atusaidie. Lakini hapo hapo Mhe. Spika, nasema katika nyenzo hizi tutizame vizuri sana huu muundo wetu wa Muungano na sijui kama pia na hili tutaambiwa tusubiri Katiba au hapa katikati panaweza pakafanyika marekebisho. Mimi namtegemea rafiki yangu Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Raisi Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa jinsi alivyotuonesha nategemea ndani ya miaka mitano ya serikali hii atuoneshe mabadiliko.

Mhe. Spika, Katiba mpya inayokuja 2014 mwaka mmoja kabla ya uchaguzi. Hizi *power* tulizotegemea awe nazo ili asimamie vizuri uchumi wetu, kweli atakapokuwa hana kipindi chote ataweza kutuletea mabadiliko na zile sera ambazo juzi tu Mhe. Nassor Mazrui hapa kazieleza kwa kina katika hotuba yake ya Biashara. Mengi miye nikiyatizama nakuta mambo ambayo baadaye tutakutana na vigingi. Kwa sababu ndani yake kuna maamuzi ya kisera ambayo hayapo katika uwezo wetu.

Mhe. Spika, naomba vile vile Waziri wa Fedha akija anisaidie. Wenzetu wamedhibiti zile *instrument of running the economy.* Moja wapo kwa mfano ni suala zima la Soko la Hisa *(stoke exchanging)*. *Stoke exchanging*, iliyokuwepo ni moja, tulitegemea kwa sababu masuala haya wameyadhibiti wenzetu, kwa

hivyo Kampuni ambazo zingeruhusiwa kuwa *registered* pale, zingekuwa zote za Zanzibar na za Bara. Kwa sababu tunategemea kila nchi inaheshimu kwamba nchi ya mwenzake inayounda muungano huu inao watu ambao wanasimamia vizuri usajili wa makampuni. Lakini njoo utizame Mhe. Spika, kampuni ya Zanzibar hairuhusiwi kujisajili katika *Stoke exchanging* iliyokuwepo Bara. Inatakiwa mpaka iyende ikabatizwe, iyandikishwe upya Bara ndiyo iruhusiwe kujisajili katika Soko la *stoke exchanging*. Vitu kama hivi havisaidii kweli kujenga uchumi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, kama nilivyosema mambo haya ni mengi. Lakini jengine nafurahi niliwahi kulitolea kauli humu ndani, nashukuru Mhe. Waziri wa Nchi anayeshughulikia Fedha ameshalitolea kauli humu ndani, nimefurahi na nataka nimpongeze kwa hilo. Ni juu ya suala zima la kusimamia, kwa kipindi hiki angalau kwa yale mambo ambayo siyo ya muungano, basi ule utaratibu wa kuwa na mahusiano ya moja kwa moja na washirika wa maendeleo, ili kuombea miradi yetu fedha hasa ile ya kisekta auanzishe kwa Zanzibar ili Zanzibar iwe na mfumo wake wa *consultative group city meeting.*

Nataka nimpongeza sana kwa hilo kwa sababu naamini yale ambayo hata Mhe. Salmini jana alipokuwa akisoma ripoti ya kamati aliyagusia. Kwamba kuna miradi mingi ya kisekta ambayo hatuipati ni 4.5% tunaweza kuipata kwa njia kama hiyo.

Mhe. Spika, hapo hapo naomba nigusie suala zima la Tume ya Pamoja ya Fedha. Wazanzibari tumefika pahala tumeshachoka na haya matusi ya reja reja. Mara nyingi tukisema vyombo vya habari tunakutia kauli za baadhi ya wanasiasa wa upande wa pili wakisema kwamba Zanzibar haichangii shughuli za Muungano. Lakini Katiba ya Jamuhuri ya Muungano imeweka wazi nadhani katika kifungu cha 133. Kwamba kuna *account* ya pamoja na fedha, ambayo itasimamiwa na Tume ya Pamoja ya Fedha na mnahitaji na muwe mahesabu ya sawa sawa, kwamba vyanzo vya fedha vya mungano ni vipi katika taasisi ya mujngano na nani anapaswa achangie nini katika hili.

Mhe. Spika, aliwahi kusema kwamba iliwahi kuwepo ripoti ya *Private House Coopers* hawa ni kampuni ambayo kuwa imekodiwa kufanya kazi ya *consultancy* kwa tume hii ili kusaidia kuainisha gharama na mapato ya taasisi za Muungano. Yakaonesha kwamba taasisi za Muungano zinapata zaidi kuliko mahitaji yanachotumia katika taasisi za Muungano. Kwa hiyo badala ya Serikali hizi mbili pengine kuwa zinachangia zingepaswa zipewe mgao kutokana na faida zinazotokana na taasisi zile.

Nilikuwa naomba Mhe. Waziri wa Fedha pia atwambie hii ripoti itaendelea kukaliwa mpaka lini. Nakumbuka mara moja aliwahi kutujibu hapa kwamba serikali ya Zanzibar ishaikalia na imeshatoa mapendekezo yake. Hawa upande wa pili mpaka lini tutaendelea kuwavumilia?

Mhe. Spika, na wao mimi Napata wasi wasi kwamba hawataikalia kuifanyia maamuzi? Kwa sababu wakikalia kuifanyia maamuzi ndio itakaporudi katika ule mfumo wa kuinufaisha Zanzibar na wenzetu hawataki kuona Zanzibar inanufaika katika Muungano huu.

Mhe. Spika, nikitoka katika masuala ya muungano sasa naomba kidogo nigusie masuala yetu hapa ya ndani. Kwanza naomba katika kitabu cha Mhe. Waziri hotuba yake aligusia suala la mradi huu wa *E- Government*. Mimi naomba niseme mapema kabisa mradi huu mimi unanipa mashaka kidogo. Kwa nini unanipa mashaka?

Mhe. Spika, kwa maumbile yake kwa *nature* yake mrada wa serikali inayoendeshwa kwa njia za kisasa za ki- *electronic* kwa mawasiliano, ningetegemea ungekuwepo katika Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu. Lakini umetajwa kwanza katika hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kwa maana ile *E-Government* nilitegemea kwamba pale ni ndio mahala pake, kwa sababu huyu ndio anayesimamia suala zima la mahusiano na mawasiliano ndani ya serikali.

Mhe. Spika, tukaja tukasikia katika hotuba ya Waziri wa Mawasialiano na Miundombinu kwamba suala la mkonga wa taifa wa *fibre optic* linasimamiwa na wao kama waratib. Lakini leo katika hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha naikuta pia na yeye anatwambia Wizara yake inasimamia utekelezaji wa mradi wa *E–Government*. Sasa tunajiuliza mradi huu hasa Mhe. Spika, mwenyewe nani?

Mhe. Spika, nasema haya kwa sababu kuna taarifa na namuomba Waziri akija katika hili anisaidie, tena ajiratayarishe Mhe. Spika, anipe maelezo ya kina kwamba mradi huu unaharufu si nzuri. Nikiangalia kitabu hiki cha *estimate* kwenye miradi ya maendeleo, nadhani ukurasa wa 659. Mradi wa *E-Government* unaukuta umetengewa mchango wa SMZ ni milioni 20 na *Foreign lones* ni 30 bilioni.

Mhe. Spika, hapa kidogo napata wasi wasi, kuna taarifa naomba Waziri akija anisaidie kwamba Zanzibar tumeingizwa katika mkopo huu au deni hili la 30 bilioni pasi na haja. Zipo taarifa ambazo naomba Mhe. Waziri akija anisaidie. Serikali ya Jamuhuri ya Muungano katika mradi wa Mkonga wa Taifa tayari

ilikuwa kuna *component* ya Zanzibar ya milioni 20. Ukifanya *exchange* ya haraka ni hizi hizi bilioni 30. Nastajabu kwamba tumeziacha zile ambazo ndio *component* yetu, tumekwenda kuingia katika mkopo unaoiingiza nchi katika deni kwa 30 bilioni.

Mimi nilitegemea kwa mradi mkubwa kama huu pia katika hotuba ya waziri akija atufafanulie huu mradi wa *E-Government* kilichomo ndani yake ni nini? Lakini tangu hotuba zimeanza inazungumziwa mstari moja tu, utekelezaji wa mradi wa *E-Government*. Wasi wasi wangu ni kwamba kama bila ya kujua nini *component* za mradi huu katika awamu zake tofauti, tutapata mashaka. Mimi nasikitika sitolipitisha fungu hili la 30 bilioni na hisi milioni 200 za SMZ.

Mhe. Spika, kama mradi huu unahusu *fibre optic* tunavyoambiwa kutokana na *experience* zinazoendelea kwa wenzetu Bara na kuendelea kuutandika mkonga wa taifa ni kwamba gharama zote wanazozihitaji kwa kilomita moja ni kama dola 10,000. Hiyo ni kuchimba na *material* zake na faibar obtic yake. Kwa Zanzibar wanasema ukitaka kuvizungushia visiwa vyote *fibre optic* basi labda uwe na kilomita 400. Hiyo ukifanya wastani kwa thamani kubwa zaidi kuliko zote ya dola 10,000 kwa kilo mita basi unazungumzia kama dola milioni 4. Hilo unachukua kiwango cha juu kabisa. Sasa unajiuliza wapi dola milioni 4, wapi bilioni 30, kuna nini hapa?

Mhe. Spika, katika suala hili kuna taarifa na naomba Waziri wakija hapa anithibitishie. Tena kama nilivyosema asije na yale maneno yake ya kutwambia ndugu yangu sijui nani nani. Katika hili tunataka maelezo ya kututosheleza tena katika hili namuomba asilifiche Baraza. Kuna taarifa kwamba mradi huu ni mradi wa watu fulani.

Ndio maana kabla hata haujatiwa saini taarifa nilizonazo mradi huu umetiwa saini mwezi wa Mei, huu mkopo. Lakini zipo taarifa kwamba kabla haujatiwa saini tayari kumeletwa vifaa hapa Zanzibar na vikaombewa msamaha wa kodi kwa ajili ya mradi huu.

Naambiwa kuna Kampuni ya Kichina inaitwa *ZTE*. Mhe. Waziri atwambie alitoaje msamaha wa kodi kwa mradi ambao serikali hata haijafika kusaini. Mhe. Spika, vifaa hivi vimetolewa katika Bandari ndio maana nikasema kuna nini hapa katika mradi huu? Na kwa nini udhibitiwe na Wizara ya Fedha?

Mhe. Spika, kama nilivyosema mimi fungu hili nitalizuia mpaka nipate maelezo ya kina kabisa. Nampenda sana rafiki yangu, kaka angu, Mhe. Omar anatoka Vikokotoni, mimi natoka Mwembetanga sote watoto wa Mji Mkongwe. Hapa tumekuja kusimamia fedha zawalipa kodi wa Zanzibar.

Haiwezekani tukawaingiza watu wetu katika deni kubwa hili tukaacha fedha ambazo zilikuwepo na *component* ya Zanzibar ilikuwepo halafu sisi tujiingize katika hili.

Mhe. Spika, kama yeye ana maelezo na mwengine yeyote katika serikali au Wizara ya Mawasiliano watwambie, kwa nini mradi huu unaranda randa. Mimi ningetegemea kwamba kwa kuanzia hapa katika utekelezaji basi suala zima lile la kutandika ile *fibre optic* kuona kwamba nchi yetu inakwenda vizuri.

Mhe. Spika, mwisho kabisa naomba waziri akija anisaidie suala hili la fungu la safari lilokuwepo katika wizara yake. Mhe. Spika, ukurasa wa 221 wa kitabu cha *estimate* fungu la safari za ndani, za nje na malipo ya *visa* kwa Wizara ya Fedha chini ya Idara ya Utawala na Huduma ni bilioni 4,491,280,000. Mhe. Spika, kuna wizara nzima bajeti zao zote hazikupewa bilioni 4, Wizara ya Fedha fungu la safari peke yake ni bilioni 4. Kwa hivyo, naomba na mimi napenda kusafiri, lakini sidhani kwa gharama ya bilioni 4.

Kwa hivyo, nilikuwa namuomba Mhe. Waziri akija hapa anipe maelezo na akija akinambia kaka yangu kwamba haya yanahusu ofisi zile za viongozi nitamuhoji mimi kwa sababu kila ofisi ya kiongozi imeomba fungu lake na baada ya kupewa maelezo tukaridhika ndio tukapitisha. Kwa hivyo, hili kubwa sana Mhe. Spika, kidogo mimi naliombea maelezo tena ya kina kama ndio tunakwenda kutembeza bakuli huko basi aje aniambie Mhe. Waziri wa Fedha. Mhe. Spika, samahani kidogo kuna suala moja ilikuwa nimeliacha muhimu unajua nilipoingia ukaniambia tu sasa hivi zamu ya Mhe. Jussa. Mhe. Spika, naomba kwa ruhusa yako nimalizie suala moja dogo nalo ni suala zima nimeligusia kidogo hapa, lakini nimegusia katika muhtari wa mradi wa umoja. Kuhusu suala zima la misamaha ya kodi.

Mhe. Spika, niliwahi kusoma katika gazeti la *Citizen* kama mwezi mmoja uliopita na ingelikuwa sikuzongwa na mambo mengi ilikuwa nataka niitafute ile ripoti katika *internet* kwa sababu ipo. Kuna watafuti fulani wamefanya utafiti ambao baadae ulichapishwa katika gazeti la *Citizen* kwa ufupi juu ya mapesa yanayopotea Tanzania kupitia misamaha ya kodi, walisema kama sikosei kama trillioni 1 na zaidi kwa mwaka mmoja zimepotea Tanzania. Mhe. Spika, katika taasisi ambazo zimetajwa mle ndani kwamba zimechangia au zinatoa hii misamaha ya kodi holela moja ilitajwa ni *ZIPA*.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, *ZIPA* ni mamlaka inayosimamia vitega uchumi katika nchi yetu, na sote tunathamini kazi ambayo wanaifanya. Lakini Mhe. Spika, mimi ninavyoelewa katika nchi takriban zote mwenye dhamana na madaraka ya kusamehe ushuru au kodi ni Waziri wa Fedha wa nchi husika. Kidogo hili

likanistaajabisha nikasema hivi Mkurugenzi Mkuu wa *ZIPA* ana mamlaka ya kusamehe kodi? Mhe. Spika, sijapata nafasi ya kuiangalia sheria zile lakini namuomba waziri akija hapa anisaidie kama sheria ya *ZIPA* inatoa mwanya huo basi tuuzibe, la kama haitoi kama ni utaratibu wa kiutawala tu Mhe. Spika, naomba suala hili lirejeshwe katika mamla ya waziri muhusika.

Mhe. Spika, kwa muda mrefu sana watu wamekuwa wanalalamika huku tunahangaika sisi kunusuru fedha chache za walipa kodi, lakini huku watu wanatumia vibaya misamaha ya kodi na matokeo yake kunakuwa na upotevu mkubwa sana wa fedha. Mhe. Spika, nataka nimpongeze Waziri wa Fedha katika hili kwa sababu katika hotuba yake ya bajeti mwenyewe alitwambia kwamba kiasi gani amepunguza mapato kutokana na kupunguza misamaha ya kodi, hilo nampongeza na namuomba aendelee na hilo. Lakini na huu upenyo mwengine wa *ZIPA* tumuombe Mhe. Waziri aufunge ili mamlaka haya adhibiti yeye, yeye ambaye anakuja kuwajibika hapa kwetu sisi tujue kwa kumbana kwamba kuna upotevu wa fedha zetu.

Mhe. Spika, na hapo hapo kwenye *ZIPA* niseme nadhani sheria hii ya vitega uchumi kwa Zanzibar imepitishwa muda mrefu, sasa hivi Zanzibar tangu umeingia uongozi mpya wa awamu ya saba inaonekana imekuja na kasi kubwa sana kutaka kuifanya Zanzibar ijenge uchumi wa kisasa kwa haraka. Mhe. Spika, katika hilo hatuwezi kuepuka suala zima la vitega uchumi sasa katika hali hiyo Mhe. Spika, nadhani tunahitaji kujitazama upya, kwani siku hizi ushindani umekuwa mkubwa katika eneo hili, kila mmoja anataka kuwavutia wawekezaji waende kwake, hebu tuipitie tena hii sheria tuone nguvu zipi tuziimarishe ili na sisi tuweze kusimama miongoni mwa nchi nyengine kuvuta wawekezaji waje kuekeza kwa wingi hapa, walete miradi ya kiuchumi izalishe ajira, azalishe mapato na nchi yetu iweze kusonga mbele.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo sitoipitisha bajeti hii nasikitika sana kwa sasa mpaka Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo atakapokuja kunipa maelezo ya kina kwa yale masuala niliyoyaulizia hasa suala la hii *government*. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Mussa Khamis Silima: Mhe. Spika, mimi sina mchango mkubwa sana na wala sitaki kurejea hayo ambayo mwenzangu tayari ameshayasema. Mhe. Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa hiyo nafasi na kukushukuru wewe pia, lakini jengine mimi nije katika hiki kitabu cha Mhe. Waziri nimejaribu kuangalia sana lakini kuna humu sikuliona na limekuwa likilalamikiwa sana, suala hilo ni suala la kodi ya kukuza ujuzi.

Mhe. Spika, ninachojua mimi ni kwamba kodi hii inatokana na waajiriwa wa serikali na wale wa sekta nyengine za binafsi nadhani wanakatwa asilimia 5 ya sehemu ya mishahara yao. Kwa hivyo, kodi hii ikikusanywa kila mwezi inafanya jumla ya shilingi kama milioni 350, fedha hizi madhumuni yake ilikuwa ni kuzipeleka kwenye Chuo cha Mafunzo ya Amali, lakini kwa bahati mbaya chuo hiki hadi wakati huu hawajazipata fedha hizo. Kwa hivyo, wanakwama na kutatua matatizo yao mbali mbali ambayo wanayo, na sio kwa kutatua matatizo yao tu pia kwa kuwasaidia zile taasisi nyengine zilizofanana na hii ya mafunzo ya amali.

Mhe. Spika, nadhani kutokana na hilo tatizo nimekuwa na wasi wasi hapa humu kwenye kitabu sikuona kwa hivyo labda Mhe. Waziri naomba pale atakapokuja kutoa majumuisho yake basi atupe ufafanuzi wa hili suala la hizi fedha ziko wapi na zinafanya nini. Kwa sababu wahusika walipokwenda kuulizia wakaambiwa watoe mchanganuo jinsi ya hayo matumizi yatakayofanyika, lakini kwa bahati mbaya mchanganuo ule wa matumizi wameupeleka na hadi leo hii hawajafanikiwa kupata fedha hizo. Kwa hivyo, namuomba Mhe Waziri atakapokuja kutoa majumuisho yake atueleze fedha hizi ziko wapi na kwa nini hazikuwafika hawa walengwa. Kwa hivyo, hilo ndio kubwa.

Mhe. Spika, mimi sitaki niseme mengine labda nijalize kidogo kwenye suala la pencheni pale. Nimeona kima cha chini cha pencheni kilikuwa ni shilingi 25,000 Mhe. Waziri anasema baada ya marekebisho yatakayofanywa huko basi na ZSSF marekebisho hayo yatasababisha kima cha chini cha pencheni kiwe ni shilingi 40,000. Kwa hivyo, hiyo ni kima cha chini, lakini haikuelezwa kima cha juu cha hiyo pencheni kitakuwa vipi ili kujua kwamba baada ya hawa wa chini na wengine wa juu nao vile vile watapata hiyo ziada ambayo imeongezwa na wizara yake.

Mhe. Spika, jengine niseme kwamba katika kitabu hiki nimeona kuna mipango mizuri ambayo imeandaliwa baadhi ya ukusanyaji wa mapato. Kwa kweli hii yote inahitaji usimamizi wa hali ya juu kabisa ili kweli fedha hizi za wavuja jasho ziweze kupatikana na kuweza kutumika kwa shughuli ambazo itakuwa zimepangiwa.

Mhe. Spika, kuna sehemu mwingi kunavuja vuja mfano kwenye Wizara ya Habari na Utalii sehemu hiyo ya utalii, pengine na bandarini na sehemu nyengine. Mhe. Spika, hapa nimuombe Mhe. Waziri kwamba ajenge mikakati madhubuti pamoja na hii ambayo imeshaandaliwa kweli iwe na usimamizi wa dhati kuona kwamba uvujaji wa hayo mapato haupo. Nimesema kwamba mimi sina michango mikubwa na kubwa lilikuwa lile ambalo nimelisema mwanzo.

Kwa hivyo, naomba niishie hapo na kuwapisha wenzangu ili waweze kuchangia na wao, ahsante sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nikushukuru kunipa nafasi hii kuweza na mimi kuzungumza machache sana katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Mhe. Spika, mimi kwanza nataka nianze moja kwa moja kwenye hotuba hii kwa kuwa na mashaka mengi kidogo, na mashaka yangu mengine yanatokana na maeleozo ya Mhe. Waziri lakini mengine yanakuja kutokana na hali halisi inavyojitokeza.

Mhe. Spika, mimi kwanza kama Mhe. Waziri hajanipatia maelezo yakutosha nitaomba kwamba akajiandae ili atueletee maelezo ya kutosha na sababu zangu ninazo. Mhe. Spika, Wizara ya Fedha ndio baba na ndio mama wa serikali mambo yote baadae yanabebwa na Wizara ya Fedha, hata wizara nyengine tulipokuwa tunapitisha kuna baadhi ya mambo tulikuwa tunataka ufafanuzi zaidi kwa Mhe. Waziri wa Fedha. Ndio maana nikasema kwamba katika hoja zangu nitakazozizungumza nitaomba sana Mhe. Waziri aje atujibu kama alivyotujibu Mhe. Waziri wa Biashara ali-*point* sana buti zetu, vyenginevyo nitamuomba tena Mhe. Waziri akakitie nyama hiki kitabu, mimi nafikiri muda bado mnao. Aidha, tutaipitisha bajeti hii hata ikiwa siku ya Jumatatu.

Mhe. Spika, mimi nataka nianze na ukurasa wa tatu kifungu Nam. 5 naomba ninukuu kidogo. Mhe. Spika, ofisi ya Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ina majukumu ya kitaifa na yale ya kisekta, utekelezaji wa majukumu haya ofisi inaongozwa na ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ikiwa mimi sasa hivi Mhe. Spika, ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa. Kwa hivyo, Mhe. Waziri anatekeleza ilani ya uchaguzi ya mwaka 2010, lakini vile vile dira ya maendeleo 2020 na MKUZA II na malengo ya millenium na maelekezo mbali mbali ya Baraza la Mapinduzi na miongozo ya Baraza la Wawakilishi ikiongezwa na Katiba ya nchi na sheria za kodi za fedha na manunuzi ya mitaji ya umma na uwekezaji nchini. Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Waziri kwa kuiandika *paragraph* hii na hiki ndio ambacho tunachokitekeleza sasa hivi.

Mhe. Spika, mimi nataka nianze katika ukurasa wa 56 katika mchanganuo. Mhe. Spika, Mhe. Waziri hapa katika paragraph 108 (1) kuna matumizi ya kawaida halafu (2) matumizi ya kazi za maendeleo na mfuko mkuu wa serikali. Mhe. Spika, mimi nakuja katika suala zima la hii Nam. 1 inayosema kwamba kuna matumizi ya kawaida kuna bilioni karibu 47, kuna mishahara bilioni 1.90, OC bilioni 11.61, ruzuku za taasisi bilioni 14.0 na marekebisho ya mishahara bilioni 19.43.

Mhe. Spika, maelezo yake ya ufupi Mhe. Waziri hayajanitosheleza na nina sababu zangu za msingi. Mhe. Spika, mpaka sasa hivi katika maelezo ya Mhe. Waziri wa Utumishi wa Umma katika kuboresha maslahi na mambo mengine tunashukuru serikali imeongeza angalau japo asilimia 25 kwa hiki kidogo ambacho tulichokuwa nacho. Lakini Mhe. Spika, bado katika maelezo tunaambiwa serikali imo katika mchakato wa kuangalia na kuhakiki wafanyakazi wote wa serikali. Kwa hivyo, ina maana mpaka sasa hivi Mhe. Waziri wa Fedha inaonesha hajajua idadi ya wafanyakazi wote wa serikali. Hapa ndio ninapokuwa nina mashaka, na hili ninaliunganisha katika hiki hiki kifungu 1 haya marekebisho ya mishahara 19.43.

Mhe. Spika, mpaka leo hatujajua idadi ya wafanyakazi ina maana tunalipa mishahara bila ya kujua tunachokilipa. Kwa hivyo, hapa ndio maana nikasema kwamba Mhe. Waziri atueleze serikali ina wafanyakazi wote wangapi? Na haya marekebisho ya mishahara pia tunataka tuje tupate *breakdown* yake. Mhe. Spika, hatuwezi tukaletewa fungu la jumla jumla bila ya utaratibu.

Mhe. Spika, nikija katika ruzuku za taasisi naomba nikisome hiki kifungu cha 108 ukurasa huu wa 56. Anasema kwa upande wa matumizi Ofisi ya Rais Fedha na Uchumi na Mipango ya Maendeleo iliomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 174.86 ambazo bilioni 47.2 ni kwa matumizi ya kawaida ikiwemo ruzuku kwa taasisi nyengine. Mhe. Spika, ndio tunaposema kwamba wakati mwengine Mhe. Waziri anaweza kuona kama tunamlaumu lakini tatizo lake hapa hakuwa muwazi, kwa hiyo ina maana hiki kitabu kimefumbwa sana hakikuwa wazi.

Mhe. Spika, unaposema turuhusu bilioni 47.2 kwa matumizi ya kawaida halafu ikiwemo ruzuku hapa ndio tunapokuwa na mashaka. Tulikuwa tunataka kitabu chake kieleza shilingi ngapi zitakuwa kwa matumizi ya kawaida ya ile ofisi na shilingi ngapi zitakuwa za ruzuku kwa ajili ya serikali na hizo ruzuku zenyewe ilikuwa tupate *breakdown.* Mhe. Spika, hoja yangu katika hizi *breakdown* inakuja hapa leo tumekuwa na mashaka makubwa katika manunuzi kwa sababu ukiangalia Wizara ya Fedha kama nilivyosema ndio wizara mama imekuwa kama pweza ana mikia minane, kila pahala mkia wake unakwenda.

Mhe. Spika, haya maelezo ya ruzuku ya bilioni 14.8 kama hayajaelezwa kwa ufafanuzi ndio pale wakati mwengine matumizi yanafanyika kinyume na utaratibu mzuri. Mhe. Spika, tumeshuhudia hivi karibuni kuna manunuzi mengi yanafanywa, yanafanywa manunuzi yanapelekwa katika taasisi husika lakini ile taasisi husika wenyewe haijui, haijajiandaa matokezeo yake vifaa vile vinakwenda mpaka vinaharibika.

Mhe. Spika, kuna suala zima la ununuzi wa *generator* la air port. Mhe. Spika, *generator* hili limenunuliwa limepelekwa tu lakini linafika linakaribia ku-*expire* halijaungwa na ndio maana tukawa tunasema Mhe. Spika, sasa hivi tunataka tuinyanganye hii ruzuku Wizara ya Fedha, hizi ruzuku kila wizara ifanye matumizi yake kwa sababu huko nyuma tulikuwa tuna wasi wasi labda kila taasisi ikiwa inanunua, lakini sasa hii ku-*centralize* masuala yote ya manunuzi kwa taasisi moja matokeo yake imeanza kutujengea mashaka. Kwanza tunataka maelezo *generator* lililoko *air port* limenunuliwa kwa utaratibu gani, taratibu zilifuatwa na kwa nini mpaka leo limekaa halifanyi kazi.

Mhe. Spika, sio hivyo tu ukiangalia hata hili generator letu la Baraza la Wawakilishi. Mhe. Spika, limenunuliwa generator pia tunaomba maelezo utaratibu ulionunuliwa generator hili mpaka likaletwa hapa. Mhe. Spika, masuala kama haya yanapokuwa mengi ndio pale yanapoleta masuala mengi kwa wananchi. Kwa hivyo, Mhe. Spika, kitu ambacho ninachokitaka Mhe. Waziri aje atuletee *breakdown* ya ruzuku kwa taasisi zote zilizopangwa ili tujue hii bilioni 14 inakwenda wapi na wapi, vyenginevyo ndio pale niliposema ina maana hiki kitabu bado kitakuwa hakijakamilika. Lakini vile vile na hii bilioni 19 tunataka tuje tupate *breakdown* ya hiyo nyongeza ya mishahara na ndio maana pale tukasema hii mishahara unaweza ukasema ni mishahara hewa, kwa sababu kama unalipa mishahara kila mwezi na sasa hivi tunatulipa kwa kutumia benki kwa nini mpaka leo tuseme hatujui wafanyakazi tuliowaajiri.

Mhe. Spika, ndio maana pale tunapojenga mashaka, na mimi juzi nilijenga hoja mpaka nikataka kuunda tume kwamba sasa hivi mpaka wanafunzi wako vyuoni wanaajiriwa. Ndio hapa tunaposema serikali haijui wafanyakazi wake ni wangapi. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nataka maelezo ya kina vyenginevyo mimi bajeti hii sitoikubali.

Mhe. Spika, nataka nije katika mradi wa *E-Government*. Mhe. Spika, hapa sio harufu, hapa dalili ya rushwa ipo haiwezekani kuna mradi huu tayari Jamhuri ya Muungano mpaka sisi kipindi kile tulikwenda tukawakuta wenzetu wameshaanza utaratibu wanachimba kwa ajili ya mkongwa wa mawasiliano Na mradi ule Mhe. Spika, ulikuwa utakuja na Zanzibar, Serikali ya Zanzibar ingeliokoa mamilioni ya fedha ambazo sasa hivi tumeshatia saini mkataba kwamba tutaingia sisi. Kwa nini tusisubiri huo muda mchache ili tukaja tukapata huo unafuu.

Mhe. Spika, mradi huu kila mtu anautaja kwenye kitabu chake kweli *E-Government* ni *coordination* ya wizara zote, lakini sasa kwa nini kila mmoja na halafu kitu kibaya zaidi kama alivyosema Mhe. Jussa. Mhe. Spika, vimeanza

kununuliwa vitu vikaletwa hapa mpaka Waziri wa Fedha mwenyewe tunamuuliza vipi bwana mkubwa mali pale itaoza *air port exemption* atwambia ya mali gani? Mhe. Spika, yeye kama Waziri wa Fedha, Wizara ya Fedha imenunua vifaa waziri hujui ni lazima tuwe wawazi.

Mhe. Spika, mimi juzi nilipokuwa kinichangia bajeti ya Mhe. Waziri wa Utumishi wa Umma mliniona mbaya niliposema kwamba mshahara ulioongezwa asilimia 25, mimi huwa nina sababu zangu nyingi najua serikalini pesa zinakuwa zipo, lakini kwa kuwa hatuna mipango makini na mizuri yakuweza kutumia pesa hizi matokezeo yake wafanyakazi tunawalipa kidogo, lakini halafu sisi huku baadae watu wanafanya njia nyengine za ajabu ajabu. Kwa sababu matumizi mengi hayaji katika utaratibu, matumizi mengi yanakwenda kinyume na taratibu.

Mhe. Spika, pamoja na maelezo yote Mhe. Waziri aje atueleze tarehe gani viliagiziwa vifaa vile na mkataba saini umetiwa lini na yeye *exemption* amelipa lini. Mhe. Spika, hapa kama hatujaridhika tume tutakuwa nayo tupate *document* zote hizi kwa sababu kuna mambo mengine yanakuwa yakuficha ficha. Kuna mambo yanakuwa yanafichwa halafu baadae yanakuja kuwekwa sawa.

Mhe. Spika, katika suala la Mradi wa *E-Government* nilikuwa najaribu kuzungumza hilo. Lakini nakuja katika *ZSSF* kwanza tunawapongeza kwa kuangalia hatma ya wafanyakazi wetu, lakini pia nilikuwa nina masuala mawili matatu nitahitaji nipate ufafanuzi kidogo. Mhe. Spika, tulikuwa tunataka ufafanuzi wa ukodishwaji wa hoteli ya *Clove Inn* je, inaleta faida? Na huyu mwekezaji anakodishwa kwa muda gani na vipi analipa vizuri? Ili tupate angalau taarifa za kuweza kujiridhisha katika suala hili la *ZSSF*.

Mhe. Spika, nataka nije *ZRB* kwanza tunawapongeza kwa kazi nzuri ambayo wanayoifanya ya kukusanya mapato na kila siku wanazidi malengo. Mhe. Spika, lakini bado nataka kusema makusanyo yanayokusanywa na ZRB bado ni madogo pamoja na kuwapongeza kwamba wanavuka malengo lakini makusanyo bado madogo. Mhe. Spika, hapa tunaishauri serikali.

Mhe. Spika, ni kwamba utaratibu sasa hivi wa kulipa malipo kupitia pesa mkononi umeshapitwa na wakati. Mhe. Spika, sasa hivi kitu ambacho tunachokitaka malipo yote yalipwe kupitia njia za benki, tunashukuru Benki yetu ya Watu wa Zanzibar inafungua matawi kila pahala ili kuondoa usumbufu kwa ajili ya wananchi na pia fedha za serikali.

Mhe. Spika, sisi tunapokwenda katika nchi za wenzetu kila kitu hakuna kwenda na pesa mkononi unakwenda benki unalipa baadae unapata risiti yako ya

umiliki au ya kufanya shughuli zako. Kwa hivyo, ndio maana mimi siku nilipokuwa nachangia bajeti ya Wizara ya Fedha nikasema kwamba tunataka ije sheria ile ya rushwa ili tuangaliwe sote nikiwemo na mimi mali ninazomiliki, na kipato changu na mamlaka iwe na uwezo wa kunitathmini tokea nilipoajiriwa, nilikuwa nna nini na sasa hivi namiliki nini. Kwa sababu Mhe. Spika, leo wastaafu wetu tunashukuru wameongezwa kutoka posho la shilingi 20,000 mpaka shilingi 40,000.

Lakini wastaafu hawa wanatulalamikia hii posho bado ni ndogo na wanasema bado ndogo kwa nini? Anasema mimi nimefanya kazi kwa muda wa miaka 25 nyumba yangu imenishinda kujenga, lakini leo kuna vijana wameajiriwa juzi hata mwaka haujafika na hili ndio maana nikasema hasa katika sisi tuliokuwepo katika taasisi za fedha, tunatakiwa sisi tuchunjwe kwanza kwa sababu wananchi huko wavuja jasho hao wanaoijenga nchi mpaka tukafikia sisi leo wao wanaishi na hali ngumu za maisha, hata pencheni tunawapa ndogo, lakini ukiangalia vitoto vidogo vimekuja jana leo vinamiliki mali nyingi.

Mhe. Spika, nilikuwa nawapongeza *ZRB* pamoja na *TRA* vile vile. Kwa hivyo, tulikuwa tunataka utaratibu mzuri na tunaamini mapato ya serikali yataongezeka. Vile vile hapa nilikuwa naomba ufafanuzi kidogo tumepata maulizo kwa wafanyakazi wetu wa serikali wanasema sasa hivi katika mishahara yao wanakatwa asilimia 40 na wanasema zinakwenda *ZSSF*. Hebu Mhe. Waziri aje atupe maelezo kwa sababu wafanyakazi wanaona wanapata pesa nyingi lakini vile vile ukija katika uhalisia wenyewe zile fedha inakuwa kama hamna kitu.

Mhe. Spika, nakuja *ZRB* katika kitabu hiki nilikuwa naomba maelezo kuna kiwanja hiki Nam. 114 kilichoko Gulioni, hiki kipo *ZRB* wamepewa, lakini sisi sasa hivi kwa taarifa tuliyokuwa nayo mbona hiki kiwanja anacho mtu wa kawaida. Kwa hivyo, tunataka maelezo na maelezo kama hayajanitosheleza ya kiwanja hiki yale yanayokataliwa na serikali itabidi niyaombe yafanywe tena. Mhe. Spika, itabidi twende tukakague tokea barua ya maombi kama hiki kiwanja anacho mtu binafsi, kama anacho *ZRB* wenyewe sisi hatuna matatizo.

Mhe. Spika, ukurasa wa 2 kifungu Nam. 9 katika majukumu ya wizara hii wanasema kusimamia mali za serikali, ndio hoja yangu hapa nilipoijenga na hili Mhe. Spika, kuna maeneo mengi sasa hivi ya serikali watu wanayamiliki tuna hofu nayo. Mhe. Spika, mimi kuna kipindi nilisokotana na mwekezaji ndani ya Jimbo langu la Kwamtipura, kuna ghala la Kwaabasi Hussein. Mhe. Spika, Tume ya Uchaguzi ilikuwemo ndani pia imeuzwa bahati mbaya kuna wafanyabiashara pale wanauza samaki na mikate yule mwekezaji kwa jeuri yake akawafukuza nikawaambia hapa huwafukuzi, tukasokotana kweli kweli

matokeo yake mpaka sasa hivi wanauza samaki na bofulo angalau virungu kidogo vimepungua. Sasa na hili pia nina mashaka nalo uwazaji wake. Mhe. Spika, hili pia nitataka maelezo kwa Mhe. Waziri ndio maana nikasema Wizara ya Fedha ndio mmiliki wa mali zote kwa sababu kuna mitaji ya umma na mingine na hili. Lakini Mhe. Spika, tumeletewa maelezo mengi ya jengo la Mambo Msiige. Mhe. Waziri maelezo ya kwenu nyote, Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kaeleza, Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, Mhe. Waziri wa Fedha, lakini maelezo yenu bado yanatutia mashaka. Tunataka suala hili Mhe. Waziri aje na jawabu tena nzuri nyengine hata ikiwa zile zile kama hazijaturidhisha tutamwambia.

Mhe. Mspika, kwani sisi kuunda Kamati ya Baraza ikachunguza mambo yote tunayo wasiwasi nayo serikali itakosa nini? Kwa sababu kama wanaofanya mambo haya si mawaziri na sisi hapa tunaitetea serikali, tunatetea mali za wananchi.

Mhe. Spika, wenzetu Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walifika pahala mpaka kwenda London kwenda kuchunguza ununuzi wa rada, sasa sisi hapa hapa Unguja na Pemba tushindwe.

Mhe. Spika, kuna hoja nyengine, mimi nikiwa Mwenyekiti wa Kamati Inayosimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa juzi nilimsikia Makamo wa Kwanza wa Rais kenda Pemba amehoji na akataka suala hili lishughulikiwe, Mhe. Waziri hayupo hapa anayeshusiana na mazingira Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, hili suala baada ya hoja tulivyoona kwenye vyombo vya habari hoja ya Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais tunataka tukathibitishe. Kuna hoteli pale imejengwa iko Wesha, kuna matenki ya mafuta tunaambiwa hakuna *document* zozote za mazingira zinazotoa *authority*.

Sasa Mhe. Spika, hii nchi tutakuwa tunakwenda tu hivi wakati tuna sheria, katiba, kanuni tunakwenda vipi. Vitu kama hivi tunataka na sisi tujiridhishe, kama tumezowea kupeana vitu kiholela kama kuna watendaji wanaowadanganya mawaziri maana yake Mhe. Spika, unaweza ukakuta saini ya waziri, lakini yeye kutokana na shughuli nyingi mara yuko Barazani kafika kakuta mafaili katia saini, pengine huku watu wameshavuta. Sasa Mhe. Spika, haya ndio mashaka na hili sasa hivi tunataka Serikali ya Umoja wa Kitaifa iwe ya umoja wa kitaifa kweli ifanye kazi.

Mhe. Spika, sheria nyingi zinakiukwa, sasa hivi tuna sheria ya mazingira hoteli zote zinatakiwa zijengwe zaidi ya mita 30 kutoka ufukwe wa bahari. Sasa hivi kuna malalamiko mengi katika maeneo mbali mbali ya wenzetu wanaokaa katika maeneo ya uwekezaji wanalalamika wanazuiliwa mpaka kupita baharini.

Sasa hivi Mhe. Spika, kutokana na kwamba tunashindwa kuzisimamia sheria zetu watu wanajenga mpaka ndani ya bahari, maana yake ukiacha ile mita 30 ya sheria watu wanaingia mpaka ndani ya bahari, sasa hizi sheria vipi. Naomba sana twende tukaangalie majengo yote yaliyojengwa kinyume cha sheria, ndani ya bahari na halafu tuje na ripoti Mhe. Spika, kwa kuja kuyavunja *other wise* sheria tuzibadilishe ndio Serikali ya Umoja wa Kitaifa Mhe. Spika inavyofanya kazi, hakuna blaa blaa sheria ifuatwe.

Mhe. Spika, hili nitamuomba sana kwa sababu hili liko *ZIPA* na hili tulizungumza. Mimi kwa bahati mbaya siku ya Hotuba ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo nilikuwa ninaumwa, lakini nilitaka kuja kuzuia bajeti mimi, kwa nini wanaruhusu ujenzi katika bahari? Mhe. Waziri wa Habari akasema hilo silangu ni la Uwekezaji, Uwekezaji iko *ZIPA*! *ZIPA* iko kwa Waziri wa Fedha.

Mhe. Spika, wananchi sawa wameshachoka kusumbuliwa tunataka twende tukafanye tathmini ya maeneo yote yaliyojngwa ndani ya bahari tuje tulete ripoti halafu tuseme hili vunja na sio vunja tu kichwamchungwa, huyu hana barua ya mazingira, huyu hana barua ya *ZIPA*, kila mmoja sasa hivi tunataka akae kwenye mstari, vyenginevyo Mhe. Spika, ndio yale tuliyokuwa tunasema kama serikali itakuwa haituruhusu hivi basi itabidi tukae mimi nitakaa ukumbini kwangu kwa sababu siku hizi televisheni *live* nitakuangalieni nakuja kuvuta hapa, lakini sitaki hivyo nataka nifanye kazi wananchi waliyoniletea hapa.

Mhe. Spika, kuna maeneo haya ambayo nina mashaka nayo, kama nilivyosema ghala langu la Kwa Abass Hussein, *Living Stone* pale, jana nilizungumza Kiwanda cha Maziwa lakini Kiwanda cha Maziwa Mhe. Waziri alisema eneo lile sio la mwekezaji aliyepewa, lile tunavyojua sisi ni eneo la Kiwanda mpaka barabarani, lakini eneo lile sasa hivi limeshajengwa hatujui kama maeneo huru au nani, tunataka maelezo eneo lile kapewa nani.

Mhe. Spika, kuna kipindi aliyekuwa rafiki yangu Mhe. Machano Othman Said aliwahi kuliomba eneo lile akazungumza mpaka hapa Baranani kuwa eneo lile analitaka kwa ajili ya wananchi wake kujenga soko, aliomba mpaka *TASAF* asaidiwe na hilo soko lipo, wale wenye soko wameshafyekuzwa fyekuzwa pale wako nje. Mhe. Spika, leo Mhe. Waziri anasema watu wajikusanye, wajiajiri, wakishajikusanya tunawatolea nje wakafanye kazi wapi? Ndio maana kila siku tunawafukuza barabarani kwa sababu pahala ambapo wanakaa baada ya kupaboresha sisi tunawafukuza. Kwa hivyo, Mhe. Spika, eneo hilo vile vile nataka maelezo.

Vile vile nataka tuje tujue hii mikataba ya maghala ya akiba. Juzi tulipitisha sheria hapa ya Akiba ya Chakula maghala hatuna, maghala haya yamekodishwa tujue mikataba yake inamalizika lini na sisi tutafaidika vipi na hicho chakula cha hifadhi ya serikali kitakuja kuhifadhiwa wapi.

Mhe. Spika, sasa nije kwenye *Rest House* ya Pemba, kwa bahati nzuri na mimi pia nimeshawahi kulala pale. Katika Ripoti ya Ukaguzi Ofisi ya Mkaguzi Mkuu na Hesabu za Serikali nyumba ile imejengwa kwa karibu shilingi 350 milioni, Mhe. Spika, mpaka leo ripoti ya mkaguzi wa hesabu haijaridhika na haijapelekewa vielelezo vya matumizi ya ujenzi ule. Mhe. Spika, na hili tunataka maelezo tena kina kabisa.

Mhe. Spika, humu imeelezwa kuna fedha katika kitabu hiki kuna ujenzi wa Makao Makuu ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Mhe. Spika, fedha hizi tunazizuia. Kwa sababu hapa tumejenga hoja na Mhe. Spika, ulisema Kamati ya Mawasiliano na mimi ukaniingiza kama Mjumbe kwenda kukagua eneo lile lakini huku fedha zinaombwa tena na Wizara ya Fedha hizi tunazizuia kwa sababu hapa pahala pana mashaka. Eneo hili kwa mujibu wa mawaziri walivyokuwa wanagongana, waziri alisema eneo hili kapewa mwekezaji lakini hajalipa, Naibu Waziri wa Mawasiliano akasema limeshalipwa shilingi 200 milioni ziko mikononi mwa mwekezaji ziko salama. Wewe pesa ziwe mikononi mwa mwekezaji ndio ziko salama hizo, na pesa yenyewe ya serikali.

Halafu hofu yetu hapa eneo hili liliuzwa mwezi Oktoba. Mhe. Spika, oktoba si unajua inakuwa na nini 2010, ina uchaguzi. Eneo limeuzwa mpaka leo pesa hazijafika serikalini. Mhe. Spika, tutakuwa na imani gani sisi? Tupelekeni tukaangalie tukakague tupate uhalali wa mambo haya. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa mazingira yanaharibiwa vibaya. Kuna mwekezaji pale Hoteli ya Mtoni kafukia bahari hana *document* ya mazingira wala yoyote, yaani jeuri, watu wasipandie migongo yetu. Mhe Spika, na pale tunataka tukapakague, ile Kamati yako ya Mawasiliano kama utaipa kazi na kamati yangu ya leo utaipa kazi ya kwenda kukagua maeneo hayo yote niliyoyataja, eneo lile Mheshimiwa limeharibiwa vibaya, kachukua eneo la hoteli, kafukia bahari bila ya ruhusa, kaharibu mazingira, mnanidhalilishia waziri wangu wa mazingira hivi hivi, sikubali kama Mwenyekiti wa Kamati.

Mhe. Spika, nije katika *BoT*. Mhe. Spika, tunataka Mhe. Waziri atueleze hisa za Zanzibar katika *BoT*, kwa sababu katika vikao mbali mbali nimeshapigwa mateke na kwa bahati mbaya wenzetu wa Jamhuri ya Muungano suala hili mpaka leo hawajatoa jawabu. Tunataka Mhe. Waziri na kwa sababu *BoT* ndio

inayo-*regulate* fedha tena mpaka sisi kama serikali tumefungua *account* yetu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar *BoT* wakati hatuna hisa pesa tumekwenda kuzigawa hatukubali. Leo tunataka waziri kama hajatwambia hisa za Zanzibar katika *BoT* bajeti hii hatuipitishi, ndio maana nikasema kitabu hakijatimia. Mhe. Spika, usione tuna jazba tunajua mengi.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Mjumbe anapozungumza tumpe nafasi azungumze tumsikie, makofi yakiwa mengi hata mimi nashindwa kumpata sawasawa. Tutapokuja kwenye vifungu baadae atapohoji mimi nitakuwa napata tabu kwa sababu sikumsikia sawasawa. Naomba tumpe nafasi azungumze na makofi tuyapige kwa nidhamu. Mheshimiwa endelea.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, *BoT* tunataka Mhe. Waziri aje atueleze tena maelezo ya kututosheleza na leo mambo ya kuambiwa sijui *document* hazijapatikana bajeti hii hatutoipitisha mpaka tutakapopata *document* zinazoonesha Zanzibar ina hisa ngapi katika *BoT*. vile vile tunataka tujue kama tuna hiza katika Benki ya Tanzania je, kiasi gani cha faida tunachokipata kama Zanzibar kwa katika mapato yanayopatikana na *BoT*.

Lakini hapo hapo *BoT* Mhe. Spika, wakati wa mtikisiko wa uchumi duniani wenzetu kule Bara juzi Naibu Waziri wa Fedha aliulizwa na Mhe. Mbunge wa Jimbo la Chumbuni kababaika pale, kaambiwa hakuna kalete ripoti. Anasema kuna kampuni au taasisi karibu 90 zilipewa msaada ili kujiendesha katika msaada na katika mtikisiko wa uchumi. Je, *BoT* Zanzibar kuna mashirika au makampuni au wawekezaji wangapi waliopewa fedha hizi kwa ajili ya kuwasaidia ili waweze ku-*sustain* katika mtikisiko wa uchumi.

Mhe. Spika, mimi nilimuuliza Gavana wa *BoT* kipindi hicho nilipokuwa waziri wenu zamani sio leo. Nilimuuliza *Governor* je, *ZSTC* katika mtikisiko huu wa uchumi duniani kule Bara wenzetu Mamlaka ya Kahawa, Pamba, Korosho mpaka watu binafsi wamepewa pesa. Je, *ZSTC* katika mtikisiko huu mmewapa nini? Hakunijibu mpaka leo, sasa waziri nataka uje utwambie.

ZSTC walipata kiasi gani kutoka *BoT* katika fedha za mtikisiko wa uchumi dunini na wenzetu Bara wamepewa ngapi. Tunataka utuletee takwimu, wasiliana na waziri mwenzako wa fedha ndio maana nikasema Mhe. Waziri jiandae Jumatatu ili upate takwimu zote hizi. Tunataka Bara kule *BoT* wamewapa makampuni mangapi na taasisi ngapi za serikali na watu binafsi na kiasi gani na Zanzibar wafanyabiashara wangapi, makampuni pamoja na *ZSTC* shirika ambalo lilikuwa linasuasua. Karafuu walikuwa wanataka kununua pesa hawana, *BoT* pesa wanawapa watu wengine au hatuna hisa? Ndio maana nikauliza hapa.

Mhe. Spika, jengine hapo hapo *BoT* . Mhe. Spika, *BoT* wanatoa mkopo wa shilingi bilioni nne (4) kwa *SME,* yaani wafanyabiashara wadogo wadogo na wa kati, yale majengo mnayoyaona ya ghorofa Dar es Salaam yanajengwa msifikiri watu wana pesa zao ile mikopo inatoka *BoT*, Zanzibar wangapi wamepewa. Mhe. Spika, shilingi bilioni nne si mchezo, mimi nazitaka tukishafunguliwa mlango wazi tupo na sisi wa chini chini hatutaki tuwe wajasiriamali tunataka tuwe wawekezaji, *BoT* ndio ituwezeshe tuwe wawekezaji sio wajasiriamali. Watu wanarambana rambana mitaani huko kumbe fedha ziko *BoT* wanagawana wao sisi hatuna kitu.

Mhe. Spika, hili naomba, leo asubuhi wamenipigia simu wanafunzi wangu wa Jimbo la Kwamtipura wa Chuo cha Chwaka, wametaka niwasaidie wanataka kufanya mitihani wanataka kuzuiliwa, nawaambia sasa taabani hivi sasa ninasokotana na Waziri wa Fedha ili nikuwezesheni. Mhe. Spika, tunaomba wanafunzi wetu waruhusiwe kufanya mitihani, Mkurugenzi wa Chuo hapa hatusemi nae leo hapa tunasema na Spika na Waziri.Tunaomba wanafunzi wetu hao ndio wataokuja kushika hatamu baadae, mambo yale ya pencheni hamna sasa hivi tunataka hawa wasomi waruhusiwe wafanye mitihani yao vyeti zuwieni tumeshakuruhusini, mtu akija akitaka cheti chake mumpe.

Sasa hivi kwanza hawana mudi ya kufanya mtihani wameshaambiwa kama hamjalipa mtihani hamfanyi kweli watakwenda kufanya mtihani wale Mheshimiwa? Tuondoe *frustration* waliyokuwanayo kichwani ili akili ile aliyosema Mheshimiwa wa Jimbo la Micheweni akili zao zishataabanika.

Sasa mtu akili ishataabanika atakwenda kufanya mtihani vipi? Tunaomba Mhe. Waziri tunakujua mpendwa wetu, ndugu yetu, rafiki yetu, swahibu wetu, mwenzetu, tunawaombea wanafunzo sio wa Chwaka tu na wanafunzi wa vyuo vingine waruhusiwe wafanye mtihani vyeti zuwieni. Hapo tukija tukipata hiyo ndogo ndogo hivyo hivyo tutawasaidia.

Mhe. Spika, nakuja jengine. Juzi katika hotuba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa bahati mbaya nilikuwa naumwa, namjua Mhe. Waziri wa Mifugo na mambo yake mimi alinipeleka kule Gando akafanya vitu kidogo lakini rafikiri yangu yule.

Lakini Mhe. Spika, hapa tuna tatizo na hili tatizo limo ndani ya nyumba yako na ndio maana nikasema sasa hivi Wizara ya Fedha tunataka kuwanyang'anya fungu hili la ruzuku za wizara nyengine kila mmoja ashughulikie mambo yake. Sisi jengo letu kwanza bovu, sio bovu kama ni bovu, zima kweli kweli, lakini limejengwa katika mazingira ya Arabuni, kule hakuna mvua za siku zote upepo ndio mwingi sisi huku kwetu mvua kila baada ya miezi mitatu, jengo sasa hivi

linavuja. Kwa hivyo, tulilalamika lakini tukasema kwa kuwa mjenzi kwa kawaida kunakuwa na mkataba wa muda, anatoa muda ili jengo lifanyiwe marekebisho.

Juzi tumemuuliza Katibu wa Baraza mbona jengo mpaka leo halijafanyiwa ukarabati? Au ina maana hata hizo fedha za kufanyia ukarabati pia hatuna? Akasema aaa, akakurupuka nikamwambia usinifiche. Mimi nina taarifa kwamba Al-Youseif ambaye ndiye aliyetujengea jengo hili kwa kusaidiana na serikali tayari tumeshamlipa shilingi milioni mia mbili (200), pesa hizo ni *installment* ambayo ilikuwa bado *installment* mbili. Shilingi 200 milioni tumeshamlipa ambapo fedha hizi ilikuwa aje alipwe mwaka 2016 hata bajeti ya mwaka 2016 hatujapitisha huku keshalipwa.

Mheshimiwa pesa zirudishwe, pesa hizi ndio zingesaidia pengine katika kuongeza mishahara ya wafanyakazi na hizi pencheni watu wanaolipwa shilingi 40,000 leo pesa anapewa Al-Youseif. Mhe. Waziri wa Mifugo samahani sana halafu baadae ukamfagilia kwenye kitabu chako, mna mpango wa kujenga mabanda ya kuku hapa Al-Youseif hajengi mabanda ya kuku, hii miradi ni miradi ya wananchi wetu wadogo wadogo, leo Al-Youseif tajiri yule aje ajenge mabanda ya kuku wananchi wetu watafuga nini, panya? Haiwezekani.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri wa Mifugo kitabu chako kile ndio nachangia kabisa nilikuwa sipo naumwa, lakini kurasa ile mimi nimeshaichanga, haiwezekani nikaikubali bajeti tena naipigia buti kabisa hotuba ya Waziri wa Mifugo. Mhe. Waziri aje atusaidie kama anataka kuja kutotoa vitoto vya kuku vile vifaranga tutamruhusu kwa sababu wananchi wetu hawana uwezo huo, lakini kama kuja kufuga kuku kwa hapa Al-Youseif hafugi kuku aje atujengee jengo letu hapa. Mhe. Spika, mimi nasema pesa alizolipwa Al-Youseif zirudishwe vyenginvyo bajeti hii mimi siipitishi.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache la mwisho kabisa Jengo la Wizara ya Fedha lililokuwa halijulikani kama litaanguka au litafugiwa kuku au samaki. Mhe. Spika, pale aibu, tunataka Mhe. Waziri akija aje atuoneshe toka zile barua *correspondence* za kuitisha *tender*, yule aliyeshinda akaeleza uwezo wake *installment* tulivyozitoa mpaka tukafika pale.

Haiwezekani Mhe. Spika, fedha za umma zishatumika halafu tuseme kwamba hapa katika kitabu mnatuomba pesa nyengine halafu mnasema tuko katika taratibu za kwenda mahakamani mpaka leo taratibu za kwenda mahakamani? Kwa sababu kwanza tunataka tujue *installment* zililipwa kwa mujibu wa mkataba?

Mhe. Spika, sijui leo nitakuwa na buti ngapi, na nitaomba ruhusa kila nitakapopiga buti uniruhusu, vyenginevyo itabidi sasa uniachie unipe ile kazi nikakague maeneo yote halafu nijiridhishe nitakuletea ripoti iliyokuwa nzuri na wewe mwenyewe utaridhika na utahikikisha hasa ripoti yangu itasaidia kuongeza mapato kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili wananchi waweze kuishi vizuri na sisi tuweze kupata afuweni katika majimbo yetu.

Baada ya hayo machache Mhe. Spika, suala la *TRA* wenzangu acha waliogolee, Mhe. Ismail Jussa keshaliogelea, lakini bado suala la wafanyabiashara mara mbili lina matatizo. Mhe. Spika, suala hili vikao vishakaliwa vingi, mimi mwenyewe nimeshashiriki vikao kama vine.

Siku moja Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa bahati mbaya sasa hivi hayupo aliambiwa kaa kitako ndani ya kikao, kaambiwa kaa kitako unasema nini tunatetea maslahi ya Zanzibar ndio maana tukasema Mawaziri wa Zanzibar pamoja na kwamba mnasema sasa hivi mmjipanga vizuri na sisi tulijipanga vizuri hakuna chochote kilichofanyika.

Mhe. Spika, leo tunajua mzigo ukishaingia nchini bandari yoyote leo watu wetu wanasumbuliwa, watu wana jamaa zao Dubai, Oman, Uingereza wapi wanakuja na mizigo yao wanashuka KLM anaambiwa mizigo yote alipe ushuru *air port* ya Dar es Salaam, kwa nini? Kule wanatwambia aa hapa unatakiwa ulipe kwa sababu ukitua katika eneo lolote la Tanzania ushaingia ndani ya nchi unalipa mapato ya *TRA.* Sasa na mzigo ukishaingia Zanzibar ushaingia ndani ya nchi, kwa hivyo, *TRA* kodi ikishakusanywa Zanzibar ndio keshakusanya kule, kwa nini watu wetu mpaka leo wakifika bandarini Dar es Salaam wanasumbuliwa?

Mhe. Spika, hili tushachoka siasa hebu tufanyeni maamuzi magumu. Tunasema hapa tuliifukuza *SUMATRA*, *TRA* tunaifukuza na leo, mpaka katiba mpua. Kwa sababu sisi sasa hivi unajua tunampatisha tabu sana Mwanasheira Mkuu, kijana mzuri anaipenda Zanzibar, lakini sasa hivi inabidi anaanza kutujibu sio anaanza inabidi na yeye aje atujibu kisiasa. Kwa sababu hili tunajua itabidi atasimama Mwanasheira Mkuu.

Suala la *TRA* halitekelezwi kimuungano, kwa hivyo sasa hivi *ZRB* tuipe mamlaka kamili mapato yanayokusanya na *TRA* yakusanywe na *ZRB* au *TRA* wafanyakazi waliokuweko hapa tutawaajiri kupitia *ZRB.* Lakini Mhe. Spika, mimi suala hili sio leo tu, nimeshasokotana na Kamishna mwenyewe Kitilia, kwamba hana imani na Zanzibar.

Mhe. Spaika, sasa hivi watu wetu wanasumbuliwa Ramadhani hii haiwezekani vijana wetu wako vigogoni wanahangaika, kuna biashara chungunzima za kupeleka Bara wakauze wakapata riski, wakifika Dar es Salaam wanasumbuliwa. Hapa nyinyi mtasema kikao mwezi gani Waheshimiwa nyinyi kaeni vikao vyenu na sisi vyetu, sisi leo sio kama tunaifuta *TRA*, kwa sababu *TRA* makusanyo yanayokusanywa Zanziabar si yanatumika Zanzibar, tuipe mamlaka hiyo *ZRB*, *TRA* tutawapangaia utaratibu wao vyenginevyo Mhe. Spika, katika *TRA* sikubali.

Sasa Mhe. Spaika, kwa haya yote niliyoyakataa bajeti ndio ipo iyo? Haipo. Mhe. Spika, tunaomba waziri akaandike kitabu chengine cha kujibu maswali yangu yote, akaandike kitabu kwa sababu atakuja kunijibu rafu rafu mtakuja kuniona mkorofi, mimi naipenda Zanzibar.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura suing mkono hotuba hii hata kwa asilimia moja kwa sababu sijaona kitu chochote kinachowafaidisha Wazanzibari na wananchi wa Jimbo la Kwamtipura. Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunivumilia.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru sana kunipa nafasi hii na naomba kwa busara zako kama ulivyompa Mhe. Hamza Hassan dakika 30 na mimi unigaiye dakika 30, kwa sababu hii ni hotuba nzuri, kubwa na ya kitaalamu.

Mhe. Spika, kwanza kabisa mimi Hija Hassan Hija, Mwakilishi wa Jimbo la Kiwani suing mkono hotuba hii hata asilimia moja. Na sio kwamba siungi mkono kwa sababu ya utashi, nina hakika Mhe. Waziri hawezi kunijibu maswali yangu niliyonayo, atakaponijibu maswali yangu kauli yangu nitairejesha nitaunga mkono.

Mhe. Spika, suala la mwanzo nataka Mhe. Waziri anijibu hii Wizara ya Fedha ni mali ya nani? Ni mali ya Wazanzibari au ni kikundi cha watu fulani ambao kuwa ndio wenyewe Wizara ya Fedha. Kwa mtazamo wangu Wizara ya Fedha si mali ya Wazanzibari ni mali ya watu fulani na akitaka maelezo Mhe. Waziri nitampa kwamba Mzanzibari wa kawaida wa Kijini, Makunduchi, Mwambe na Wete hafaidiki na Wizara ya Fedha. Kwa hivyo, kama Wazanzibari hawafaidiki maana yake si mali ya Wazanzibari wote.

Mhe. Spika, nasema kwamba Mhe. Waziri ametuomba kwamba tumuidhinishie shilingi 19.43 bilioni kwa ajili ya marekebisho ya mishahara, hakutwambia anakusudia kurekebisha mishahara ya wafanyakazi wangapi nina hakika hawajui. Mhe. Spika, Zanzibar bado wafanyakazi hewa wapo, kwa vile wapo

na sisi ndio wasimamizi wa Wazanzibari lazima tuchunguze kwa nini wafanyakazi hewa Zanzibar wapo. Mhe. Spika, mimi ninajua majina ambayo watu wako chuoni wanasoma wanalipwa mshahawa wa *degree* wakati bado ni wanafunzi. Mhe. Spika, wakati Wazanzibari wako wengi wamemaliza skuli hawajaajiriwa tunawalipa watoto wa vigogo mishahara ambayo bado wanafunzi hii ni zambi na hatukubaliani nayo.

Mhe. Spika, mimi nasema kwamba Mhe. Waziri, Mhe. Omar Yussuf Mzee ni makini lazima akubaliane na wawakilishi kwamba Zanzibar kuna tatizo Wizara ya Fedha. Ukiangalia mafunzo yanayotolewa kwa watendaji wetu watendaji wengi wa fedha hata kwa fani ya sheria hawasomei Tunguu, Chukwani wala Tanzania Bara wanapelekwa nje, wakati mahitaji yao Tanzania yapo, Zanzibar yapo kibao lakini mwanafunzi wa sheria wa Wizara ya Fedha basi anapelekwa nje, huu ni upotevu wa mali za umma. Mhe. Spika, Wizara ya Fedha kuna tatizo.

Mhe. Spika, leo Mhe. Waziri anatwambia tumuidhinishie fedha eti akajenge jengo jengine la Wizara ya Fedha Pemba. Wallahi tutakuwa wendawazimu sana sisi wawakilishi, kama tunaidhinisha mapesa mengi jengo linaning'inia kama mkungu wa ndizi baadae wawakilishi wamuidhinishie tena wakaharibu hatufanyi kosa hilo. Nadhani Mhe. Waziri kama ni muungwana angetwambia wapi tunasikia kuna jengo limefeli kwa kutumia nadharia ya fedha sio atuombe fedha hii ni kejeli.

Mhe. Spika, mimi nawaomba wawakilishi wenzangu sana wasiidhinishe fedha kwa ajili ya ofisi ya jengo la Wizara ya Fedha Pemba, hizi fedha zitafujwa ovyo *unless* watwambie jengo ambalo limejengwa kwa nini limefikia pale na nani aliyejenga. Mimi siamini kwamba mkandarasi ndio mkosa, naamini Wizara ya Fedha ndio mkosa. Kwa nini? Kama mkandarasi ni mkosa na kuna mkataba kwa nini hahukumiwi tukapata haki yetu?

Mhe. Spika, nataka nikwambie kwamba natumia sheria nambari nne ya Haki, Kinga na Fursa za Mjumbe kifungu cha 9 kuomba kwamba mikataba ifuatayo ije hapa.

Kifungu Nam. 9 cha *Members to be furnished with Information*, kinasema kwamba:

> *"Subject to this Act and to any statute relating to security of the government, a member shall be furnished by the Public Officer Conserned, any information be requests".*

Naomba mikataba ifuatayo ije hapa ni Mikataba ya Umma Zanzibar, ije hapa tuishuhudie vyenginevyo kitabu hiki kirudi.

1. Mhe. Spika, naomba Mkataba wa Mambo Msiige uje hapa Barazani, kama kweli ni mali ya Wazanzibari uje hapa tuushuhudie.

2. Mkataba wa Ununuzi wa Mitambo ya Televisheni Pemba ije Barazani hapa tuione.

3. Mkataba wa Ujenzi wa Jengo la Afisi Pemba uje Barazani tuuone.

4. Mkataba wa Ukodishaji wa Kisiwa cha Changuu uje Barazani tuuone.
5. Mkataba wa Ununuzi wa Majenereta 32 Mtoni uje tuuone.

Mhe. Spika, ni aibu maana yake ni kuchukua umeme mdogo wanapandisha sio majenereta yale. Kwa hivyo, mkataba huu uje hapa Barazani. Haiwezekani majenereta yale 32 lakini fedha hapana na kwamba yale si majenereta lazima mkataba uje Barazani tuushuhudie.

Mhe. Spika, jengine mkataba wa matangazo ya mabango ya makampuni ya simu tunaomba uje Barazani tuuone na mikataba yote iliyofungwa kuanzia tangu siku ya mwanzo ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa ije Barazani tuione. Mhe. Spika, hayo ni matakwa ya Sheria Nam. 4 kifungu cha 9 mimi kama Mjumbe naomba mikataba ije Barazani tuishuhudie.

Mhe. Spika, jengine ni kwamba Sheria ya Kutangaza Mali haijafika lakini mimi nasema wazi kwamba nina nyumba mbili ndogo, nyumba moja nimeijenga kabla ya kuwa Mwakilishi nikiwa mwalimu sasa hivi wanakaa wazee wangu, nyumba ya pili nimejenga Unguja hapa baada ya kuwa Mwakilishi. Sasa na wenzangu nao watangaze mali zao hasa watendaji wa Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo hatuwaamini wana mali kubwa mno kuliko uwezo wao wa mishahara.

Mhe. Spika, lazima tusimamie watendaji tuangalie uwezo walioupata kwa mshahara gani wakajenge maghorofa. Mhe. Spika, leo tunawajua watu hapa wana maskuli mengi makubwa tu. Kuna taarifa kwamba kuna mtu amenunua viwanja vinane ameunganisha ukiangalia mshahara wake ni chini ya laki sita kwa uwezo gani alioupata. Mhe. Spika, lazima tuwachunguze watendaji wa Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na tabia ya kumuweka mtendaji miaka 40 si tabia nzuri. Lazima tufanye *rotation* ya madaraka, huwezi ukamuweka Mkurugenzi pahala miaka 40 huu ni ufisadi mkubwa.

Mhe. Spika, jengine ni suala zima la manunuzi ambalo mimi nashangaa, naiomba sana serikali kuanzia sasa itwambie inanunua magari kwa vigezo gani. Nchi hii ina magari zaidi ya aina 40, yapo Toyota, Mitsubishi, kila aina ya gari zipo hapa Zanzibar. Wengine wananunua gari kwa ajili ya kupata mtaji tu, wanajua gari hili siku nne hazifiki litaharibika. Kwa hivyo, utaratibu wa manunuzi ya mali za serikali lazima uangaliwe vyema Mhe. Spika, naomba sana Mhe. Waziri hili akubaliane nalo.

Mhe. Spika, juzi tumesikia mmeuza vipuri na magari mabovu UUB Pemba, mkataba umeanza asubuhi mazungumzo, barua imeandikwa mtendaji anapewa laki mbili nauli akenda Pemba jioni akapelekewa muuzaji si utaratibu kabisa. Huo ni utaratibu ambao haukubaliki kuhusiana na matumizi mazuri ya fedha za umma.

Mhe. Spika, nasema kwamba serikali hii kama kweli ipo kwa ajili ya watu lazima tuwe wawazi. Mimi najua nikisema hayo watu watakasirika lakini ndio ukweli wenyewe, ukikasirika sawa lakini ukweli wenyewe ni kwamba wananchi wapo hali ngumu sana mitaani na hatuwajali.

Mhe. Spika, jengine Wajumbe wa Bodi ya Zabuni. Mimi nashangaa Zanzibar ina wataalam wengi lakini unamchukua mwalimu wa chuo cha kur-an unamwambia Mjumbe wa Bodi ya Zabuni, hata haelewi hiyo bodi nini, hana utaalam nayo, *just* amewekwa kisiasa tu kwamba huyu atabakia hapa hana uwezo wa kuhoji. Kwa hivyo, Wajumbe wa Bodi ya Zabuni waliochaguliwe wataalam wenye sifa.

Mhe. Spika, jengine ni suala zima la daftari la mali za serikali. Mhe. Spika, Idara ya Mitaji ya Umma kwa kweli ilitoa muongozo ambao hautekelezwi, haufuatwi na kwa kweli ndio mwanya mkubwa wa upotevu wa mali za serikali. Kwa hivyo, nasema kwamba idara hii ipo zaidi ipo kinadharia na ndio chanzo cha upotevu wa mali za umma. Haiwezekani kwamba idara ipo, majengo yanachukuliwa, mashamba yanachukuliwa lakini hakuna hatua ya idara, leo waje hapa watwambie tuwatengee fedha maana yake wakale halafu watupotezee mali zetu. Mhe. Spika, nadhani hilo si sahihi.

Mhe. Spika, jengine Mhe. Waziri ametwambia hapa kwamba Benki ya Watu wa Zanzibar ina mitaji ya bilioni 15 zaidi, lakini hakutwambia *ZSSF* ina mtaji wa shilingi ngapi. Kwa hivyo, labda Mhe. Waziri akija atwambie shirika hili la umma *ZSSF* mtaji wake ni shilingi ngapi ili tuweze kuwashauri vizuri kwenye uwekezaji hapa Zanzibar.

Leo Mhe. Spika, tuna matatizo ya umeme, tuna matatizo ya maji, kama wenzetu hawa wangekuwa na nia nzuri na mtaji wao ni mkubwa kwa nini wasiwekeze badala yake wananchi wahangaike kwa umeme na masuala ya maji.

Mhe. Spika, jengine ni majenereta ya msaada ya *UNICEF*. Mhe. Spika, mwaka juzi hapa tulipata shida ya umeme miezi mitatu, wafadhili wetu *UNICEF* wametusaidia zaidi ya majenereta 12 leo yako wapi watu wamegawana kama njugu. Mhe. Spika, tunaomba Mhe. Waziri atwambie majenereta yale 12 yako wapi ambayo tumesaidiwa Wazanzibari kwa ajili ya shida ya maji mwaka juzi.

Mhe. Spika, jengine *BoT* imejengwa kwa Tanganyika na Zanzibar tuambiwe hisa yetu sisi ni shilingi ngapi na kwa kweli hatutaki tena maneno ya kisiasa, siasa imepita wakati wake sasa tunataka vitendo.

Mhe. Spika, mwisho kabisa ni mafungu makubwa ya Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Mhe. Spika, sisi hatukubaliani na hili, kila wizara, kila idara tumeitengea fungu lake la safari za ndani na nje ya nchi. Limewatengea zaidi ya shilingi bilioni 4 Wizara ya Fedha hatukubaliani nalo suala hili na kwa kweli wenzangu mimi nitawashangaa sana wakikubali kupitisha fungu hili kwa ajili watu kwenda kutembea nje.

Mhe. Spika, niseme tu kwamba Mhe. Waziri ni kaka yangu, mtoto wa mjini, nikuombe urudi na kitabu chako hichi ukakutane tena na wataalam wako mtuletee kitabu chengine kizuri ambacho kitawaridhisha Wazanzibari. Lakini hichi kitabu hakifai kuletwa ndani ya Baraza hili la Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa hakina maana hata pesa mbili. Mhe. Spika, nakushukuru siungi mkono hoja.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, nakushukuru sana na mimi kunipa nafasi hii jioni ya leo kuweza kuwatetea wananchi wetu haki zao kwa kupitia Wizara hii ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na hususan wale wafanyakazi ambao wametoa jasho lao kwa nguvu zao zote. Masikitiko makubwa ni kupewa mshahara mdogo ambao unachukua muda wa miezi mitatu, sasa leo wamenileta hapa ili niweze kuwatetea. Mhe. Spika, hiyo ni *message* ambayo naomba niifikishe.

Lakini Mhe. Spika, kutokana na hali yangu leo maneno ya vijana puresha ipo juu sijui nimeshapigwa juju au vipi, kwa hivyo utanistahamilia ule ukali wangu nitakuwa sina nitakwenda kidogo kidogo.

Mhe. Spika: Ukijisikia vibaya zaidi unaweza ukakaa.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, *inshaallah* na mimi kunipa nafasi hiyo lakini nitajitahidi bado kijana wako nipo *strong* pasipo budi nitakata rufaa nitakaa kitako.

Mhe. Spika, kwanza nimshukuru na nimpongeze sana Mhe. Waziri hiyo ni lazima tuwapongeze kutokana na jitihada zao za kutuletea kitabu hichi. Pia nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohammed Shein kwa kutuchagulia kijana wetu, upande mwengine shemeji kwa kutuletea hapa kutuongoza katika Wizara hii ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Spika, niende katika ukurasa wa 25 kuhusu *ZRB* ambayo wenzangu wengi wamezungumza. Mhe. Spika, kusema kweli *ZRB* inastahili sifa, bodi hii ndio mkombozi wa kupata mapato yote ya Zanzibar kwa sababu takwimu zake hapotezi. Mara nyingi sana *ZRB* wanasema kuwa jamani uchumi juu anamuelekeza waziri wake na hilo ni kweli kwa sababu watendaji wake wapo katika *experience* nzuri, wana data nzuri na hawawezi kuipotosha serikali hata siku moja. Mimi naamini hivyo kwa sababu wao tunawaona na tunawaona walipa kodi wanapokwenda kupeleka kodi zao kule.

Lakini Mhe. Spika, mimi kinachonishangaza zaidi kwa nini kitu kizuri tusikipambe tunachotupatia kodi kama hizi. Unajua *ZRB* inafanya kazi kwa nguvu kwa sababu mle ndani wamo wavuja jasho wenyewe wakulima na wakwezi na ndio maana wakahiari kufanya kazi kwa bidii ili kuipatia pato serikali yao na wale wakulima wa chini wainuke. Hivi kweli Mhe. Spika, vyereje inakuwa leo tunaambiwa tunapewa asilimia 25 mshahara mtu wa hali ya chini na *ZRB* anakusanya vizuri. Hapa ukipiga kura asilimia kubwa watasema *ZRB* tuwape wao kuliko *TRA* na kama husadiki hebu tutoe mfano.
Kama upo wakati tuweke kanuni kando si ndio kawaida yetu tumezoea, maneno ya mwalimu wangu mmoja ni kawaida, jambo la kawaida twende nalo kikawaida tusiliache.

Sasa hii Mhe. Spika, ukisema tupige kura hapa watu wote watasema *ZRB* ndio muongozo, ndio watataka wapewe kukusanya kodi. Lakini tukiangalia Mhe. Spika, wafanyabiashara wetu hawabariki wana kodi nyingi, wakizunguka huku *ZRB* inawabana, wakizunguka huku *TRA* inawabana, wakizunguka huku Manispaa inawabana, jamani kweli kutakuwa kuna uchumi hapa, halafu tunasema wanapandisha bei za vitu siku hadi siku lazima watapandisha. Bado serikali haijataka kukaa ikatulia kabisa kuweza kumuinua huyu mfanyabiashara katika hali ya kumuondolea umaskini kumpeleka kule katika lengo alilokusudia kwa sababu kodi zimekuwa nyingi sana.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri akitaka niipe asilimia hotuba yake hii aje anambie kuwa *TRA* sasa tumeiondoa nitakubali sana na nitamuunga mkono asilimia hiyo. Lakini sasa hivi sitomuunga mkono kama *ZRB* sasa hivi haijapewa kipaumbele.

Mhe. Spika, unajua kuna wakati mwengine sisi waheshimiwa tunajua mambo mengi dhidi ya mawaziri na wizara zao kwa sababu tunakuwa tunatembea na kamati. *Wallahi* Mhe. Spika, mambo mengine Mwenyezi Mungu atusamehe tukubali wanakamati tuseme *astaghfirullah*, Mwenyezi Mungu atunusuru. Mhe. Spika, tunaficha mambo mengi mpaka inafika pahala inabidi sasa tuyaseme, kwa hivyo leo mimi nitasema tena ninayo mengi.

Mhe. Spika, Mhe. Hamza Hassan Juma alizungumzia suala la *Rest House* ya Micheweni. Mhe. Spika, *rest house* ile amepewa mkandarasi anaitwa *Alhal Constructions Company*, huyu kijana amefanya kazi lakini kazi yenyewe sijui kwa kuwa hajatoa 10% au vipi mara anasimamishwa, mara anapewa kazi nyengine. Lakini kuna barua ya ushahidi tosha hapa anaombewa fedha shilingi milioni 40 kutokana na kifungu cha miradi ya maendeleo Mkoa wa Kaskazini.

Mhe. Spika, fedha hizo ameziomba Katibu ili alipwe yule mkandarasi na akasema tuna kifungu tumepitisha kwenye Baraza hili hili tukufu la maendeleo shilingi milioni 264 ambazo hizo ndio katika hilo fungu lenyewe alilloonesha Katibu zilipwe kwa huyu mkandarasi. Kinyume chake mkandarasi hajalipwa ameelekea kwenda kuitia kashfa serikali yetu, sio kashfa ni wajibu wake lakini utaona kama ni kashfa kwa sababu serikali kushtakiwa na mkandarasi ni aibu.

Mhe. Spika, siku zote mwanasheria wangu namnukuu katika suala moja hili ambalo halikubali *wallahi* anaumia kiasi kikubwa sana kusema kweli kijana, lakini tutamfanya sasa hivi atakuwa na lugha za kisiasa na akiziendeleza hizo zitampotosha, aende *straight* kule kule kwenye sheria zake.

Mhe. Spika, *wallahi* mwanasheria katika kitu ambacho hana mzaha nacho ni hicho, kila siku anawaambia kuwa jamani tuheshimu mikataba. Lakini kwa uzembe wetu tumekwenda kuvunja nae mkataba huyu kijana kaingia Mahakamani, kuingia Mahakamani serikali imerudi nyuma sasa tufanye majadiliano nje ya Mahakama, tunaona hatari kwa sababu tunashindwa tu. Aliporudi nje ya Mahakama kijana huyu anadai milioni 104,300,000/= wamekubaliana wamlipe hizo kwa makubaliano ya nje ya Mahakama.

Lakini mpaka leo Mhe. Spika, hawajamlipa hii ni aibu yule mtu ana watu wengi, amewaajiri watu maskini ya Mungu, wanyonge kwa kutekeleza, amenunua vitu kwa mfanyabiashara ili nae ajiendeleze. Hatimae

mfanyabiashara yule hakuweza kulipwa pesa zake na yeye anampeleka Mahakamani hatari kubwa. Mhe. Spika, huku kwa wale wafanyakazi wanamlaani jamaa haingii nyama kinanyofuka tu kutafuta haki yake haijui. Sasa haya ndio mambo ambayo tulikuwa sisi hatutaki kuyazungumza, tungependelea serikali iende kwa utaratibu na iweze kuwalipa watu.

Lakini Mhe. Spika, Wizara hii hii ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kuna matatizo makubwa sana ambayo ni ya muda mrefu shemeji yangu nae karithi atanipa ufafanuzi. Kwa sababu unaporithi hurithi kiti tu unarithi na vyote vilivyokuwa pale na mazuri anapokea hivyo hivyo anarithi kwa hivyo utatusaidia.

Kuna utata pale katika jengo kumezungushwa mabati, Wizara ya Fedha wanasema kiwanja chao wamenunua, lakini kuna familia ya kina Dorado pale. Sasa pale kuna *eight* na *nine* viwanja hivyo naomba Mhe. Waziri anisaidie ufafanuzi. Mwanzo Mji Mkongwe wametoa kibali kwa ujenzi, lakini kwa bahati mbaya kibali kile ikafuta kutokana na kuonekana kuwa kuna matatizo.

Mhe. Spika, hawa wananchi jamani tusiwadhulumu kwenye ardhi zao, hebu tuwaambie inataka serikali, ikitaka serikali inunue ndio wajibu wetu wa sheria, mwiteni mnunue lakini leo mnamhangaisha, kiwanja kile kauziwa jamaa mmoja anaitwa Said kutoka ukoo huo wa kina Dorado. Sasa Dorado alipe pesa ziko wapi pale nae kauza kwa mujibu wa mali yao na hati hii hapa wanayo na ramani yao ipo ya kuonesha kweli uhalali wa kiwanja kile chao. Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri anisaidie kabla sijatoa tume na mimi kutaka kuunda. Kwa sababu wenzangu wengi wamepiga kelele kutaka kuunda tume.

Mhe. Spika, masuala ya viwanda japo hatuna viwanda lakini tunavipotosha viwanda hatuvisaidii, navyo ni moja katika changamoto ya kutuletea mapato. Mhe. Spika, *ZRB* anashindwa kukusanya pale mapato kwenye viwanda kwa sababu viwanda vingi vimekufa. Lakini kuna kiwanda hichi ambacho nilikisema mimi cha ufugaji wa kuku na utengenezaji wa chakula Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko alieleza hivi, Serikali imeuza lakini sikumfahamu, serikali imeingia ubia. Sasa hapa ipi ni sahihi, ikiwa kama imeuza serikali kwa kiasi gani, ikiwa kama serikali imeingia ubia tuone basi mapato yake yanakwenda wapi. Mapato haya Mhe. Spika, kila tukiyapata ndio mishahara inaondoka kuwa midogo inakwenda mishahara mikubwa.

Mhe. Spika, wafanyakazi wanalia kipato kidogo. Kwa mfano, wafanyakazi wa Shirika la Umeme sasa hivi wanasema kuna asilimia 40 inakatwa na kilichoongezeka ni kidogo na hicho hicho kidogo kinachukuliwa. Wafanyakazi wanalia mmewaongezea halafu asilimia kubwa mnawachukulia wenyewe kwa

kodi zenu mnazozikata kwa hivyo, tuwafikirie hawa. Kweli mtu anapata laki tano lakini laki mbili unaichukua wanabakishiwa laki tatu sasa tunafika wapi, hebu tuangalie ile imani.

Mhe. Spika, mimi siku zote nasema tunapotunga hizi sheria tuwe makini, sheria hatumkomoi mtu wa nje aliyekuwa hayumo kwenye Baraza, tutafanya na sisi itatukomoa. Hebu tufikirie hili, si kitu cha masihara hii sheria, tunapiga makofi tunatunga sheria hapa tunajidhatiti, mwanao ndio inamu-*affect* ile sheria.

Kwa hivyo, tunapotunga sheria hebu tuwe *aste aste* kidogo tena tujitahidi sana tuiangalie baadae itakuja kutuumiza. Leo unamuwekea mtu asilimia 25 wewe una mwanao unakusudia nini. Leo ni waziri na hii waziri nakwambia tusidanganye bwana, mimi sijaona asilimia kubwa Mhe. Waziri akatoa nje akawa tajiri, utakwama tu, kwa maana yapo tunayafanya hapa si kweli. Hata Mhe. Mwakilishi tisijinasibu hii si utajiri bwana hata siku moja. Kama wenzetu wana mkono wa nyuma nilivyokusudia wa kupata fedha hapo ni sawa hatuna tatizo. Sasa hii sheria tunapopanga mishahara tuwafikirie ili na mwanao kesho kutwa akiwa Mkurugenzi pale aweze kufanikisha.

Mhe. Spika, niingie ukurasa wa 30 kifungu cha 57 Uhakiki Mali. Mhe. Spika, wafanyakazi wa idara hii wanafanya kazi nzuri sana na kwa uadilifu. Lakini Mhe. Spika, katika idara zake zote mtoto huyu hakumpenda, hana maposho huyu, anafanya kazi katika mazingira magumu. *Wallahi* wale ndio hiyo kutaka kuingia tonge mdomoni tu lakini Mhe. Spika, ungejua hawa wahakiki mali ni sawa sawa na *PAC* ya Baraza hili. Tena sikufundishi waziri wangu, hawa mazingira yao hata zile ripoti inavyoonesha wanavyozichapa wanazichapa nje ya utaratibu kwa sababu hawana mashine.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa taratibu wanatakiwa wapewe maposho, wapewe vitendea kazi ndani ya ofisi zao lakini hivyo vitu hawavipati ni hatari kubwa, maposho yao hamuwapi mnawaonea. Mhe. Spika, mimi nitakuja kuzuia kifungu hichi. Fungu lake la mshahara Mhe. Waziri namnyang'anya naliweka hapa ili nihakikishe kweli ana nia nzuri ya kuwasaidia hawa watu wa Uhakiki Mali.

Mhe. Spika, niingie ukurasa wa 44 Benki ya Watu wa Zanzibar *(PBZ).* Mhe. Spika, hapa kwa kweli wamejitahidi sana katika kuondoa umaskini kwa wananchi wetu, walichokosea tu walitoa mikopo ile ya JK na AK walifanya ile *pressure* na tumewa-*pressure* sisi viongozi hili tuliseme, hatari yake leo fedha hazijarudi. Lakini ninachowaomba hivi sasa katika marekebisho yao watenge fedha maalum za kufanyia semina za kuelimisha ili wajue mradi gani ambao wataukopesha pesa na uwe una tija.

Mhe. Spika, watu wanafikiri miradi ni kuchukua pesa basi tayari umeshakuwa na miradi. Mimi nasema siku zote huwezi ukachukua leo ukenda ukapeleka ndizi Kitope kama ndio unafanya biashara hufanikiwi. Kwa sababu Kitope inatoa asilimia ya ndizi, ndizi leo ukaipeleke Makunduchi ndio kwenye uhaba wa ndizi, sehemu nyengine Matemwe ndio kuna uhaba wa ndizi. Hivyo ndio inavyotakiwa biashara lakini watu wetu hawajapata taaluma ya kibiashara, biashara tano wanafanya sehemu moja ni zile zile. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri hapa safari hii benki wajitahidi kuziokoa hizi fedha na wengine waweze kupewa, wasifanye pupa, watulie, watumie nguvu zao zote ili kuweza kufikisha taaluma na kuweza kufanya biashara inayotakiwa.

Mhe. Spika, nizungumzie Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Mhe. Spika, mfuko huu kama tulivyosema sheria ile ya sasa hivi iliyowekwa ni kubwa sana kupata mtu mafao yake. Mhe. Spika, wafanyakazi wanajitahidi kupeleka michango mingi sana kwenye mfuko huu lakini sheria iliyokuwepo kwa kweli haikidhi haja. Kwa sababu leo mtu mpaka ufike miaka 60 ndio uweze kupata mafao yako, kuna wengine wafanyakazi wa mahotelini hawatimizi, wanafika miezi yao mitatu wanafukuzwa kazi. Je, kile walichokichangia watakipata vipi.

Lakini hapa Mhe. Spika, naomba nitoe rai kwa kuwa hizi ni fedha na mara nyingi sana nawaona hawa wahusika wanatafuta miradi ya kuwekeza. Mhe. Spika, ningeomba wafikirie sana hiyo bodi na wakurugenzi wake na wao watatoa mkopo kwa wale wenyewe wanaochangia lile pato lao ili waweze kuondoa umaskini. Mhe. Spika, hawa-*risk* hapa kabisa kwa sababu yule unayemkopesha pesa tayari umeshakuwa na taarifa kamili katika wizara yake, kiinua mgongo chake unacho wewe leo wanaogopa nini wasiwakopeshe haki yao.

Mhe. Spika, naomba wapewe fedha hizi ili waweze kujiondolea umaskini kwa njia ya aina yoyote ambayo wanaiona wale wafanyakazi wenyewe. Au wawajengee nyumba za mkopo nafuu ili kiinua mgongo chake asiweze akafika pahala akakijengea nyumba na hiyo ndio wanapofeli watu wetu. Mhe. Spika, naomba sheria irekebishwe na hili suala tumeshalisema siku nyingi sana kuwa sheria irekebishwe wenzetu wanaumia. Hii ndio nimesema jamani sheria hii tunaitunga hapa hatuwakomoi watu wengine tunajikomoa sisi wenyewe. Kwa hivyo, naomba sana hili suala mwaka unaokuja tusizuie bajeti hii sheria ije kwenye meza na tuweze kuipitisha kwa uadilifu kabisa.

Mhe. Spika, jengine nizungumzie ukurasa wa 52 kuhusu *ZIPA*. Mhe. Spika, wenzangu wamezungumzia suala la *ZIPA* lakini niseme ni asilimia kubwa mpaka sasa hivi wenzetu wanatusaidia sana. Wanatusaidia katika uwekezaji lakini kuna mambo mengine katika utata wa sheria hapa kidogo lazima wakae

watu wazuri. Mhe. Spika, Mhe. Hamza Hassan Juma kasema hapa inatakiwa wakae watu wa Mazingira, watu wa Utalii, watu wa Ardhi, wakae pamoja ili kulitafuta jambo lenye msingi na kulitatua pale na kulisema.

Mhe. Spika, ni kweli sasa hivi michanga ya mahotelini inapandishwa na hoteli zangu mimi pale kati ya *Blue Bay* na *Bravo* wanapandisha mchanga ndani wanachimba na hakuna sheria yoyote ambayo imechukuliwa. Mhe. Spika, inasikitisha sana . Wanachimba watu kwa makusudi na wameshawahi kuitwa wanafanya jeuri hawataki kwenda.

Sasa hii sheria nasema siku zote tunayoitunga hapa inakuwaje. Kwa hivyo, mimi nasema kwamba hebu tuangalie kama kuna mapungufu ya sheria hebu tuyaangalie na tuweze kusaidia, kwa sababu hali ni ngumu sana. Watu hawa wanaharibu kwa makusudi sana. Kwa hivyo, ninachokiomba ni kwamba serikali sasa hivi ikae macho kabisa. Mimi nimesema hapa kwamba namngojea Mhe. Waziri kwa hayo niliyoyasema ili na miminiweze kuomba niunge tume ili kuondoa huu uovu uliofichikana hapa na kuweza kuutaja mara moja.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kuwa leo kutokana na hali yangu sitokuwa na mengi sana. Kwa kumalizia naiomba tena wizara hii ya fedha, ndio mkombozi wa wananchi na wanyonge ili kuondoa umaskini. Mhe. Waziri kama utaona hali ya hewa ilivyo, hatuna mvua hatuna jua, hali ya hewa iko kati na kati. Nini maana ya kusema hivyo. Wenzangu wamesema kuwa wafanyakazi wengi wanafanyakazi hewa wapo na wengine wanafukuzwa makazini kiholela na mishahara iko mpaka leo.

Mhe. Spika, KMKM wameshafukuzwa watu na hili suala nimeshalisema sana na nitaendelea kulisema sana. Wizara ya Afya keshafukuzwa mtu na mahakamani keshashinda. Kwa nini asilipwe pesa zake jamani. Mhe. Waziri ndio tukasema wizara yako hii ina mapungufu, kitabu chako tukasema kirejeshwe kwa tabia hizo zinazofanywa Mhe. Waziri na wewe unalipa mishahara. Mfanyakazi wa Wizara ya Afya Pemba kafukuzwa.

Kuna mama mmoja mafanyakazi wa serikali ya Mkoa Pemba kafukuzwa, tume imemrudisha tuna jeuri, mkoa hautaki kumrudisha yule mtu. Mahakama imeamuru arejeshwe, hataki kumrejesha kwa kuwa nini, anadai pesa zake milioni 85 alipwe, hataki tumlipe. Jamani tunakufuru vipi.

Mhe. Waziri nimewaambia KMKM kuna wafanyakazi ambao wamefukuzwa, hebu tukae nao kwenye meza tuwasikilize. Lakini mishahara yao mpaka leo inakwenda na kama uongo basi tuundeni tume tufuatilie, sasa hayo ndio mapungufu yenyewe, tukiunda tume serikali hamtaki na wakati ni haki yetu

kuunda tume teule. Mhe. Spika, hayo ndio yanayotufanya sisi tuwe na jazba, tuwe na uwezo wa kusema. Inasikitisha kuona watu wanafukuzwa kiholela tu. Bosi akimchukia mtu anamtafutia sababu toka nenda zako, kwa nini mheshimiwa, yule ni binadamu bwana.

Juzi mimi nilisema suala la yule kijana wetu wa Shirika la Umeme nimesema hapa, sasa jamani kama mnaona ana makosa, Mahkam imeamuru hana makosa, arejeshwe kazini hatimae tumekwenda kumfukuza kabisa, tumeacha kiumbe kizuri tu kile Meneja wetu aliyekuwa Shirika la Umeme zamani tumemfukuza. Tume imeundwa hapa na mwenyewe Waziri Kiongozi wakati ule imesema hana makosa hana chochote bado yule kijana tuliyemuwacha nje anahangaika masikini ya mungu.

Sasa haya Mhe. Omar ndio maana tunakutesa kwa sababu haya Mheshimiwa huyafatilii. Imeundwa Tume ya Kiwanda cha Sukari leo yangapi, hebu nambie na wewe jana ulikubali mwenyewe ukubali ulisema mkataba tulompa afanye sukari, lakini leo anatengeneza spiriti haya nambie sasa Serikali imekaa kimya mwenyewe umesema Waziri. Sasa leo utakuja kunijibu nini Mheshimiwa ninakupiga budi sikwachi kitu hiki Mheshimiwa. (*Makofi*).

Mheshimiwa ulikuwa hupo nilishindwa kwa sheria hapa moja, kuambiwa mkataba wa Kiwanda cha Sukari utapewa wewe Mhe. Spika, ukitoka hapa mimi ninakufuata nipate mkataba wangu wa Kiwanda cha Sukari. Kama wamekudanganya haukufika uone tabia ya Mawaziri wetu wanavyotudanganya au wanavyokudanganya na wewe katika Baraza lako Mheshimiwa. (*Makofi*).

Wananchi wa Kaskazini Mheshimiwa hawana imani na suala hili wananyanyaswa katika ardhi yao, wallahi Mheshimiwa ni kitu cha kusikitisha, watu wanatoka nje wanakuja kunyanyasa watu kwenye ardhi yao, wameigomboa inasikitisha inatia uchungu Mheshimiwa.

Serikali imelala halafu tukisema tuwe wabaya hatuogopi, tutasema kadiri ya uwezo wetu, na tunatetea wananchi, watu wanachukua ardhi heka tisa, tisa wananchi mnawapeleka wapi hamuwapi wananchi halafu leo tunasema kilimo, kilimo mwananchi utampa wapi alime. Wakati wewe Mheshimiwa mkubwa ushachukua ardhi heka tisa niambie mwananchi wa chini atapata wapi heka ya kulima. Halafu utapata wapi kumuelekeza Mhe. Omar aweze kupata uchumi wake mkubwa hupati.

Mhe. Spika, kwa hayo machache naona nisiendelee naona *pressure* inapanda juu, kwa hivyo Mheshimiwa siungi mkono.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ninakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, ninakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika, mimi nimshukuru Mhe. Waziri kwa kutuletea kitabu hiki ambacho kama wajumbe wengi waliotangulia kusema wamesema kwamba hakijitoshelezina akakipange upya ili atuletee tena tuweze kuyaona hayo ambayo wengi wameyatoa kasoro mimi naunga mkono katika hilo.

Mhe. Spika, mengi yameshazungumzwa hapa na wajumbe waliotangulia na mimi nitilie nyama katika baadhi ya maeneo ambayo ninahisi bado yana kasoro kidogo.

Mhe. Spika, mimi nianze kwenye suala la *BoT* ingawa humu Mhe. Waziri sikuliona hata kama kaligusa humu kwenye kitabu chake ndio maana wajumbe wanalalamika sana, kwa sababu nalo limo katika hesabu, tuna hesabu zetu pale. Mimi nirejee kama wenzangu waliopita kutaka kujua hasa ule uanzishwaji wa *BoT* Zanzibar ilikuwa na hisa ngapi turejee katika hali nzima inavyokwenda ya mgao kwa faida au hasara inayopatikana katika hilo.

Hebu atupe Mhe. Waziri maelezo ya kutosha juu ya hili atuletee hesabu tunazotaka. Ilivyoanzishwa na mpaka sasa Zanzibar inafaidika vipi na hili, maana yake hesabu yake hii hatuifahamu na sisi si wadau tu pale ni *share* pale kama inavyoambiwa, sasa ndio maana tunataka Mhe. Waziri bahati nzuri yeye alishakuwa Naibu Waziri kule Jamhuri ya Muungano na leo hii ni Waziri wa Fedha hapa, nina hakika atakuwa na majibu mazuri kweli katik hili. Maana wengine wengi tulikuwa tukiuliza yanakuwa kidogo majibu yake hayendi sawa.

Sasa tunamuomba sana Mhe. Waziri katika hili aje atupe hasa haya mahesabu ya BoT kuanzia kuanzishwa kwake ile *share y*a Zanzibar walipoanzisha ile BoT. Na kutoka huko mpaka hapa tulipo Zanzibar inafaidika vipi? Tuone yale mapato au hasara inayopatikana katika hili. Basi ninamuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja hapa atupe kinaga ubaga juu ya jambo hili, ili wananchi wetu huku waweze kujua ule uanzishwaji wake na faida wanayoipata, hayo ni malalamiko ya wananchi. Sasa sisi tunawakilisha kilio cha wananchi hapa kama kazi yetu ambayo inatutaka tufanye hivyo.

Mhe. Spika, tuje katika uundaji wa ile Bodi yenyewe ya *BoT* sijui tuna wazanzibar wangapi katika bodi ile, lakini tukija katika Gavana wa *BoT* mimi sijawahi kumsia Mzanzibari pale kuwa Gavana tangu imeanzishwa ile. Sasa hebu Mhe. Waziri atuambie hasa hivyo Zanzibar haina mtu ambaye anafaa kuwa Gavana wa *BoT*? Hakuna tangu imeanzishwa hii taasisi tunayoambiwa ni

ya Muungano na sisi pale tuna *share*. Basi mbona inaonekana kama imeelemea upande mmoja tu, upande wa pili hakuna kitu na tunavyoambiwa tuliunganisha hizi nchi zetu tukaanzisha kile chombo tulipokuwa tumeungana kwa ajili ya kuweka mambo sawa. Sasa mpaka leo hata siku moja basi hakuna Mzanzibari ambaye amewahi kuwa Gavana hii inatupa shaka kidogo. Sasa tunamuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja atueleze kwa nini inakuwa hivi.

Halafu tunataka kuon uwiano ya wajumbe pale, maana hiki chombo cha watu wawili, sasa uwiano wa wajumbe wa bodi pale hebu tuuone ukoje? Akitukamilishia hayo vizuri Mhe. Waziri inawezekana ikawa anapunguza budi lakini kama hakuna hapo budi ipo na lazima tupate maelezo ya kina juu ya jambo hili. Kwa sababu wazanzibari wanapenda kujua haki zao na hii ni sifa ya kila mwanadamu huwezi ukaiacha haki yako ikapotea. Sasa kama kuna jambo letu pale ni vyema likatangazwa wazi na watu wote wakajua, kuliko kuwa kuna mambo ya mjificho mjificho hii haitupeleki mbele.

Mhe. Hamza hapa alisema tunataka uwazi, sasa uwepo uwazi katika mambo haya pia. Sasa Mhe. Waziri utakapokuja kwa sababu wewe umeshakamata nafasi zote mbili umeshashika kule ushashika na huku nahisi hapa ni pahala pazuri na wewe ndio mtu hasa unayeweza kutujibu katika hili. Mhe. Spika, tukishapata hayo ya *BoT* faida na hasara na mambo mengine.

Nije kwenye *TRA*, *TRA* nacho ni chombo cha muungano lakini nacho ni vile vile kama *BoT* sijui kama kumbukumbu zangu zinaniambia sahihi kwamba hapajawahi kuwa na huyo Kamishna Mkuu wa *TRA* kutoka Zanzibar, utasiki *Deputy Commissioner* tu tena huko huko Zanzibar hakuguswi kule. Imekuwa kama hiki chombo si cha Muungano, lakini kule kuna makamishna wanafika wanne huku kuna kamishna mmoja tu akienda kule si watam-bana tu wao atatoa maamuzi gani, pakipigwa kura yuko peke yake atakatwa tu. Kwa hivyo uwiano wa ile baina ya Mkurugenzi Mkuu na hawa Makamishna wengine, mimi ninafikiri kuna haja ya kuangaliwa. Basi Mhe. Waziri utakapokuja hebu tueleze sababu za msingi zinazofanya kuwa hivyo wakati chombo hiki ni ch muungano.

Kwa sababu chombo hiki ni cha muungano nayo ninakuja kwenye bodi vile vile utueleze hao wajumbe wa bodi hii ya *TRA* wapo wangapi, wazanzibari wangapi. Na ukishaona wazanzibari wamo kidogo basi anza na majibu huko kabisa ya kutujengea hoja kwa nini wakawa kidogo tusiwe sawa kwa sawa. Kwa sababu sisi tumeungana na hii taasisi inaitwa ya muungano. Sasa sijui itakuwaje taasisi hii tusiwe na wajumbe sawa kwa sawa na ile ya *BoT*. Mimi ninapata shaka na si mimi tu na wazanzibari wengie wanapata shaka juu ya jambo hilo ndio maana kelele hizi zinakuwa nyingi, kwamba mnakaa vikao

wanasiasa mnaamua juu ya hili suala la ulipaji kodi mara mbili, lakini utekelezaji huku unakuwa haupo. Na haupo kwa sababu nyinyi mkesha kaa wanasiasa mmeshaamua lakini hawa watendaji hawa, wakifika mahala hawasililizi yahuku na kwa sababu ya wingi wao katika ile bodi na ule ugawanaji wa madaraka kuanzia Mkurugenzi Mkuu au Kamishna Mkuu sielewi wetu sisi nafikiri *Deputy Commissioner* mmoja ndie anayekwenda kule katika uongozi. Sasa unafikiri maamuzi yatakuwaje, hawezi kuwa kusema huyu.

Sasa mimi Ninafikiri Mhe. Waziri utakapokuj uje utupe uzuri juu ya jambo hili. Ili wazanzibari waelewe hasa utaratibu na mambo yote yanayohusu suala hili la *TRA* kuondosha haya manun'guniko yaliyokuwepo. Kwa sababu mimi nina hakika manun'guniko ya wafanya iashara wa Zanzibar kwa ajili ya kupeleka mizigo yao kule Dar es Salaam ni ya kweli na ya uhakika. Ingawa hapa kila tukiuliza tunaambiwa tatizo hili hapa limeshatatuliwa. Lakini kwa kweli utatuzi wake umeishia huko huko juu tu kwa wanasiasa, huku chini kwa watendaji haujafika na ndio maana kila wakienda wanaendelea kulipa kodi tena.

Vile vile Mhe. Waziri utakapokuja hebu tueleze kama hili suala kweli mmekubaliana, kuna maofisa gani ambao mmeshawachukulia hatua juu ya ukiukwaji wa agizo hili, kwamba mmeagiza hili liende hivi hakutekeleza Afisa yule, basi kuna huyu na huyu labda tuliwafukuza kazi au tumewachukulia hatu, naomba uje utupe maelezo hayo, kwamba tumeshafanya hili halafu tumuone kama kweli kuna Afisa mkaidi ambaye anaweza kukaidi agizo la ngazi za juu. Lakini mimi narejea tena kutokana na mgawanyo ule ule wa ile taasisi kimuundo wake, basi hili linasababisha kuendelea kwamba wafanya biashara wetu wanapata tabu ya kutozwa kodi mara mbili.

Mhe. Hamza alitoa mfano hapa kwamba ikitoka huko kwamba umesafiri umeshuka Dar es Salaam hata kama umeteremka pale unakwenda kupanda ndege kiwanja cha pili tu pale cha ndege ndogo, basi mzigo uliokuwa nao utatakiwa ulipe kodi kabisa pale. Kweli kwa sababu umeshafika katika nchi ya Tanzania.Unalipa kodi unakwenda zako uwanja mdogo unapanda ndege unakuja zako Zanzibar.

Lakini leo hii mfanya biashara akaja akashuka Zanzibar atalipa kodi hapa, akisafiri akenda zake Dar es Salaam na vifaa vile vile akaonesha kwamba mimi nilishuka pale nilmeipia hivi, ataambiwa kodi ndogo lipa tena. Sasa hii Mhe. Spika, uone namna gani haki haitendeki, inakuwa *TRA* kama iko likizohakuna maana yake lakini ofisa huyu aliyeko hapa anaitwa afisa wa *TRA*.

Sasa hili kwa kweli Mhe. Spika, ni tatizo kubwa sana lakini lisababishwa na watendaji. Na watendaji hawa wanaosababisha wanajulikana wako upande gani, lakini hakuna hatua zinazochukuliwa kwa watendaji wale, wataendelea kudharau maagizo yale kwa sababu hakuna hatua zinazochukuliwa. Au inaonekana hawa wenzetu hawapo ukweli kwenye hili.

Kwa hivyo mimi katika hili ninaunga mkono hoja ile ya Mhe. Hamza hii *TRA* bora tuihamishe tuwaachie *ZRB* wafanye hii kazi. Kwa sababu *ZRB* wanatufanyia kazi nzuri, wanakusanya kodi zetu vizuri basi na hii mamlaka ya ukusanyaji wa kodi hizi nyengine za ndani tuwape wao vile vile watatukusanyia vizuri zaidi. Halafu hiyo *TRA* tukae tutizame labda hivyo vitu vyengine. Mimi ninafikiria hiyo labda inaweza ikatusaidia tukaondosha hili tatizo.

Mhe. Spika, niondoke hapo nisogee kwenye kitabu cha Mhe. Waziri ukurasa wa 30 kwenye Idara ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma. Mhe. Spika, nimesoma kidogo kwenye kitabu hiki cha Mhe. Waziri juu ya kazi na mambo ambayo imepangiwa Idara hii kuyafanya, kuna mambo mengi sana sana. Lakini mimi naanza hapo katika hii jambo la pili kabisa anasema kufanya uhakiki katika Wizara ya Kilimo na Maliasili, Mawasiliano na Miundombinu, Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, Ofisi ya Makamo wa Kwanza na Makamo wa Pili wa Rais. Sasa mimi ninajiuliza mbona zimetajwa taasisi kidogo sana za Serikali wakati ilikuwa ifanywe katika taasisi zote? Wizara zote ninafikiria zinawajibika kufanya hivyo. Maana Idara ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma, anasema imeweza kufanya uhakiki.

Sasa kama imehakiki huko mimi ninafikiria Idara hii haifanyi kazi zake ipasavyo, imejaribu tu kutuwekea katika kitabu hapa lakini kwa kweli Idara hii ina matatizo mengi mno. Mhe. Spika, kama utakumbuka hapa tulivyokuwa tunapitisha bajeti ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, tulizungumzia uhaulishwaji wa fedha za bajeti ya Ujenzi wa Wizara ya Miundombinu. Waliomba milioni 100 katika bajeti ya 2009/2010 lakini wakapewa milioni 49 matokeo yake badala ya kwenda kujenga makao makuu ya Wizara wakenda wakakarabati *godown* ili Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu wakae pale.

Sasa huu ni ufujaji wa mali za Serikali, pesa zile zilizokuja kuombwa hapa ni kwa matumizi ya ujenzi wa makao makuu ya Wizara, unapokwenda kulikarabati *godown* si ujenzi huo wa makao makuu ya Wizara. Maana hilo *godown* lenyewe limechanganywa taasisi chungunzima. Kwa hivyo na wao wakapia *repair* tu. Sasa sisi tulipokwenda na kamati ya *PAC* hatukuridhika kabisa hasa huo ukarabati wenyewe, kwa sababu tukitizama *value of money*

haipo pale. Milioni 49 kuzikarabatia kukata *partition* ya ofisi tatu haiko sahihi. Mhe. Spika, ndio maana wachangiaji hapa waliopita wamesisitiza juu ya haja ya Baraza lako tukufu kuunda kamati teule ya uchunguzi juu ya mambo kama hayo.

Idara hii ya Uhakiki wa mali na Mitaji ya Umma ina mambo mengi sana imefanya. Nimekuba hilo dogo sana Mhe. Spika, lakini yapo na mengi kabisa. Kuna uhaulishwaji wa hicho kiwanja pia kilichokuwa kimekusudiwa kujengwa makao makuu ya Wizara Mtoni kimehaulishwa kimepelekwa kwa mtu binafsi. Wizara yenyewe imeomba sehemu nyengine kwa ajili ya ujenzi wa Wizara. Sisi tunapata shaka, mimi naungana mkono na wenzangu wanaosema kwamba pesa zile zilizoombwa za ujenzi wa makao makuu ya Wizara ya Miundombinu hatutoziruhusu hapa. Tutazizuia mpaka tupate maelezo ya kutosha.

Kwa sababu hatuwezi kuwa tunatoa mafungu ya pesa kwa matumizi tunarudiwa kuombewa matumizi yale yale na yale mwanzo hayakutumika. Kwa hivyo hii sio sahihi na ndio maana tukakubaliana kwamba *PAC* irudi katika kuangalia uhaulishwaji au utaratibu mzima uliotumika juu ya uhaulishwaji wa kiwanja kile kutoka Miundombinu kwenda kwa mfanyabiashara binafsi.

Mhe. Spika, nikiendelea katika Idara hiyo ya Uhakiki mali na Mitaji ya Umma, Idara hii imekuwa ikihaulisha mali nyingi sana za Serikali iko mifano hai kabisa. Hivi juzi juzi tu imehaulisha au sijui kama imeuza au imekodisha maana ufafanuzi wake hatujaupta vizuri, sasa nilikuwa nataka nimuombe sana Mhe. Waziri atakapokuja atueleze utaratibu mzima uliotumika kuondosha jengo la mambo msiige kutoka milki ya Serikali kulipeleka kwa wawekezaji.

Mimi ninaweza kusema kampuni ya mtu binafsi kuondosha kwenye milki ya Serikali. Aje atueleze utaratibu wake aliotumia, lakini pia atuambie sababu za msingi kwa sababu Mhe.n Spika, katika jengo lile zilikuwemo taasisi za Serikali zikiwa ndio ofisi zao. Imefika mahala tumezihamisha taasisi zile kuzipeleka mahala ambapo tumepatoa pakubwa tumewapeleka mahala padogo hawajitoshelezi.

Kwa mfano imehamishwa pale ofisi ya vizazi na vifo kupelekwa iliyokuwa jengo la benki ya watu wa Zanzibar Forodhani. Mhe. Spika, mimi niliwahi kwenda pale nilikuwa nataka cheti cha mtoto wangu, lakini siku niliyokwenda ilikuwa kuna mvua mvua inanyesha pale, nilipofika nikaiona ile hali, document zinarowa na mvua kwa sababu lile jengo la *PBZ* pale ndani liko wazi. Mimi nikauliza mbona hizi document zinarowa au hazina kazi? Wakasema hapana hizi ni *document* bwana sio hazina kazi zina kazi na ni muhimu hizi, lakini

hatuna pa kuziweka. Humo mote unamuona mmejaa ndio tumeweka hapa lakini mvua inanyesha zinaroa. Sasa mimi nikapata shaka sana Mhe. Spika, nikawauliza kule mlikokuwepo zilikuwa zinarowa hizi wakasema hapana

Namuomba sana Mhe. Waziri hivi vitengo kwanza viachiwe vifanyekazi zake sawa sawa, kwa sababu wakifanyakazi zao sawa sawa hawa, basi hayo malengo tunayoyakusudia kuyapata tutayapata. Lakini leo kama wanafanya uamuzi wa jambo fulani na anakuja mkubwa anasema hapana geuzeni fanyeni hili, basi watakuwa hawatendi kazi zao na watakuwa wanafanyakazi zao kwa woga maana mkubwa hataki.

Mhe. Spika, amesema malengo yao ni kuhakikisha kwamba wanawasaidia waweze kujua zile hazi au kazi zao hasa, basi hawa wapate mafunzo na wala wasipate hao tu pamoja na hao maafisa wa ngazi za juu wasomeshwe ili waelewe, kwa sababu leo unaweza kumkuta afisa wa mkubwa tu wa serikali lakini ukimuuliza maswali haya hakujibu, yaani hana jawabu Mhe. Spika, kwa sababu na yeye ameyaona na wala hajapata elimu ya jambo hili.

Kwa hivyo, inawezekana na wala usishangae kwa sababu ana *PhD* ukafikiri yote atayajua, inawezekana *PhD* yake ya mizizi na suala hili ikawa kwake halimo. Mhe. Spika, nadhani ni vyema na wao wakapewa elimu, kwa ajili ya kufanyakazi zao vizuri zaidi.

Mhe. Spika, kitengo hiki ni muhimu sana kabisa kwa serikali na ndio maana ninahakika serikali iliamua kwamba kila wizara kiwepo. Lakini jambo la kushangaza kitengo hiki kinapewa zile kazi ndogo ndogo tu kwenye zile wizara, na hapa nazungumzia vile vitengo vya *Payments*.

Sasa kazi nyingi sana zimeonekana tulimopita wananunua Wizara ya Fedha na wanakwambieni tu mnahitaji nini? Tunahitaji redio. Redio gani? redio ya *band* nne, yaani wao ndio wanaoagiza na kununua na halafu ndio wanawaletea. Kwa kweli nafikiri hii sio sahihi Mhe. Spika. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Wizara ya Fedha wawaachie kazi hawa, kwa sababu tumeshagawa haya madaraka, kwa nini wao na Mhe. Hamza Hassan Juma amezungumza hapa kuhusu suala la janareta la hapa Barazani kwetu halikununuliwa na Baraza, isipokuwa Baraza limeletewa tu, mnahitaji janareta KV na mimi sijui utaratibu huo, basi limeletwa tu, vile vile *Airport* kule.

Kwa mfano, kama lile la *Airport* kwa kweli Mhe. Spika, ni hasara shjilingi milioni 380/= zilizonunuliwa janareta lile na lina *guarantee* ya mwaka mmoja na *guarantee* ile imekufa janareta lile bado halijawa *installed*. Kwa hivyo, leo

litakapofungwa janareta lile likawashwa na lisiwake bovu, hasara kwa nani, serikali. Lakini ukiwatizama wale watu wa Uwanja wa Ndege wao wameletewa tu na wala fedha za kulifunga hawakupewa, watalifunga vipi lile na hawana hizo fedha. Mhe. Spika, wao walipotaka kununua hilo janareta waliomba huko Wizara ya Fedha kwamba tunaomba fedha kwa ajili ya ununuzi, aa! Leteni *specification* zenu, basi wao walipeleka na Wizara ya Fedha wakanunua, lakini hao wanunuaji walisahau kama linataka kufungwa, mpaka leo hii tunayozungumza Mhe. Spika, bado halijafungwa. Kwa hivyo, uone namna gani fedha za wananchi zinavyopotea kwa uzembe tu wa watu. *(Makofi)*

Sasa leo hii kingekuwa Kitengo cha Manunuzi pale ndicho kilichoshirikishwa kufanya hiyo, basi nahakika kitengo kile katika zabuni yake ingeingiza na fedha za uunganishwaji wa janareta lile, kwa sababu ni utashi wa huko na mimi nasema utashi. Kwa hivyo, wao wanachojua ni kukununulia janareta na kukuletea tena shauri yako ukilifunga usilifunge wao si kazi yao. Kwa kweli si janareta tu na vitu vingi vimo vya namna hiyo vinafanyika, yaani wanafanya hivyo Wizara ya Fedha na wenyewe wanasema wanazo fedha zao sijui *MDRA* na mimi sizijui.

Mhe. Spika, kwani fedha zile ukimuachie huyu na kumwambia vitu vyote vile na tumeweka vitengo, sasa kwa nini visifanyekazi na viwe vinafanyakazi kwa kununua *oil* pamoja na mpiga magari basi. Kwa mfano, ikeshakuwa pahala panaonekana pana fupa au pamenona basi tena wewe huna mamlaka ya kununua akanunue Wizara ya Fedha. Kwa kweli nahisi huu si utaratibu Mhe. Spika.

Kwa hiyo, kama tumeamua kufanya hizi kazi na ndio maana tukaanzisha hivi vitengo katika kila wizara, kwamba kila wizara ijitegemee, yaani ifanye mambo yake na wao waje wamuhoji, hawa Uhakiki Mali watakapomkagua pale au watakakwenda kuangalia hizi mali, basi waje wamuhoji ununuzi wake au matumizi vile ambavyo amefanya *CAG* anakwenda kukagua mahesabu pale ataangalia pale na kuona namna gani matumizi ya fedha zile yamefanyika. Kwa maana hiyo, akiridhia ataridhia na kama hakuridhia basi anatuletea kwenye kitabu na tutayaona hapa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ningeshauri sana Mhe. Waziri wizara yako ivipe nafasi hivi Vitengo vya Manunuzi katika taasisi hizi vifanyekazi zao na wala asiviingilie sana kama ana maelekezo basi ni vyema kutoa maelekezo, lakini kwenye masuala haya awaachie wenyewe. Kwa hiyo, hii Taasisi yako ya Uhakiki wa Mali ndio kazi yake ya kuhakiki mali pamoja na mitaji ya umma, sasa ikahakiki kule na zile mali izione, lakini ikiwa yeye mwenywe ndiye mnunuzi na baadaye ndio anayewapelekea halafu utahakiki vipi unatupa tabu.

Vile vile Mhe. Spika, nizungumze kidogo kuhusu suala zima la uhusiano baina ya Uhakiki Mali na *CAG*. Mhe. Spika, hawa Uhakiki Mali sijui kama wana mawasiliano yoyote na *CAG*, yaani sijui kama kuna ripoti yoyote wanapeleka kwa *CAG* juu ya mali za serikali, kwa sababu wao ndio wahakiki na baadaye wamwambie *CAG* hapa kuna hiki na kile.

Kwa kweli sifikirii kama kuna ripoti yoyote inayoonesha kwamba katika kipindi cha miaka mitatu tu nachukua mimi ilipelekwa kwa *CAG* juu ya mali za serikali. Mhe. Spika, ndio maana mpaka hii leo tumejaribu kuzunguka sisi *PAC* pale, basi unaikuta wizara haijui hata mali zake ni ngapi au ina nini na nini, mpaka unawauliza wanasema siburi tukapekuwe *files*, wanapopekuwa *files* hilo wanalolikuta sawa na ambalo hawakuliona ina maana mali ile ndio imekwenda.

Kwa hivyo, utakuta hapa kuna uharibifu mkubwa unatokea wa mali za serikali, kwa sababu hakuna ripoti inayotoka kwa Uhakiki Mali kwenda kwa *CAG*. Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri wakati atakapokuja aje atueleze hii idara ametoa ripoti ngapi kupeleka kwa *CAG* kwa ajili ya ukaguzi wa mali zile, kwa sababu atakapompelekea *CAG*, basi yeye atakwenda kuzikagua na hata kuziona na sisi *PAC* tutapata fursa ya kujua katika wizara ile kuna kitu gani.

Mhe. Spika, katika suala hilo namuomba sana Mhe. Waziri ahakikishe hili linafanyika, ili kuisaidia serikali kuweza kujua angalau hizo mali zake. Kwa kweli Mhe. Waziri ametueleza kwamba mara hii imepata fungu la fedha kwa ajili ya uhakiki wa hizo mali, lakini haya malalamiko kwenye taasisi za serikali yako makubwa mno, kwa sababu wanashindwa kupata fedha kwa ajili ya uhakikia wa hizo mali zao.

Kwa mfano, Mhe. Spika, wizara ina maeneo au nyumba itakapohitaji kupimiwa maeneo yale, basi ni lazima iombe kwenye Idara ya Ardhi na Upimaji kule, lakini Idara ya Ardhi katika kitengo kile ni lazima ulipie. Sasa kama hawakuingiziwa fedha za kazi ile hizi taasisi haziwezi kufanya, ndio maana utakuta kuna matatizo makubwa sana katika suala zima la uwekaji wa kumbukumbu za mali za serikali.

Wizara ya Fedha tulipokwenda walituambia wameshatoa muongozo, lakini ukishuka huku kwenye taasisi husika unakuta hakuna kitu. Sasa humu ametueleza kwenye kitabu chake Mhe. Waziri kwamba kuna muongozo umeshaandaliwa, fomu zimeshatoka. Kwa hivyo, tunaomba sasa hii idara ikasimamie ipasavyo, ili kuhakikisha kwamba hata kama kuna kalamu ya serikali basi ijulikane kalamu hii iko wapi na anaitumia nani, kama si hivyo Mhe. Spika, uendeleaji wa kutoa mali za serikali kiholela kuzihaulisha kutoka serikalini kwenda kwa watu wengine utaendelea na hautokoma.

Kwa kweli kuna mali za serikali hapa Mhe. Spika, zinauzwa hata wizara yenyewe haijui mali ile kama mali ile ni ya kwake. Kwa mfano, Mhe. Hamza Hassan Juma alizungumza kidogo kuhusu suala la kiwanja cha *Living Stone* pale, wakati tulipohoji kwenye Wizara ya Kilimo na Maliasili, basi Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili alituambia kiwanja kile kinamilikiwa na *ZRB*.

Kwa hivyo, tulipomkaba hapa Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili na baadaye akanyanyuka Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na kutueleza kwamba kweli wanamiliki, mimi nilitaka ushahidi wa umilikaji wa kiwanja kile, alinileta. Mhe. Spika, nataka nikwambia kwamba zile taarifa nilizozitaka Mhe. Waziri ameniletea.

Jambo la kushangaza sasa *ZRB* kiwanja kile walimilikishwa kihalali kabisa wakapewa *document* zote, lakini baada ya kuona kwamba wao hawapahitajii au kwa mahitajio yao ni padogo hapawatoshi, walichukua *document* zile wakakirejesha kiwanja kile Wizara ya Ardhi, au Maji, Ujenzi na Nishati wakati huo barua zipo zinaonesha hivyo.

Mimi ninachoshangaa kwamba ambaye aliyetujibu kuwa kiwanja kile kinamilikiwa na *ZRB* kwa sasa ni Waziri wa Kilimo, lakini kwa wakati ule alikuwa ndie Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kiliporejeshwa kwake. Sasa uone namna gani tunababaishwa na majibu, kwa sababu ilikuwa ni rahisi kwake yeye kutujibu tu kwamba kiwanja kile kilikuwa kinamilikiwa na *ZRB* kimerejeshwa Maji, Ujenzi maana ndio wamiliki waliokitoa kile kiwanja, tukapata ufumbuzi wa lile tatizo. Matokeo yake Waziri wa Fedha yeye hana tatizo, kweli mimi nilikimiliki lakini mimi nimerejesha.

Sasa Waziri wa Kilimo wa sasa ndie ambaye alikuwa Waziri wa Maji, Ujenzi kiliporejeshwa pale, ina maana hapa kidogo tumepigwa chenga juu ya kupata maelezo sahihi ya kiwanja kile Mhe. Spika. Ningewaomba sana Waheshimiwa Mawaziri wanapotujibu, basi wawe wanatupa majibu ya uhakika siyo ya kufyetua. Kwa sababu hapo ilikuwa kama katufyatua, lakini tulipofuatilia kimerudi na kimekuwa kule kwake ambako alikuweko.

Sasa kuna uzito gani kutuambia hiki sasa kiko kwenye Maji, Ujenzi kwa hiyo kwa taarifa zaidi labda ninde kwa Waziri wa Maji, Ujenzi wakati waziri yupo basi angetujibu na sisi tunayoihoji hpaa ni serikali na wala hatumhoji mtu *personal*, kwa hivyo serikali itujibu. Mhe. Spika, ikiwa *Cabinet* inatubabaisha si sahihi Mhe. Spika na wala hatupati majibu mazuri hivyo na tunaendelea kuwa na shaka. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ningeomba sana Waheshimiwa Mawaziri wasaidiane kwenye hayo majibu na Kanuni inatuambia kama waziri huyu itakuwa kwake kidogo ni gumu basi waziri mwengine anaweza kujibu kwa niaba, ugumu uko wapi kutuambia jambo likawa wazi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, namsifu sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko jana alitujibu maneno haya basi ikawa buti zilipungua, alipata buti lakini utaziona Mhe. Spika, zilikuwa nyepesi, lakini katika majibu ya kubabaisha basi siku zote buti zinakuwa kali. Kwa hivyo, ninawaomba sana Waheshimiwa Mawaziri katika kutupa majibu, basi watupe majibu yaliyosahihi na wala yasiwe majibu ya ubabaishaji. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tunafika pahala tunapata tabu, yaani tunakuwa kwenye mtihani na sisi, kwa sababu wananchi wanajua kinachoendelea kule ndio maana wanatutuma kuja kuhoji, sasa wasifikiri tunahoji kimya, inakuwa tayari tumeshafanya utafiti wa lile jambo, ndio maana tunakuja hapa na kusema.*(Makofi)*

Mhe. Spika, katika suala hili la mali za serikali mimi ndio ilikuwa mada yangu kubwa kabisa, kwa sababu wewe Mhe. Spika, ndiye uliyeniweka kwenye Kamati ya *PAC*, basi nimeona na nimejifunza mengi sana kwenye *PAC*, tunakwenda tunakagua unawakuta maafisa na ukiuliza vitu pale jawabu hakuna, yaani majibu yanakuwa ya kubabaisha.

Kutokana na hali hii tunasikitika sana, kwa kweli watupe majibu ya kuridhisha na hata kule tunakokwenda, kwa sababu tunaporudi hapa ndio maana tunatoa ripoti, sasa tukitoa ripoti zetu za kamati zetu zile, huwa tunaomba sana serikali izichukue na izifanyiekazi.

Kwa kweli tumeshazungumza na Makamu wa Pili wa Rais hapa juu ya jambo hilo na alituahidi kabisa kwamba atawaelekeza mawaziri wake kuwa kuhakikisha kuwa ripoti zile zinafanyiwa kazi. Lakini mpaka leo hii ripoti ya mwezi wa nne tuliyoiwasilisha bado sijaona utekelezaji wake hasa kwenye suala hili la mali za serikali, kwa sababu tulilalamika sana.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja atueleze kwenye ripoti yetu ile amefikia wapi au yepi ameyafanyiakazi mapendekezo yetu ya ripoti ile pamoja na hatua ambazo amechukua.

Nikiendelea na mchango wangu nizungumzie kuhusu Benki yetu ya *PBZ*. Mhe. Spika, *PBZ* pale *Alhamdulilah* mambo si mabaya, kwa sababu tumewakagua pale na tumeona mambo yao mazuri kabisa, yaani wanajiweza na wanaendelea

vizuri sana. Kwa hivyo, niwape hongera kwa kazi nzuri wanayoifanya. Mhe. Spika, wameiwezesha benki ile sasa kuwa inajiweza kabisa na kuingia kwenye ushindani na mabenki mengine. *(Makofi)*

Lakini kuna tatizo moja la pale Mhe. Spika kuhusu hatima ya wale wastaafu wa *PBZ* wale waliostaafishwa, kwa kweli kuna kizungumkuti pale. Mhe. Spika, suala hilo tumeshaliulizia na tulipata majibu pale ambayo ni tofauti na hali halisi. Kwa mfano, ukiwauliza watendaji pale wanakwambia kesi hii imekwisha na tumeshinda, lakini ukikutana na hao wastaafu wenyewe wanakwambia sisi tumshinda na ukiangalia maamuzi ya kesi unakuta ni kweli. *(Makofi)*

Sasa namuomba Mhe. Waziri atakapokuja atupe kinaga ubaga juu ya jambo hili, yaani wastaafu wale kesi ile wameshinda au wameshindwa, ikiwa wameshindwa basi aje na vielelezo vya kutuonesha kuwa wastaafu wale walishindwa na kesi pamoja na maamuzi yake ni haya hapa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nasisitiza tena kwamba aje na vielelezo vya kutuonesha kuwa wastaafu wale walishindwa na kesi pamoja na maamuzi haya na wala sio *documents* nimezisahau. Kwa hivyo, aje nazo hapa na tuzione na baadaye tukubaliane, ili na wenzetu hawa waondoke katika mashaka haya, kwa sababu ni muda mrefu na wamekuwa wakihanaishwa huku na kule bila ya kupata haki zao za msingi ambazo wamenyimwa kutokana na kustaafishwa kwao.

Mhe. Spika, kwa kweli mimi nilitaka zaidi niogelee katika suala la mali za serikali na ninashukuru *Alhamdulilah* nimepata uwezo huo na nimeogelea vizuri sana.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, bajeti hii siungi mkono. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Spika, mimi sina mengi isipokuwa nitakuwa na mawili tu. Lakini namuomba Mhe. Waziri hayo nitakayoyazungumza ayape kipaumbele, yaani ayaangalie kwa makini.

Nikianza mchango wangu moja kwa moja niende kwenye ukurasa wa 46 kuhusu Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Mhe. Spika, naipongeza serikali kwa kuanzia mfuko huu kwa kiasi kikubwa umewasaidia wafanyakazi hususani

wafanyakazi wa serikali wakati wanapofikia umri wao wa kustaafu. Lakini kuna baadhi ya wastaafu huwa wanapata usumbufu mkubwa sana wakati wanapomaliza muda wao wa utumishi hususani katika Kisiwa cha Pemba.

Vile vile baadhi ya wastaafu hawa huwa wanasumbuliwa sana na wanapodai mafao yao ya uzeeni hucheleweshwa au wakati mwengine kutofautiana na mafao hayo. Mhe. Spika, pengine waajiriwa hawa kuanza kupeleka mafao yao katika kipindi kimoja tu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri pamoja na serikali kwa jumla itoe taaluma kwa watumishi hawa kuhusu mwenendo mzima wa mafao kuanzia pale mapato wanapokusanya hadi wakati wa malipo.

Nikiondoka hapo sasa nije kwenye ukurasa wa 48 kuhusu Shirika la Bima. Mhe. Spika, nalipongeza sana shirika hili kwa kazi nzuri wanazozifanya kwa kutoa huduma za bima ambazo ni muhimu sana kwa maendeleo ya jamii pamoja na uchumi kwa jumla.

Mhe. Spika, jambo la kusikitisha katika Kisiwa cha Pemba Shirika la Bima pamoja na huduma zake nzuri, lakini bado wana matatizo ya afisi ya kufanyiakazi, ambapo watu hawa huwa wanayumba sana kwa kuazima nyumba kama vile kupanga na zile za kufanyiakazi. *(Makofi)*

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aliangalie sana tatizo hili la wafanyakazi hawa ambalo linalipa aibu hata na serikali kwa ujumla, kwa sababu watu hawa ikiwa hawana afisi za kufanyiakazi na kuyumba kwa kupangisha kila nyuma, basi pia itakuwa ni aibu kwa serikali yetu.

Kutokana na hali hiyo, naiomba wizara pamoja na serikali kwa jumla iwajengee afisi hii, ili waweze kufanyakazi vizuri na waache kupanga kila mahala pamoja na kuwaondoshea usumbufu. Mhe. Spika, baada ya hayo naomba nikaae kitako.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nami nishukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia bajeti hii muhimu katika maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, nianze kama kawaida yangu kumpongeza Mhe. Waziri, Mhe. Rais wa Zanzibar hakufanya kosa kumteua Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo Mhe. Omar Yussuf Mzee kutokana na uwezo pamoja uzoefu wake kuhusiana na mambo yanayohusiana na fedha.

Kwa kweli Mhe. Omar Yussuf Mzee ni mtu aliyesoma na kubobea katika fani fedha, vile vile ni mtu ambaye amepata uzoefu mzuri sana wakati alipokuwa kwenye wizara kama hii katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kumpongeza kutokana na uteuzi huo, tena naamini kwamba atafika mbali na ataifikisha nchi mbali katika suala zima la kunyanyua uchumi pamoja na maendeleo ya kiuchumi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo sasa naomba ninukuu kifungu cha nne kwenye ukurasa wa pili kuhusu majukumu makuu ya Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, Mhe. Waziri hapa ameainisha majukumu kama 9, lakini mimi nitaka nizungumzie majukumu matatu.

Ukurasa wa pili kifungu cha nne kinasema hivi:-

(i) Kusimamia ukusanyaji wa mapato,
(ii) Kusimamia uandaaji na utekelezaji wa bajeti ya serikali na
(iii) Kusimamia mali za serikali.

Mhe. Spika, nitazungumzia zaidi hayo majukumu matatu. Jukumu la kwanza katika kusimamia suala la mapato, kwa sababu tunafahamu kwamba kinachoendesha serikali, nchi pamoja na kinachokuza uchumi wa nchi ni mapato ya serikali na mapato yetu tunayapata kwa njia mbili kubwa. Kwanza ni suala la ukusanyaji wa mapato ya ndani, pia fedha tunazozipata kutoka kwa wahisani kwa njia ya mikopo na ruzuku.

Sasa fedha hizi za ndani Mhe. Spika, kama nilivyozoea kusema mara nyingi kwamba Zanzibar katika hali tuliyonayo sasa si masikini, iwapo tungeliweza kukusanya mapato vizuri na iwapo tungeliweza kudhibiti mapato yetu, basi hiki kidogo kama kingekuwa na udhibiti mzuri basi ninahakika kuwa Zanzibar ingepiga hatua kubwa ya kimaendeleo.

Lakini tatizo linalojitokeza Mhe. Spika, kutokana na ukweli kwamba mapato yetu kwa sehemu kubwa yanavuja, yaani kuna uvujaji mkubwa wa mapato ya serikali, kwa sababu mapato yanayokusanywa sio yanayofika katika serikali, yaani sio yanayoingia Hazina. Kwa kweli tuna tatizo la mapato kutokuyakusanya, pia kuna tatizo la kutokuwa na vyanzo vya uhakika vya mapato, vile vile kuna tatizo la kutokuyakusanya vizuri mapato pamoja na tatizo la uvujaji wa mapato.

Kwanza ni vyema Mhe. Spika, tukaweza kulijua tatizo hilo na kama waziri au wizara tuna wajibu wa kutafuta suluhu katika kuimarisha au kujenga uchumi pamoja na kuongeza mapato ya nchi, basi Mhe. Waziri ana jukumu la kujua sehemu hizo tatu. Vile vile ana jukumu la kuandaa mkakati maaluma

kuhakikisha kwamba mapato ya serikali, vyanzo vyote vya mapato vinajulikana na kutumika kama vilivyopo pamoja na suala la udhibiti wa mapato ya serikali.

Sasa suala la kusimamia mapato ya serikali au linalohusiana na mambo ya fedha Mhe. Spika, linasimamiwa na Sheria ya Fedha Nam. 12 ya mwaka 2005. Mhe. Spika, sheria hii ina matatizo au mapungufu na tangu iundwe tokea mwaka 2005 hadi sasa inakaribia miaka 6, hivyo ni vyema serikali ikaifanyia mapitio, ili kubaini mapungufu.

Mhe. Spika, takribani kupitia Kamati yangu ya *PAC* tumekuwa tukienda nao sheria hii, lakini mwahala mwingi inaonekana ina mapungufu hasa katika upande wa adhabu.

Kwa kweli sheria imeonesha mambo mengi lakini adhabu zake ni ndogo na sheria takribani haikugusa adhabu Mhe. Spika, sheria iliyokuwa haina adhabu huwa ina matatizo. Kutokana na adhabu zilizomo kwenye sheria ile ni ndogo sana na imeshapitwa na wakati na zinatoa fursa na mwanya watu kuiba mali za serikali pamoja na kuiba mapato ya serikali.

Kwa hivyo, naishauri wizara ifanye kadri inavyowezekana ifanye mapitio ya Sheria ya Fedha, ili iendani na wakati pamoja na mazingira tuliyonayo sasa.

Mhe. Spika, katika hilo na ndio maana wenzangu walizungumza hapa kwamba kuna tatizo maafisa hawa tunaowapa kazi ya kukusanya mapato. Mhe. Spika, ni tatizo kubwa, kwa sababu mapato mengi yanavuja katika sehemu hizo. Kwa mfano, ukienda Bandarini pale unatakiwa ulipe shilingi milioni 3 basi pale ni sawa na mnadani unapatana, yaani ukikubali kutoa shilingi 500,000/= au 1,000,000/= na mkakubaliana na afisa basi wewe utaoa chini ya hapo na kwa masharti nusu ziingie serikali na nusu ziingie kwenye mfuko wao.

Mhe. Spika, hilo ni suala la msingi na ninamuomba Mhe. Waziri pamoja na serikali kwa jumla iweze kulizingatia hilo. Mhe. Hija Hassan Hija ametaka watu wafanye uchunguzi na mimi nasema kwamba serikali lazima iweze kulifanyiakazi. Kwa mfano, vijana wadogo wanapoajiriwa ndani ya kipindi cha miezi 6 Mhe. Spika, mali wanazomiliki ni za ajabu sana na huo ni ushahidi tosha kwamba kunakuwa na uvujaji mkubwa sana kupitia maafisa wetu hawa, hivyo serikali haina budi kuliangalia hili.

Jambo jengine ambalo linahusiana na udhibiti wa mapato ni risiti hizi Mhe. Spika, kwa sababu mapato ya serikali yanakusanywa kupitia risiti za serikali. Sasa taarifa tulizonazo ni kwamba risiti za serikali zinachapishwa na mfanyabiashara binafsi. Mhe. Spika, kama hivyo ndivyo na hilo ni kweli basi

namuomba Mhe. Waziri atakapokuja atuthibitishie ni kweli kama risiti za serikali za kukusanyia mapato zinachapishwa na mfanya biashara binafsi na kama ni kweli itakuwa ni ajabu kubwa na aibu kubwa kwa serikali, risiti kuzichapisha kwa mtu binafsi kwa sababu risiti ni kitu nyeti sana na kitakiwa kiwe na ulinzi mkubwa sana.

Leo ikiwa tunampa mfanya biashara tu wa kawaida au tunaipa kampuni binafsi ya kuchapisha hizi na wakati Zanzibar tuna kiwanda chetu cha uchapishaji, tuna uhakika gani kwamba *order* tunayoitoa hapa haizidi ile *order* ambayo inahitajika. Kwa hivyo Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri atakapokuja anijibu hilo kuhusiana na suala zima la uchapishaji wa risiti.

Mhe. Spika, naomba nijikite kwenye jukumu la kusimamia uandaaji na utekelezaji wa bajeti ya serikali. Tunachokizungumza hapa ndani ya mwaka ni suala zima la bajeti ya serikali na utaratibu wa uandaaji wa bajeti unafahamika kwamba serikali ndio inayoandaa bajeti na serikali ikishaanda bajeti huileta mbele ya Baraza lako tukufu kwa ajili ya kuidhinisha bajeti, baada ya kuidhinisha sasa ni jukumu la Mdhibiti Mkuu na Mkaguzi Mkuu wa Hesbu za Serikali kuweza kuangalia na kudhibiti matumizi, lakini vile vile kuweza kudhibiti mapato, kudhibiti mahesabu ya serikali pamoja na kufanya ukaguzi wa mahisabu.

Mdhibiti anapotoa ripoti yake sasa ni jukumu la Baraza lako tena Mhe. Spika, kuweza kupitia ripoti ya Mdhibiti na kubaini yale yote ambayo yanayoonekana katika ukaguzi wake ule. Sasa Mheshimiwa bajeti ni kitu cha utaalam sana na wanaofanya bajeti ni wataalam kutoka Wizara ya Fedha, Uchumi, Mipango ya Maendeleo na wanaofanya ukaguzi ni wataalam kutoka ofisi ya Mdhibiti, lakini hawa wanaopitia ripoti za Mdhibiti na hatimae kutoa ripoti serikalini ni Baraza lako hili kupitia kamati yake ya *PAC* .

Sasa hoja yangu hapo ikiwa utaratibu wa uandaaji wa bejeti ni huo inatoka serikalini inakuja kwenye Baraza la Wawakilishi, inarudi kwenye Ofisi ya Mdhibiti na baadae mwisho inakuja tena kwenye Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kutolewa ripoti kupitia kamati ya *PAC*, ni dhahiri utaona Mhe. Spika, kwamba kamati yako hii ya *PAC* inahitaji kuwa na uwezo mkubwa sana kitaalam katika ufuatiliaji wa ripoti za mdhibiti.

Vyenginevyo kamati hii kwa sababu inaundwa na wajumbe tofauti na wajumbe wenye uelewa tofauti, wajumbe ambao hawana uwezo wa kuchambua mambo haya ya mahesabu kama hatutowawezesha Mhe. Spika, tusitegemee kwamba itafika mwisho wa siku Baraza hili litawatendea haki wananchi kupitia ripoti za Mdhibiti.

Mhe. Spika, ninachosisitiza kwa hapa kwa Wizara ya Fedha kwa sababu ndio walezi wa sheria ya fedha, Wizara ya Fedha ndio walezi wa sheria za manunuzi, kwa hivyo ni wajibu wa Wizara ya Fedha kuona umuhimu wa kuandaa *program* maalum kwa ajili ya kuiwezesha kamati ya *PAC* kuweza kufanya kazi zake kwa vizuri. Kuna tatizo la elimu inayohusiana na mambo hasa ya uandaaji wa bajeti wenyewe wanaita *MTEF*. Hii ni elimu kubwa hasa sisi wajumbe wako hatujui hata namna ya uandaaji wa bajeti hii na elimu hii hatujapata na kamati inayohusika haijapata. Sasa kama ikiwa haijatuwezesha nasema kwamba tunachokifanya hatukielewi na mwisho wa siku tutakuwa wananchi hatuwatendei haki.

Kwa hivyo sisitizo langu kwa hapa Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri alizingatie hili kwa mapana yake ili mwisho wa siku kamati iwe na uwezo mzuri sana, kamati iwe na uwezo mkubwa sana wa kufanya uchambuzi wa bajeti, wa kufanya uchambuzi wa mapitio ya sheria za fedha na sheria za manunuzi pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Lakini vile vile Mhe. Spika, katika hilo nielezee umuhimu kwa serikali kwa sababu mwisho wa kamati inapotoa ripoti yake hutoa mapendekezo yake kwa serikali ili serikali iyafanyie kazi, taban Mhe. Spika, mara nyingi hapa kamati imekuwa ikionesha matatizo mengi yaliyojitokeza kupitia ripoti hiyo. Lakini serikali haijaja hata siku moja ikatueleza kati ya ripoti zile zilizotolewa na kamati kupitia Baraza lako hili ni hatua gani zimechukuliwa kwa wale ambao wameonekana na matatizo ya ufujaji wa mali za serikali pamoja na fedha za serikali.

Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri na pia naliomba Baraza hili na naiomba serikali kwa ujumla iweze kuzifanyia kazi ripoti hizi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za serikali zinazoletwa mbele ya Baraza lako ili tufike pahala tuone kwamba kunakuwa na utendaji na utawala bora uliotukuka katika nchi yetu.

Mhe. Spika, sasa nizungumzie kazi ile ya tatu ya wizara hii inayohusiana na mali za serikali, katika tatizo kubwa linaloiandama serikali hii ni suala zima la upotevu wa mali za serikali, tuna tatizo kubwa sana katika serikali, ni tatizo ambalo nahitaji majibu sahihi ya serikali kwanza kwa kuhakikisha kwamba mali zote za serikali inazifahamu mali zake zote.

Tatizo kubwa leo kwamba serikali haijui mali zake ni ngapi na mali zake ziko wapi na zipi hili ni tatizo na ni tatizo kwamba hadi leo tunashindwa kuandaa *ficture register* mpaka leo serikalini hakuna unapopita katika Mawizara na Maidara hakuna buku linaloonesha mali za serikali. Mimi nadhani inafanywa

kwa makusudi ili wajanja wachache waendelee kujitwalia mali za serikali. Katika hili Wizara ya Fedha ndio wanaongoza kwa sababu wao ndio wenye idara hasa inayohusikana na mambo haya ya uhakiki mali.

Sasa sisi kama Wawakilishi wa wananchi hatutovumilia kuona mali za serikali zinagaiwa kama mali ya sadaka, kwa watu ambao hawahusiki watu wa kujineemesha na watu kujitajirisha kupitia mali hizo. Sasa tunaiomba serikali iweze kutupa jibu maana yake inaonekana mchezo huu hauna mwisho, kawaida mchezo wa sinema saa tatu huwa unamalizika lakini mchezo huu hauna mwisho na kadri kamati zako zinapokwenda katika kufanya kazi tunababaishwa babaishwa na watendaji, hakuna *formular* moja wengine hata ile kurekodi hakuna. Sasa mimi nataka tutoe muda maalum kwa serikali kwamba tuhakikishe wizara inayohusika na mambo yanayohusiana na mali za serikali idara ile ya uhakiki mali itupe jawabu rasmi ni lini serikali itakuwa imeshaandaa utaratibu wa kuzitambua mali zake.

Katika hili Mhe. Spika, linahitaji uwezo maana suala la urekodi wa mali za serikali kunahitaji uwezo na uwezo ni uwezo wa kibajeti, nimuulize Mhe. Waziri ili suala hili lisiendelee kuwa ni hadithi katika serikali kwa bajeti ya mwaka huu wameandaa kiasi gani

Mhe. Spika, kuikamilisha kazi hii katika maidara na Mawizara mbali mbali. Nilisema katika Baraza lako kwamba kuna utaratibu ambao si mzuri na sasa hivi wa kulitumia vibaya jina la Rais, katika hili kumezuka mtindo kwa baadhi ya taasisi za serikali, kuna ujanja fulani unaoendelea katika taasisi za serikali hususan katika kumiliki viwanja vya serikali. Nafahamu kuna tatizo la miundombinu na kiwanja chake cha Mtoni, nafahamu katika kiwanja hiki kilichozungumzwa juzi kilichopo Mabluu pale na nafahamu hata Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko kwa kiwanja chake kilichoko katika maeneo ya Mabatini, viwanja vyote hivi vilikuwa ni milki ya serikali lakini ujanja unaofanyika ni nini? wakubwa wanapoona hii ni mbinu sasa ya kutaka kujipatia fedha hujaribu kukichukua kwanja kile na kurejesha serikalini na kiwanja kinapofika serikalini hutolewa akauziwa tajiri fedha nyingi sana.

Sasa hii ni mbinu ambayo tayari tumeshaigundua kwamba ni ujanja maalum unaofanywa na baadhi ya viongozi kuweza kuvihaulisha kuvirejesha serikalini na baadae vikitoka serikalini kuuziwa wafanya biashara binafsi, nimetaja viwanja hivyo vitatu kwamba tayari vimeshapitia kwenye mkondo huo. Mhe. Spika, katika hili tunahitaji maelezo tena yawe ya kina yasiwe ya kijuu juu tu ambayo kwa kweli hapa tutakujapata tatizo wenzangu wameshadai mikataba mimi bado sijadai mikataba lakini naomba tupate maelezo ya kina juu ya hili.

Mhe. Spika, kuna mradi huu kuendeleza kazi ya mradi wa *ZANCAT* katika ukurasa wa 17 hiyo imo katika ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali na mradi huo umetengewa shilingi milioni 946 lakini bahati mbaya haukutolewa maelezo ya aina yoyote huu ni mradi gain. Mhe. Waziri hebu tupe maelezo huu mradi ili na sisi tuweze kukuidhinishia fedha au tuweze kuzinyima fedha hizi.

Mhe. Spika, mfuko wa *ZSSF* tulinung'unika sana hapa katika Baraza lako hili kwamba tunahitaji kubadilisha sheria ile ili wafanyakazi hawa watakaokuwa hawakutimiza muda ule wa kustaafu, mtu inapotokea kustaafu ama inapotokea kupata tatizo lolote lile la kazini aweze kupata haki yake, lakini kusubiri mfanyakazi yule mpaka kufika miaka sitini kwa kweli ni unyang'anyi wa mchana.

Serikali yetu hii ya awamu ya saba Mhe. Spika, haifanyi kazi ya kunyang'anya na kama haifanyi kazi hiyo, maana yake sasa tunahitaji tupate marekebisho ya sheria ile ili wafanyakazi waendelee kuwekeza fedha katika mfuko na mtu anapopata tatizo lolote lile ama la kustaafu alipwe haki yake ili aendeshe maisha. Lakini si hoja ukaambiwa mtu asubiriwe mpaka afe maana yake miaka sitini sasa hivi kufika ni matatizo, huku mtu anakusanya fedha yake kwa kutegemea kutumia mwenyewe hategemei kukusanya fedha waje kutumia wajukuu hiyo sio lengo. Mhe. Spika, ukusanye pesa yako umalize kustaafu upige tasi mwenyewe sasa tunahitaji turekebishe sheria ile ili watu wapate haki zao kabla hawajafa.

Mhe. Spika, kwa sababu wizara hii ndio wizara ninayoifanyia kazi muda mwingi naomba Mhe. Waziri aje kunijibu masuala yangu hayo ili tuangalie ili somo yangu nimpitishie au tumpigie buti. Mhe. Spika, nashukuru ahsante sana.

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuweza kuchangia mawili matatu katika hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha Uchumi Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Spika, kwa kuanza kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima salama na uhai na kuweza kufika hapa na kuendelea na taratibu zetu, lakini pia nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba hii. Tatu nimshukuru Mhe. Waziri wa Fedha pamoja na kamati yake kwa kututayarishia bajeti hii na kutuletea hapa tukaweza kuiona leo kwa kuja kuisoma pamoja na kuijadili.

Mhe. Spika, kwa kuanza naanza na suala la utaratibu wa ajira ndani ya *TRA*. Tunamuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atufahamishe namna gani vijana wetu wa Kizanzibari wanavyofanya taratibu za uajiri ndani ya *TRA* na hadi hivi

sasa vijana wetu wa Kizanzibari wanaendelea vipi na taratibu za kimasomo pale ambapo nafasi zinapatikana kwa ajili ya kwenda kuongeza taaluma na ujuzi katika vyuo mbali mbali vya ndani na nje ya nchi yetu ya Tanzania.

Nikihama hapo Mhe. Spika, nakuja katika malipo ya magari ya abiria. Juzi tulipokuwa tunachangia katika bajeti ya Wizara ya Utalii hapa tulisema kwamba tuna utaratibu ambao tulikuwa tumeupitisha hapo, watu wenye magari ya kubeba abiria watu hawa unapofika mwisho wa mwaka hutakiwa kulipa malipo ya kukata leseni kwa sababu ya kuhudumia huduma mbali mbali, kuna magari yanakatiwa leseni kwa sababu ya kuchukua abiria wa kawaida.

Kuna magari yanakatiwa leseni kwa ajili ya kuchukua wazungu na kuwapeleka katika maeneo yao ambayo watakuwa nayo kwa wakati ule ambao watakuwa wapo hapa. Chakushangaza na kushtusha zaidi Mhe. Spika, ni kuona kwamba watu wale pamoja na kuwa tumeshawakatisha leseni za mwaka mzima wanapobeba abiria wanatakiwa wapite Bwawani wakakate vibali vyengine wakafanye malipo mengine kwa sababu tu wamebeba watalii.

Sasa Mhe. Spika, hebu Mhe. Waziri atufahamishe maana ya kukata zile leseni katika *grade* ile na sifa ile ilikuwa ni nini hata ikabidi sasa wanapotaka kupakia hao wazungu wenyewe waende tena kukata vibali vyengine au wakafanye mambo mengine ndipo wapate haki ya kuweza kupakia hao wazungu ambao tayari washawakatia leseni.

Jengine Mhe. Spika, naondoka sasa katika ofisi za *TRA* na *ZRB* na kwenda *ZIPA* Mhe. Spika, kuna hoteli mbili hizi ambazo katika matembezi ya kamati yetu ya fedha biashara na kilimo tulitembelea na kuona kwamba kuna matatizo. Tunamuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atuelezee maelekezo na maamuzi pamoja na utaratibu mzima uliofikiwa juu ya suala la Hoteli ya Mpapindi Pemba pamoja na hoteli ya Venta Club Kaskazini Unguja. Tunaomba maelekezo ya kina katika hoteli hizi mbili ili tuweze kujua kwamba hawa wawekezaji ambao wako hapa wataruhusiwa kuendelea na kazi watafungiwa ili hatua za kiserikali ziweze kuchukuliwa na hawa watu ambao wana matatizo katika maeneo haya yaweze kutatuliwa matatizo yao. wani katika hawa kuna maeneo ambao wana madeni yao hapa na muda umekuwa mrefu mno. Sasa Mhe. Spika, Mhe. Waziri atakapokuja hapa tunamuomba atusaidie kutufahamisha katika masuala ya kadhia hizi mbili.

Mhe. Spika, sasa nakuja katika suala la *JFC*. Mwezi wa oktoba mwaka 2006 tume ya pamoja ya kusimamia fedha baina ya serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliundwa, tume hii inasimamiwa shughuli zake na Jaji Mstaafu Mzee wetu Shelupindo.

Chakuchangaza na kusajabisha Mhe. Spika, ni kuona kwamba tume hii hadi hivi sasa kazi ambazo inaendelea nazo hazijafikia kikomo katika utekelezaji wake.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa maelekezo ya hotuba ya Mawaziri wetu wote wawili tukiangalia taarifa ya Waziri wa Zanzibar wa Fedha na Uchumi na Waziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, suala hili bado lipo katika hatua za maongezi mpala leo utekelezaji wake haujaanza, kwa ruhusa yako tunamuomba Mhe. Waziri wa Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo aje atwambie hasa leo tatizo la kutokukamilika utekelezaji wa tume hii ni kitu gani, kwa sababu bado tunaendelea kupata hadithi tu mpaka leo, tunaomba maelekezo ya kina kitu gani hasa kimekwamisha ndani ya muda wa miaka mitano tume hii ikawa haijakamilisha bado kazi yake mpaka leo.

Mhe. Spika, baada ya maelekezo haya sasa nije kwenye suala la uhaulishaji wa mizigo baina ya Zanzibar na upande wa pili wa Muungano. Wenzangu waliokuja hapa kuzungumza wamelizungumza sana suala hili limezungumzwa katika sekta nyingi sana na mwisho wa habari hata katika suala la jana katika bajeti ya Waziri wa Biashara suala hili Mhe. Ismail Jussa Ladhu alilizungumza sana. Lakini bado Mhe. Spika matatizo ya uhaulishaji wa mizigo kutoka sehemu moja ya muungano kwenda sehemu nyengine yako pale pale.

Kwa mujibu wa sheria za *TRA* ni kwamba mzigo unapofika *Airport au port* yoyote inayoingilia ndipo inapotakiwa kufanyiwa malipo, na mtu anayekuwepo pale wakati ni mtu wa *custom* na ni mtu ambaye anaaminika na mamlaka ya *TRA* basi ina maana kitu kile kimekubalika kwamba kimeingia katika taratibu zinazostahiki. Sasa kinachoshangaza Mhe. Spika, mzigo ule unapotoka tena sehemu moja kwanda sehemu nyengine kuja kulipishwa tena na hapa pamoja na maelekezo mazuri ambayo Mhe. Waziri mara zote anakuwa anayatoa kwamba hawa wanaochaji pesa hizi za ziada kinyume cha taratibu. Sasa kama mambo haya yanafanyika kinyume cha taratibu kwa nini kama serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tunakubali bado watu wetu waendelee kudhalilishwa, kuteswa na kunyanyaswa katika masuala kama haya.

Mhe. Spika, baada ya maelekezo haya kwa heshima na taadhima naomba kufikia hapa na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nashukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa ya kuchangia mawili matatu katika hotuba hii ya Waziri wa Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Mhe. Spika, mchango wangu mimi kwa sababu hii ni Wizara ya kitaalamu ya Fedha na Uchumi na mimi sio mchumi kwa hivyo nitakuwa na machache sana.

Mhe. Spika, kwanza mimi namuomba Mhe. Waziri kwa sababu sina utaalamu wa mambo haya ya fedha anisaidie kuhusu benki hii ya matajiri wakuu iliyopo pale Shangani, hii benki nasikia kuna matajiri saba ambao wanaitumia hii benki. Sasa naomba Mhe. Waziri anielimishe kwamba je hii benki kunakuwa na vigezo maalum vya fedha kiasi gani zinatakiwa ziwe nazo ndio ziweze kutumia ile benki, au ile benki inatumika na mtu yoyote yule anayetaka kuitumia benki ile pale. Kwa sababu wasi wasi wangu mimi ni kwamba benki ikiwa ina watu maalum kuna siri gani ndani yake mpaka iwe ina watu maaluma wanaotumia, na ikiwa ni benki ya matajiri watupu ukionekana unaingia kwenye benki ile unakuwa unaonekana kwamba wewe ni tajiri kwa upande mwengine haiwezi kuhatarisha maisha ya watu wetu.

Kwa sababu unabagua watu wanajua kwamba anayeingia mule ni mtu tajiri kwa kuwa wanaoingia mule ni matajiri peke yao wenye pesa nyingi, je kwa upande mmoja haiwezi kumhatarishia maisha mtu wetu. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri anielimishe kwa hayo kwa sababu na mimi ninaweza kuwa na vijisenti vyangu nikataka kwenda kuweka kule benki, sasa nijue je kuna kiwango maalum cha benki hizi.

Jambo jengine nataka kumuomba Mhe. Waziri anisaidie kuhusu hatma ya jengo lile la Wizara ya Fedha na Uchumi lilioko Tibirinzi, pamoja na kuwa wenzangu walilizungumza lakini na mimi naomba Mhe. Waziri atupe hoja nzuri ambazo zitakuwa zinatuweka katika mstari mpaka tuweze kuvumilia, kwa sababu kipindi cha bajeti iliyopita tulilizungumza sana na mara hii tunalizungumza tena kwa sababu pale ni fedha nyingi za serikali ambazo zimetumika kiholela.

Leo jengo lile saa hizi halina maana ya kitu chochote, huwezi kufanya kitu chochote na sasa hivi Mhe, Waziri amekuja tena kutuomba fedha kwa ajili ya kujenga jengo jengine. Sasa je kwanza tulitaka tujue lile jengo linataka kuvunjwa au kuna kiwanja chengine ambacho kinataka kujengwa. Je, na zile fedha zetu zilizopotea pale ndio zimeshapotea moja kwa moja na kuna sababu gani ya msingi mpaka leo ikawa mkandarasi yule mpaka leo serikali ina kigugumizi wanasema wanaandaa sasa utaratibu wa kumshtaki wakati ametupotezea fedha nyingi kweli kweli.

Leo badala ya kumshtaki unasema unaandaa utaratibu hivi sasa kwa nini utaratibu uwe na msururu wa kuandaa, uwe unachukua muda mkubwa wa kuandaa, kwa nini mtu ameshatuharibia sisi tumuonee haya kwa sababu kuandaa utaratibu ni kumuonea haya, kwa nini tumuonee haya mtu aliyetuharibia mapesa yetu. Kwa hivyo sisi tunaamini kwa mawazo yetu hapa kuandaa utaratibu kuna mbinu za watu na mkono wa watu ambao

umejinufaisha sasa wanaona wakimsakama kwa nguvu atawafedhehesha. Kwa hivyo hapa tunataka kitolewe kigugumizi serikali itueleze kuhusu fedha zile zilizoteketea pale.

Mhe. Spika, suala jengine ninalotaka kuzungumza ni suala la serikali yetu kutumia fedha nyingi kujenga majengo ya serikali na ikawa wanatumia fedha nyingii kama vile sisi ni matajiri wenye fedha, wakati sisi ni nchi masikini. Sasa utaratibu huu unaotumika ni utaratibu wa kutumia fedha nyingi kama nchi za ulaya ambazo zinaendelea na wakati sisi ni nchi masikini. Mfano wa mambo haya au majengo haya ni majengo yanayojengwa ya *ZRB,* haya majengo yanajengwa kwa pesa nyingi na wakati sisi hatuna uwezo wa kujenga majengo kama yale. Sasa fedha nyingi za walipa kodi tunazitumia kwa ajili ya kujenga majengo na wakati sisi huku ni watu tunaotegemea misaada.

Sasa namuomba Mhe. Waziri atueleze kama yale majengo yanayojengwa ya *ZRB* hivi sasa yameshatumia kiasi gani cha fedha, na hata yakimalizika yanatarajiwa kutumia fedha gani. Kwa mfano wenzetu wa Tanzania Bara kipindi kilichopita siku za nyuma kuna benki ya *BoT* ilijenga majengo kule na wananchi walitumia fedha nyingi, kwa hivyo walihoji majengo yale na ikawa utata mkubwa. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri atueleze majengo haya hivi sasa yameshatumia kiasi gani cha fedha na yanatarajiwa kumalizika kwa kutumia mamilioni mangapi, wakati sisi huku bajeti yetu mpaka tuombe leo wahisani fedha watatuamini vipi wakati sisi ni masikini na tunajenga majengo ya kifahari makubwa kama ya watu wanaoendelea, Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri atakapokuja na hili atueleze.

Mhe. Spika, kwa sababu mimi nimekwambia si mtaalam wa fedha na bajeti hii inatumia mambo ya fedha na uchumi, na mimi sio mchumi kwa hivyo mchango wangu utakuwa mfupi. Kwa hayo machache naomba kujibiwa na bajeti hii mimi siko tayari kuunga mkono.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuto mchango wangu katika bajeti hii ya serikali, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo na afya njema ya kuweza kuchangia bajeti hii, pia nimshukuru Mhe. Waziri na wataalam wake wote waliotayarisha bajeti hii na kuiwasilisha.

Mhe. Spika, mimi nitakuwa na mchangio katika maeneo matano eneo moja zaidi nimetumwa na jimbo langu la Mfenesini na maeneo mengine ni kutoa mawazo ya wananchi wangu vile vile, eneo la mwanzo ninalotaka kulichangia liko ukurasa wa 28 linazungumzia juu ya mfuko wa barabara, pale Mhe. Waziri ametueleza kwamba mfuko ule una malengo yafutayo.

Kwanza kukarabati barabara katika maeneo yaliyoharibika sehemu kubwa, pili kufanya matengenezo sehemu zenye matatizo na tatu kutengeneza sehemu zilizotokea dharura, bahati nzuri au bahati mbaya katika jimbo langu katika masika yaliyopita mwaka jana na mwaka huu pana njia ipo pale Kihinani inaendea mashimo ya mchanga. Pale pahala pana kijimto kilichounganisha na mto wa Kihinani Meli Nane. Yanapokuja Masika wanashindwa watoto kuvuka kwenye mto huo kuja upande wa pili ili waende shule au kutumwa madukani.

Mhe. Spika, tukawahi kuwachukua wataalamu wa *UUB* wakaja wakafanya makisio na tukapata shilingi milioni 5 ili kuweza kuondosha tatizo hilo, ili waweke bomba na kifusi ili masika na Kaskazi papitike kwa uhakika. Makisio yale tukaelekezwa tuyapeleke katika mfuko huu. Tumeyapeleka na tumekabidhi na *copy* nyengine nnazo. Sasa namuomba sana Mheshimiwa swahibu wangu, kwamba bado kilio kile hakijamalizika na hatujapata jibu. Namuomba kwa hisani kubwa, awaonee huruma wananchi wa jimbo la Mfenesini wa Shehia ya Kihinani, ombi hili tukimaliza bajeti alitizame na akitaka copy nitamletea ili masika yatakayofuata tusipate tatizo hili.

Suala jengine, katika jimbo langu kuna vijiji vingi lakini kijiji ambacho kipo mbali sana na barabara kuu inayotokea mjini ni kijiji cha Mwachalale eneo la Mwakaje. Kule tayari tumeshajitahidi wananchi pamoja na sisi viongozi kupeleka mambo yote ya jamii, tumeshajenga shule, tumeshapeleka maji, tumeshapeleka umeme na sasa tunamaliza kituo cha Afya. Ili tusiwape wananchi tabu kuja Selem au kwenda kwa rafiki yangu Mshimba, Kitope. Kilichobakia sasa hivi kituo baadae kuomba wataalamu.

Kilio chetu cha kijiji kile ni barabara ambayo kila yakisha masika tunatumia si chini ya milioni 18 kutia kifusi kutoka Mwakaje kwenye Mwachalale. Hizo ni nguvu za wananchi pamoja na sisi viongozi wao pamoja na wadau wa maendeleo. Ninachoshauri kwamba kuwa tumeshajua tatizo kila masika yakisha zinatakiwa milioni 18 na inakuwa mzigo mkubwa kwa hali ya umasikini na unyonge tulionao. Sisi waheshimiwa mikono mirefu lakini tuna mengi. Mimi nina shehia saba pale na zote zinahitaji, sasa kama milioni 18 nitakuwa nazipeleka Mwachalale tu, sehemu nyengine itakuwa tunawadhulumu.

Sasa naiomba Wizara angalau wangetutilia lami ya rojo na kifusi, ile faida yake ni kwamba maji inakuwa hayachukui kifusi inakuwa maji yanapita juu tu, yanateleza. Namuomba na hilo vile vile tukimaliza wataalamu wapo waende wakafanye makisio kama bado zile zile mioni 18 au zitapungua ili kilio hichi cha barabara kwa upande wa Mwachalale kimalizike. Namuomba sana haya ni mambo muhimu nimetumwa.

Nikiendelea katika mchango wangu nije kwenye ukurasa wa 46, Mashirika yetu tuliyonayo. Kwanza nitaanza katika mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Kwanza naupongeza sana mfuko sio wa muda mrefu lakini maendeleo yake makubwa. Tayari sasa hivi wamewekeza katika majengo ya Unguja na Pemba. Nadhani wanafanya biashara kubwa kuhifadhi mfuko wa wafanyakazi. Lakini nilikuwa nina mashauri mawili katika mfuko huu. Moja mwenzangu kaligusa kidogo lakini mimi nitalizungumza kwa upande mwengine.

Muda mwingi mfuko ninavyoona hapo mwanzo ulikuwa umelenga sana kwa wafanyakazi wa serikali, kwa sababu wao ndio wanaojaza mikataba ya mtu kustaafu miaka 60 kwa mwanamme na kwa mwanamke miaka 55. Lakini haya mashirika yetu ya utalii, watu binafsi hawana mikataba kama hiyo, mikataba yao mifupi. Unakwenda pale na utaalamu wako mkataba wako ni wa mwaka mmoja tu, unaondoka. Unaambiwa ungojee miaka sitini ukachukue kiinua chako mgongo. Inakuwa kinyumenyume haieleweki, wananchi wanateseka.

Ningeshauri hiyo sheria ikirekebishwa ieleze kwamba mashirika yote mtu akimaliza apewe chake, akenda kuongeza mke, akila tasi, akenda kujenga, hiyari yake kadiri mwenyewe atakavyojipangia. Hili la serikali tuiwache kama ilivyo mtu akimaliza miaka 60 anaondoka yeye anakuja mwenzake anachukua pencheni yake. Lakini katika taasisi za watu binafsi na mahoteli na maeneo mengine ni ngumu kungoja miaka 60 hakuna mkataba huo. Mkataba mkubwa wa miaka miwili. Hoteli zenyewe watu wajanja wajanja leo Venta, kesho Vera, keshokutwa Mafarasi. Kila baada ya miaka miwili wanabadilisha mtu anachukua chake anaondoka. Kwa kuwa sio kazi ya kuendelea hilo tunalijua.

Sasa ningeshauri katika marekebisho ya Sheria hii katika sekta binafsi zote mtu mkataba akimaliza apewe chake. Nadhani hii itasaidia sana kuendeleza utaratibu huu wa mfuko wetu.

Pia nawashauri wa mfuko kwamba Zanzibar na Pemba wameshawekeza sana, lakini kisoko la biashara kwetu ni dogo. Ningeshauri na wao wakavuka mpaka wakendazao Dar-es-Salaam, Arusha, Mbeya kwenda kuwekeza kibiashara. Watanufaika zaidi na kwa kipindi kifupi. Naomba na hili wataalamu kama wapo wanatusikia basi waweze kufanya hivyo. Wenzetu Bara biashara ni kubwa na wigo mpana kuliko hapa petu. Nadhani watapata kipato kikubwa kwa muda mfupi. Nashauri hilo kama litakuwa lina manufaa kwao basi tungejaribu kulifanyia kazi.

Nikiendelea na mchango wangu nije kwenye shirika jengine la Benki ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*) kwanza niipongeze kwa kazi kubwa. Kitabu kimetueleza kwamba wamepata manufaa na mfuko wao umetuna katika kuendesha biashara

zao. Tunawashukuru na wao tayari kitabu kimetueleza kwamba wameshafungua tawi Dar-es-Salaam ili kuweza kutanua wito wa kibiashara. Nawambia na wao pia wasisite hapo wasogee Arusha, biashara kubwa, Mwanza biashara kubwa.

Mhe. Spika, sisi Kamati yako tayari tumekwenda Mwanza kuangalia tawi la Bima na Arusha kwa kweli kazi nzuri sana. Kipato cha Arusha kwa mwezi mmoja hapa petu anakaa mwaka mzima hawajakipata. Sasa nadhani na Benki ikenda huko (*PBZ*) itapata kusaidia sana kuendeleza mtaji wao.

Pia nilikuwa nina ushauri katika benki yetu ya watu wa Zanzibar. Kwanza tunawapongeza wanatukopesha sisi waheshimiwa, wafanyabiashara na watu wadogo wadogo wa vikundi *SACCOS*. Lakini bado kilio chetu kwamba wameeleza pesa nyingi sana humu wametukopesha ni milioni 53.2 ni pesa nyingi sana katika kuekeza. Nadhani na wao wanapata faida kubwa sana. Ningeliomba jambo la msingi kama zaidi watahitaji wateja basi wangelitupunguzia riba. Riba bado ni kubwa na petu sasa hivi tuna matawi ya benki yanafika 16 yote ni ushindani wa mikopo. Sasa naomba benki yetu itupunguzie riba ili tuweze kukopa zaidi.

Jengine niwashukuru kwamba wamefungua Benki ya Kiislamu. Benki ya Kiislamu tumefanyiwa semina lakini wananchi wangu bado hawajaelewa. Na mimi nilikuwa nina suala nataka nimuulize Mhe. Waziri akija atupe ufafanuzi ili na wananchi wanaosikiliza waweze kutambua.

Benki hii masharti yake hupewi pesa kesh kama *PBZ* na Benki nyengine. Unakwenda pale unasema nataka nyumba nimeiyona ama nataka gari, kabila unaitaja. Wanakwambia wao wanakwenda kwenye soko, watainunua halafu watakulipia wewe utalipa fedha kwao. Sasa mimi nimehitaji gari au nyumba je, mkulima anayetaka mbegu, ayataka kuchimbuliwa konde, mbolea, dawa za wadudu, sasa yeye afanye utaratibu gani ili aweze akakope kwenye benki hiyo.

Ningeliomba tukapata ufafanuzi zaidi ili na wakulima na wao waweze kuitumia benki hii ili iweze kuwasaidia katika kilimo, mifugo, uvuvi. Kubwa lilozungumzwa kama watu wafanyabiashara wanataka gari, nyumba, shamba lakini wakulima wanataka kukopa je, wafanye utaratibu gani? Naomba hilo Mheshimiwa ukitoa ufafanuzi inaweza kuwa wenzetu huko wakaweza kusikia.

Nije suala la nne Shirila la Bima, nalo nalipongeza kwa kazi kubwa na matawi waliyokuwa wameshafungua Bara kwa kweli yanawapa faida kubwa. Wameweza kujenga jengo lao la kisasa kabisa na watahama kule kwa zamani wahamie kule kwenye jengo lao, tunawapongeza sana.

Lakini na hapa nilikuwa niombe serikali kuuliza swali moja vile vile. Hivi sasa nchi nyingi duniani nadhani na Tanzania Bara tayari wamewawekea wafanyakazi wao bila ya afya. Lakini bado vitabu vyote vilivyosomwa kwenye bajeti hii si cha Afya, si cha serikali, si cha uwezeshaji, hapakugusiwa suala hilo. Nilikuwa nataka nimuulize Mhe. Waziri je, serikali yetu inawatizamaje watizamaji wake juu ya suala zima la afya. Kwa sababu binaadamu sio kama samaki, nasikia samaki kila akipea anazidi nguvu, lakini sisi kila tukipea tunapugua nguvu na baadaye tunakuwa vizee kabisa, baada ya kuendea miguu miwili inakuwa na mgokongojo unakuwa mguu wa tatu.

Tungeliomba na serikali ina mpango gani juu ya suala hili kwa wafanyakazi wake. Kama lipo basi tupate kama halipo wanalifikiria vipi. Ni jambo muhimu kwa sababu binaadamu kuna siku anakuwa mzima na kuna siku anaumwa. Huduma za afya sasa hivi zinagharama yake. Naliomba hili serikali tupate jibu ili wananchi na wafanyakazi waweze kutambua hilo.

Nije, kwenye mchango wangu wa tano ukurasa wa 23 Idara ya Fedha za Nje. Hapa tumeelezwa kwamba Idara ya Fedha za Nje zinahusika na kusimamia misaada kutoka nje, ruzuku, mikopo na kadhalika. Nilitaka nijue katika Idara hii kwa kipindi hichi cha bajeti inayoendelea tumepata msaada wa kiasi gani kutoka nje, kwenye bajeti kubwa ya serikali, lakini katika msaada wa kuendesha hii bajeti yetu. Kwa sababu tunasikia kuna nchi zinasaidia mabajeti ya serikali wakati wa kipindi kama hichi.

Mfano Tanzania Bara kuna fungu linatoka nje linasaidia mabenki mbali mbali ili kuendesha bajeti yao. Sasa na mimi niulize sisi katika bajeti hii kuna msaada wowote. Je, katika bajeti ya serikali kuna msaada wowote vile vile ambao tumeupata tuelezwe ili tujue. Au kama kuna ruzuku vile vile tuweze kufahamu imetusaidiaje na kiasi gani ruzuku hiyo, ili tuweze kujua na sisi tumesaidiwaje katika bajeti yetu.

Mhe. Spika, mwisho kabisa na mimi sikutaka kuwa na mchango mrefu nilitaka kidogo tu nitoe mawazo yangu. Mwisho katika bajeti hii nadhani takriban nusu ya wizara kwamba mishahara ya wafanyakazi inaishia katika miezi 9, miezi mitatu ya mwisho mengine inakuwa haijakamilika hasa kipindi cha nyuma kilichopita. Tukafanya hofu tukauliza tukaambiwa kuna fungu limetengwa la kuweka hakiba kama litatokea hilo basi litachukuliwa ili liweze kufidia. Mimi nilikuwa nina wasi wasi mmoja kwamba mimi nina familia ya watu watano nyumbani ikifika mwisho wa mwezi nafanya makisio kwamba polo moja la mchele, kilo 50 za sukari, kilo 50 za unga, kilo 25 za vitu vyengine. Sasa nakwenda mpaka nikimaliza muda wangu najua hapa ndipo nilipofikia nimeshafanya makisio kwa kitu ninachokijua.

Ningeshauri serikali nayo ingefanya sensa ya wafanyakazi wote walionao ili kuondosha kitu cha kukisia. Kitu cha kukisia unaweza ukafikia lengo au unaweza usifike lengo, haki za watu kama hivi kama hukufika lengo ndio unawatesa. Kwa sababu ukifika tarehe 30 inakuwa unawalipa kwa siku 45 mbele, itakuwa haipendezi wakati serikali yetu imeanza vizuri. Sasa naomba hilo lifanywa litasaidia hata ile mishahara hewa itaondoka. Mhe. Spika, baada ya mchango wangu huo na mimi naunga mkono hoja. Nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mhe: Amina Iddi Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi name nichangie hotuba ya Mhe. Waziri. Awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia kuwa wahai na wazima. Lakini pia kanijaalia kunipa pumzi ya kuweza kusimama mbele ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, pia nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa namna alivyokiandaa kitabu hichi. Mimi mchango wangu hautokuwa mrefu sana, namuomba Mhe. Waziri yale nitakayoyachangia basi ayape uzito na ayazingatie.

Mhe. Spika, nikija katika kitabu hiki nianze katika ukurasa wa 20 Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali Malipo ya Wastaafu. Sote tunajua kwamba malipo ya wasataafu sio makubwa sana lakini pia wasaafu wengi hapa kwetu Zanzibar wanaishi mashamba na wale ambao wanaishi mijini wangi wao wanaishi mbali na Wizara yetu ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Kutokana na hivyo wastaafu wengi wanatumia fedha nyingi katika kufatilia mafao yao wizarani. Lakini pia hata wanapopata mapato yale fedha zile basi ukiangalia nusu ya mapato yale utakuta yamekwenda katika matumizi ya kufatilia fedha zila katika Wizara ya Fedha.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa namuomba Mhe. Waziri kwamba kama itawezekana basi wastaafu hawa tuweze kuwalipa kila baada ya miezi 6 badala ya kuwa na mpango huu tulionao sasa hivi wa kuwalipa mezi hadi mwezi. Hii itawapunguzia wastaafu hawa usumbufu na itawadundulia kile kiasi cha fedha. Wanapopata pesa ya miezi 6 itaweza kuwasaidia katika matumizi yao. Lakini pia itawapunguzia ile gharama ambayo wanatumia katika kufatilia fedha zile.

Mhe. Spika, nikiendelea nije katika mfuko wa barabara ukurasa wa 28. Nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa kumpongeza Mhe. Waziri kwa namna ya juhudi anazozifanya katika mfuko huu wa barabara. Ukweli usiopingika kwamba katika idara yetu hii ya mfuko wa barabara ni Idara ambayo inavianzio vya uhakika wa mapato. Kwa maana hiyo hata mipango yao huwa ya uhakika.

Mhe. Spika, kutokana na juhudi ya taasisi hii basi inaonekana kwa muda mfupi ujao barabara nyingi zetu za hapa nchi kwetu zitakuwa zimemalizika na nyengine zitakuwa zimepungua kwa kiasi kikubwa sana. Kuna barabara nyingi ambazo zilikuwa ni kero sana hapa, lakini sasa hivi tunamshukuru Mhe. Waziri ukiangalia ile barabara ya Mombosa ya kupitia soko la mbogamboga hadi Mbuyu Mnene tunamshukuru Mhe. Waziri imeanza kufanyia matengenezo.

Pia nimpongeze Mhe. Waziri katika hii barabara yetu ambayo ya Mchina hadi nyumba mbili pia tunaona kwamba sasa hivi imeanza kufanyiwa matengenezo. Hata hivyo kuna barabara nyingi ambazo zipo katika maeneo mengi bado ni mbovu zipo katika hali mbaya. Lakini hali mbaya huja wakati wa kipindi cha Masika wakati wa mvua. Sote tunafahamu kwamba wananchi wetu wengi wao wanavipando kama Honda, gari na baskeli, inapofika wakati wa mvua barabara zile huwa hazipitiki kwa tope. Namuomba Mhe. Waziri ajitahidi sana katika kuhakikisha kwamba barabara zetu hizi tunazifanyia matengenezo lakini pia tunawaondolea wananchi wetu usumbufu.

Mhe. Spika, nikija katika idara hii hii nije katika idara ya jenzi wa idara hii. Nimpongeze sana Mhe. Waziri, lakini namuomba anipe ufafanuzi katika sehemu hii ya suala zima la gharama ya ujenzi. Inaonekana kwamba katika mikataba inavyoonesha kwa gharama ya ujenzi inaonekana kuwa itatumia kama milioni 500 na kidogo. Lakini mpaka sasa hivi tulipo zimeshatumika milioni 697. Sasa namuomba Mhe. Waziri kwa sababu tofauti hii si kidogo ni tofauti kubwa sana. Ningependa kujua na wananchi wangependa kujua imesababishwa na nini hata tofauti hii ikawepo na sio ndogo.

Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anieleze ongezeko hili limetokana na nini. Lakini nikiendelea Mhe. Waziri na mchango wangu nije katika Idara ya Uratibu Shughuli za Mapinduzi ya Zanzibar Dar-es-Salaam katika ukurasa wa 42. Idara hii ina majukumu makubwa sana ambayo ya kushughulikia mambo yote yanayohusu Zanzibar kwa Muungano.

Pia taasisi na mashirika ya nje. Lakini cha kusikitisha sana Idara hii kwa kweli hailingani na shughuli ambazo zinazofanywa pale. Wafanyakazi hawana pahala pa kufanyia kazi, nafasi hazitoshi, wanabanana hata ule ufanisi na utendaji wa kazi kwa hali ile haupatikani. Pia ukiangalia hali halisi ya jengo lile kwa kweli utafikiria ni nyumba ya kuishi tu na sio taasisi ya serikali.

Lakini jengine kutokana na majukumu waliyopewa ofisi ile ni lazima tuwe na wafanyakazi ambao wanamudu na wanatekeleza majukumu yanayohusiana na wizara ile. Inavyoonekana sasa Mhe. Waziri taasisi ile wengi wa wafanyakazi wanamekwenda pale kwa sababu tu waume zao wamepata *transfer* kule Dar-

es-Salaam na sio hasa hali halisi ya kuwa wamekwenda pale kwa sababu ya kutekeleza kazi ambazo wametumwa pale. Kwa hivyo, naomba Mheshimiwa Waziri tuwapeleke wafanyakazi ambao wanafani ya diplomasia ya utawala ili kuweza kuzifanya shughuli zile kwa manufaa ya taifa letu.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba waheshimiwa wengi wamechangia mambo mengi na mimi nikasema nitie barka katika katika kitabu hichi cha Mhe. Waziri wa Fedha, lakini namuomba sana yale niliyoyachangia anieleze nifahamu, nimuelewe ili niweze kumpitishia bajeti yake hii. Baada ya hayo Mhe. Spika, naomba kuishia hapo, suingi mkono mpaka nitakaporidhika na majibu yake.

Mhe: Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, kwanza na mimi namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia asubuhi hii ya leo kupata nafasi ya kuchangia kitabu kizuri cha Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Pili nakushukuru wewe kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia angalau machache. Hichi kitabu kimeandikwa kiutaalamu mkubwa sana. Kwa sababu na mimi si mtu wa mahesabu kama alivyosema Mhe. Subeti , lakini na mimi nimeona nitoe Baraka zangu katika bajeti hii.

Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri wa Fedha atueleze angalau tupate matumaini na wananchi wetu juu ya fedha za uuzaji wa Meli ya MV. Mapinduzi. Tuna taarifa kwamba meli hii imeuzwa, kutokana na usumbufu mkubwa uliopo hapa Zanzibar, Pemba na Unguja katika usafiri wa bahari wananchi wengi walikuwa wana matumaini makubwa waliposikia meli yao imeuzwa kwamba itanunuliwa meli nyengine iwe ni badala ya meli hii ya Mapinduzi ambayo ilikuwa ikiwakomboa wasafiri wa fisiwa viwili hivi. Namuomba Mhe. Waziri awaeleze wananchi kwa kina fedha hizi ziko wapi, zimefanywa nini na zina malengo gani?

Mhe. Spika, baada ya kuondoka hapo niingie kidogo katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*). Kwa kweli mimi naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa makusudi kuanzisha mfuko huu. Mfuko huu uliwapatisha mashaka makubwa wafanyakazi kwa sababu walikuwa hawaamini kwamba kukatwa kwa fedha zile zitawasaidia baadaye. Hatua kubwa ya serikali iliyochukua baada ya kukatwa pesa zile wafanyakazi kila wanapofika kustaafu wanapewa mafao yale. Hili ni jambo la kushukuru sana na la kupongeza. Lakini Mpango wa serikali kuwashawishi wafanyakazi kuupenda mfuko huu, serikali ilitumia mbinu mbali mbali za kuwashawishi wafanyakazi ikiwa ni pamoja kuwaelezea kwamba mfuko huu utawasaidia wafanyakazi wakiwemo

kazini kwa njia za mikopo pamoja na kuwasaidia huduma mbali mbali. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri awambie wafanyakazi ni lini atawakopesha pesa hizi angalau wajikimu wakiwemo makazini.

Mfanyakazi wa Zanzibar anapofikia umri wa miaka 60 kwa kweli huyo anaendea gongo. Shilingi zile anazopwa kwa ajili ya kustaafu hawezi tena kuzitumia hata kwa chakula anakuwa taabani. Jamani umri wa Wazanzibari kwa wingi wa hali basi ni miaka 63 kama itafika. Hiyo ndio miaka hata kiongozi wetu wa Kiislamu Mtume Muhammad (*SAW*). Kwa hivyo na sisi asilimia kubwa ndio tunaishi katika miaka hiyo hiyo. Unakuja kumpa mtu mafao miaka 60 zitamsaidia nini.

Watu wetu hivi sasa wanaishi katika mazingira magumu, hawana pa kukaa, kula tabu, hawana vipando vya kwendea kazini. Kwa nini tusiwakopeshe kwa masharti nafuu. Jambo ambalo litawakomboa. Jamani ili tuwe na wafanyakazi bora basi tuwatafutie mbinu bora. Hizi pesa ni haki yao. Hebu wambie wafanyakazi mfuko huu kabla ya kustaafu utawasaidia nini?

Mhe. Spika, jengine nakwenda *PBZ* kidogo mimi nachukua mambo ya jumla jumla. *PBZ* kwa kweli ni benki yetu ambayo tunaipongeza sana kwa juhudi kubwa ambayo wameichukua baada ya kutetereka tetereka katika kipindi kilichopita. Hii benki ilifika wakati ikawa inatisha kiasi fulani, lakini kwa sababu walijipanga upya sasa benki inafanya kazi viziru. *Alhamdulillah.*

Lakini sasa kuna wito wa wafanyakazi wote wa serikali kupokea fedha zao Benki, hii sio nia mbaya. Lakini kutokana na uwezo wa benki yetu hivi sasa kuwakusanya wafanyakazi wote kupokea fedha pale ni usumbufu wa hali ya juu kabisa. Kwa hivyo Mhe. Waziri labda hapa ningelimuuliza pia kwamba amejipanga vipi ili wafanyakazi hawa kuwaepusha na usumbufu. Kwa sababu *ATM* tulizonazo ni chache, vituo vya Benki vilivyopo na wafanyakazi wetu wanaofanya kazi wapo katika maeneo ya mbali ni wengi. Vipi utawaokoa wafanyakazi hawa.

Kunamfanyakazi siku nyengine yupo Tumbatu lakini benki ipo Darajani, hebu muhesabie mfanyakazi huyu ambaye atapokea mshahara, siku nyengine mshahara wake ni mdogo tu, kima cha chini cha mshahara, atoke Tumbatu mpaka Darajani, leo aje mara *ATM* haifanyi kazi au pana msururu wa wafanyakazi arudi nyumbani, kesho aje pana msururu wa wafanyakazi. Inawezekana mshahara unaweza ukatoka leo kesho, keshokutwa ni sikukuu hakuna ofisi. Jamani huyu itakuwa tumeshamtia kitanzi. Kwa hivyo Mhe. Waziri nakuomba hili ungeliangalia vizuri ili uwasaidie wafanyakazi wa nchi hii kuwaepusha na usumbufu mkubwa wa kukimbilia katika benki kwa

kupokea mishahara yao. Kama hatujakuwa tayari jamani kwa baadhi ya mambo tusiyafanye. Kwa sababu hasara yake ni kubwa kuliko faida ambayo kuwa tumeikusudia.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo niende katika Idara ya Uhakikimali. Hapa mimi nina masikitiko makubwa na nakuomba Mhe. Waziri hapa unisikilize kwa makini zaidi kuliko niliyoyasema mwanzo. Kwa sababu masikitiko yangu kwa kweli ni haya yafuatayo.

Idara ya Uhakikimali inakodisha maeneo ya serikali ya nchi hii kwa wawekezaji wa kwa miaka 99. Hili kwa kweli mimi nalihisi ni jambo zito kabisa, jamani itakuwa tunakodisha tunauza. Wazanzibari tunazaliana siku hadi siku, keshokutwa watoto wetu wanakuja kuwakutia wawekezaji wameyahodhi maeneo siye hatupo tena. Ina maana kwamba watu hawa wau watoto wetu hawa tutawaingiza katika matatizo makubwa sana. Maeneo ambayo yametakuwa yamedhibitiwa na wawekezaji, watoto wetu watakuwa hawana hata ruhusa ya kupita siku nyengine.

Jamani nchi tukifanya masihara hii wawekezaji hawa waifanya yao kuliko sisi wenyewe. Nasema kwamba Mheshimiwa Zanzibar ni ya Wazanzibari tuwekeni utaratibu ambao utatutoashaka. Sisi tunachagua viongozi kila baada ya miaka mitano kwa sababu gani? Kiongozi huyu baada ya miaka mitano tunamuona anasuasua, tunamuondosha tunamuweka mwengine. Wawekezaji tuwapeni mikataba ya miaka mitano au kumi. Tutakapomuona anakwenda ndivyo sivyo tunamuondoa na majengo yale yanabakia kwetu. Lakini tunamkodisha mtu miaka 99 tunamkataba gani wa kuweza kumuondoa ngani ya miaka mitano, sita au saba.

Mhe. Spika, hili nahisi tuliangalieni upya. Zanzibar ni yetu tunayo haki kubwa ya kuilinda katika kila hali ili Wazanzibari wajivunie maeneo yao. Kuyakodisha maeneo miaka 99, miaka 33, nahisi kwamba hapa ni kuwaonea Wazanzibari.

Mheshimiwa niende kidogo katika eneo cha Changuu pale kuna kisiwa cha Changuu. Kisiwa kile watu wa Shirika la Utalii lilikuwa linakusanya mapato karibu dola 8,000 kwa mwezi. Lakini la kushangaza ni kwamba kisiwa hiki kimekodishwa kwa wawekezaji, tunakusanya dola 3,500. Tulipokuwa tukikusanya sisi wenyewe ni 8,000 jamani hizo ni ndogo, 3500 ndio kubwa.

Kwa hivyo Mhe. Waziri tunakuomba kwa heshima na taadhima uwe makini sana katika kuitunza Zanzibar, katika kuwatunza Wazanzibari, ndani ya ardhi yao ya Zanzibar. Vyenginevyo watoto wetu wanaokuja keshokutwa watakuja

kutulaumu na kusema jamani wazee wetu walikuwa wakifanya nini. Kisiwa chetu kuwatia wageni mpaka hivi leo maeneo mengi wameyahodhi. Jamani miaka 99 ni mengi, naamini sote tuliyokuwemo humu huyo mkongwe wetu hafiki miaka 99. Leo unakikodisha kisiwa kwa miaka 99.

Namuomba Mheshimiwa anijuilishe ni maeneo mangapi aliyoyakodisha miaka ya 99 na ni mangapi aliyokodisha miaka 33. Baada ya kunieleza hivyo nikaridhika nayo nitaunga mkono hoja.

Mimi kama nilivyosema mapema michango yangu itakuwa ni ya jumla jumla na shukuru sana kupata fursa hii ya kuchangia na mimi nitaunga mkono hoja baada ya maelezo ya Waziri. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe: Spika: Waheshimiwa Wajumbe nimeombwa niwatangazie waheshimiwa wawakilishi wa upande wa Chama cha Mapinduzi, kwamba leo mnamo saa 8:30 watakutana hapa katika ukumbi wa juu. Kwa hivyo tunakwenda kupumzika lakini tukikumbuka kwamba muda huo wajumbe wa Chama cha Mapinduzi watakutana huko.
Baada ya hapo sasa naakhirisha kikao hichi hadi saa 11:00 jioni

(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Haji Faki Shaali (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Spika, umenichukua kighafla nilikuwa sijajiandaa vizuri lakini hata hivyo nitaendelea *inshaallah*. Mhe. Spika, kwanza nikushukuru na mimi kunipatia nafasi hii fupi kuchangia machache sana katika hotuba hii ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Spika, kwanza mimi nataka nianze kwa kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa uwezo wake mkubwa alionao katika kuiongoza wizara hii, pia nimsifu kwamba ana bahati kuwa anaongoza wizara ambayo tayari amekuta watu wazoefu, wenye elimu ya kutosha kwa hiyo hata ile kazi yake ya kuongoza wizara nasema kwa upande mwengine imekuwa nyepesi.

Ni tofauti kama labda angekuwa waziri ni mpya, Katibu Mkuu wake mpya, Wakurugenzi ni wapya kidogo ingekuwa ni mtihani, lakini amerithi ambao wana uzoefu wa kutosha, wana elimu ya kutosha na wana ujuzi wa kutosha. Kwa hivyo, hili limemsaidia katika kutekeleza majukumu mazito ya wizara hii.

Mhe. Spika, sote tunajua kwamba wizara hii ina majukumu mazito sana, maana yake fedha ndio fitna na baadhi ya wazazi wengine wanasema bora wafe wakiwa hawakuacha fedha katika familia zao, kwa sababu wanasema ukiacha fedha unaacha ugomvi. Kwa maana hiyo fedha tunazihitaji sana katika maendeleo lakini, fedha zina fitina kubwa. Kwa hivyo, namshukuru, nampongeza na vile vile nampa pole kwa sababu mara nyingi duniani mawaziri ambao wanakuwa na mzigo mkubwa ni Mawaziri wa Fedha na Mawaziri wa Mambo ya Ndani. Mhe. Spika, wizara mbili hizi zinakuwa zina mambo kweli kweli, lakini *inshaallah* Mwenyezi Mungu atamsaidia.

Mhe. Spika, baada ya hayo nasema nataka nimpongeze Mhe. Waziri na timu yake kwa jinsi walivyojidhatiti katika kuyapitia mashirika ya umma katika nchi yetu. Mhe. Spika, kwa kweli tunayo mashirika mengi ya umma hapa Zanzibar mengine tayari yameshakufa na yameshazikwa, mengine yameshakufa lakini hayajazikwa, mengine yako mahututi na mengine yana ugonjwa wa kawaida. Kama walivyotaja katika hotua yao ni mashirika machache sana ikiwemo PBZ ambalo linaonekana lina uhai wa kweli kweli, lakini mengi ni magonjwa magonjwa. Kwa hivyo, mimi nampongeza sana Mhe. Waziri na timu yake kwa msimamo wao huu thabiti wa kufanya zoezi hili la kuyapitia mashirika ya umma kwa sababu naamini mimi baada ya mapitio yao tutaweza kuupunguzia mzigo mkubwa serikali ambayo tunaibeba.

Mhe. Spika, sasa hivi kwa kweli serikali inabeba mzigo mkubwa sana kutoa ruzuku kwa mashirika ya umma ambayo hayana tija. Kwa hivyo, imani yangu baada ya zoezi hili wataweza kuyagundua mashirika ambayo haya hayawezi tena kuendelea kuwepo na kupeleka mapendekezo serikalini ili kufanya maamuzi yanayofaa. Nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko yeye bahati nzuri katika hotuba yake tayari alikwishazungumza maandalizi ya kutaka kulifunga shirika la magari kwa sababu tija yake ni ndogo.
Nadhani hii ilikuwa ni bashrafu lakini baada ya zoezi la Mhe. Waziri nadhani ataweza kugundua mashirika gani hasa yaendelea na mashirika gani tuyafunge ili kunusuru hizi ruzuku nyingi tunazopeleka katika mashirika ambayo hayana tija na badala yake fedha hizi kuzielekeza katika maeneo muhimu kwa maendeleo ya uchumi na ustawi wa jamii wa nchi yetu. Mhe. Spika, jambo hilo ilikuwa lazima nilipongeze kwa sababu na mimi limo ndani ya nafsi yangu kwa hivyo nilipoliona limo katika hii hotuba ya bajeti kwa kweli nimefurahi sana na watu wa wizara hii.

Mhe. Spika, jengine nataka nimpongeze tena Mhe. Waziri na watu wake kwa kuthamini kilio chetu Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu hasa

wanaotoka Wilaya ya Wete na Wilaya ya Mkoani ambao tulikuwa tuna kilio cha muda mrefu cha kukosa huduma za benki katika Wilaya zetu. Kwa hivyo, katika hotuba yao hii ya bajeti ibara ya 85 kifungu kidogo cha (b) wameeleza dhamira yao hii kurejesha huduma za benki katika Mji wa Wete na Mji wa Mkoania na Mkoa wa Kaskazini Unguja. Wanasema ni huduma ndogo ndogo, mimi imani yangu kwamba hazitakuwa huduma ndogo ndogo, imani yangu kwamba madhali wananchi watakuwa na uwezo wa kuweka pesa zao, wananchi wataweza kwenda kuchukua fedha watakapozihitaji, pengine kupata huduma za mikopo pale pale. Mimi naona hizo hazitakuwa huduma ndogo tena, itakuwa ni huduma za kawaida.

Mhe. Spika, siku hizi tushukuru Mungu kwamba kuendesha huduma za benki ni rahisi, siku hizi mtu mmoja tu kwenye kaunta na kompyuta yake anakumalizia kila kitu bila ya kuwa na urasimu kama uliokuwepo zamani. Mhe. Spika, zamani kufungua tawi la benki ilikuwa ni hasara kwa sababu ilikuwa mpaka wapite watu watatu wanne hivi kuidhinisha wewe upate pesa, lakini siku hizi ukifika kwenye *teller* dakika moja unapata pesa zako. Kwa hivyo, ilivyokuwa siku hizi kutokana na teknolojia hii ya kompyuta na mambo haya ya *internet* imekuwa rahisi kutoa huduma za kibenki. Mimi nadhani wataweza kuendesha vituo hivi bila ya hasara na wananchi watafaidika na kile kilio chetu cha muda mrefu kwa kukosa huduma za benki itakuwa kimeondoka. Kwa hivyo, hilo Mhe. Spika, vile vile naomba niwapongeze sana.

Mhe. Spika, jengine ni ushauri katika mfuko wa barabara. Mhe. Spika, jana nilikuwa nikizungumza na Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano ilikuwa tunazungumza mimi na yeye watu wawili tu lakini mambo ya maendeleo, maana mukishakuwa na majukumu kama haya hamuna nafasi ya kuzungumza mambo ya alifu ulela ulela itakuwa munazungumza mambo ya maendeleo. Mhe. Spika, katika kuzungumza mambo ya maendeleo na Mhe. Hamadi nilimkumbusha nikamwambia mheshimiwa unajua kwamba tulipokuwa na ziara na Mhe. Rais kukagua maendeleo tulikwenda Kangani kukagua barabara inayojengwa na ulimuahidi kwamba barabara hii baadae serikali itaiunganisha mpaka Mkanyageni kutokana na mfuko wa barabara.

Mhe. Spika, kwa hiyo sasa nataka ku-*officiate* yale mazungumzo yangu na Mhe. Waziri wa Miundombinu kwa sababu hili suala sio lake peke yake. Naomba sana niwaombe watu wa mfuko wa barabara kwamba watakapopanga na Wizara ya Miundombinu vipaumbele vyao basi hii barabara ya Kangani-Mkanyageni waipe kipaumbele kwa sababu barabara hii ilikwishaombewa fedha mara mbili, fedha za usanifu. Lakini bahati mbaya mara zote mbili hazikutiwa na mara hii watu wa Mawasiliano wameitoa kabisa, sio wameitoa kwa sababu ile dhamira ya kujenga barabara haipo, dhamira ipo kwa sababu

Mhe. Waziri tayari ameshaji-*commite* kwa Mhe. Rais kwamba ile barabara wataijenga. Kwa hivyo, ushauri wangu kwamba Mfuko wa Barabara kwa barabara za Pemba basi hii waipe kipaumbele namba moja na nyengine zitakazofuata zifuate namba mbili, tatu na nne, lakini hii ningeomba waipe kipaumbele namba moja kwa vile Mhe. Waziri wa Miundombinu ameshaweka ahadi mbele ya Mhe. Rais wakati wa kutembelea barabara ya Kangani.

Mhe. Spika, jengine ni ushauri wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Mhe. Spika, kwa kweli mimi naupongeza sana mfuko huu kwani ni ukombozi kwa Zanzibar kwani umesaidia mambo mengi. Mhe. Spika, kwa sababu hata hilo tawi la Benki ya Kiislamu sio lao lakini limo katika jengo lao. Kwa hivyo, nadhani ile kuwepo kwa lile jengo imekuwa ni kishawishi kwa watu wa Benki ya Watu wa Zanzibar kuona hapa pahala tukaweke hii benki yetu. Pengine lisingekuwepo lile jengo hata wao ile hamu ya kufungu tawi isingekuwepo, maana pengine wangekuwa hawana pahala pazuri penye heshima pakuweka tawi lao. Kwa hivyo, mimi nasema ni kichecheo kizuri cha maendeleo Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi ilikuwa nafikiria katika uwekezaji wao, nimeona wanasema wamepeleka watu wao China kwenda kujifunza ujenzi wa nyumba za mkopo nafuu, hilo ni wazo zuri sana imani yangu kwamba baadae watakaporudi watu hao watajenga nyumba hizi Unguja na Pemba ili wananchi waweze kufaidika. Mhe. Spika, la pili ninalowashauri waangalie uwezekano wa kujenga *hostel* hapa katika Baraza la Wawakilishi, kwa sababu Waheshimiwa wengi Wawakilishi wanalazimika kukodi nyumba mijini.

Nafikiri kama wangejenga hapa *hostel* karibu na Baraza la Wawakilishi nadhani ingekuwa ni mradi mzuri kwa wao, lakini vile vile ungepunguza tatizo katika nchi juu ya wawakilishi kuhangaika sana kwenda masafa marefu. Kwa hivyo, naomba hili walichukue walifikirie na kama wakiona lina tija basi naomba walifanyie kazi ili watusaidie Waheshimiwa Wawakilishi lakini na wao vile vile itakuwa ni uwekezaji wao.

Mhe. Spika, mimi nadhani lengo langu kubwa ilikuwa kwa leo niseme hayo na kumpongeza Mhe. Waziri na timu yake yote na kwa kumalizia niseme kwamba naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, nakushukuru sana na mimi kunipa nafasi ya kuzungumza machache katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Mhe. Spika, kwanza naomba nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa namna ambavyo ameandaa kitabu chake lakini pia kwa alivyoiwasilisha, naelewa kwamba wizara ambayo

anaisimamia ni moja katika wizara muhimu katika nchi yetu, pia ni wizara ngumu kwa ilivyo. Maana ni wizara ambayo inashughulikia mambo ya uchumi na mipango ya maendeleo katika nchi, lakini zaidi masuala yanayohusu fedha ni wizara moja ngumu sana. Mhe. Spika, lakini kwa namna ambavyo amejipanga kuitumikia mimi nampongeza sana Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, mbali ya kumpongeza Mhe. Waziri mimi naomba niwapongeze sana watendaji wake. Mhe. Spika, sisi wengine tunakumbuka sana hali ilivyokuwa miaka ya nyuma, lakini watendaji hawa wameweza kufanya mambo makubwa ambayo kwa kweli wanastahiki kupongezwa sana. Sote tunakumbuka hali ya mishahara ilivyokuwa siku za nyuma katika nchi yetu ilikuwa tunagonga mpaka tarehe 50, lakini watendaji hawa wamefanya kazi nzuri kwamba sasa mishahara inapatikana kwa wakati.

Mhe. Spika, kubwa na la muhimu ni malipo ya wastaafu nalo wameliweza sasa wasi wasi wa mtu kustaafu akasubiri sana bila ya kupata haki yake *alhamdulillah* suala hili limeondoka. Lakini jambo jengine ni namna ambavyo wameshirikiana kwa pamoja na Bodi yetu ya Mapato katika ukusanyaji wa fedha, wamefanya kazi nzuri *ZRB* imekuwa ni taasisi muhimu sana katika nchi yetu inafanya kazi vizuri, watendaji wake na kamishna wake kwa kweli wamekuwa wakisaidiana na uongozi wa wizara hii sasa hali ya upatikanaji wa mapato kwa kweli umeongezeka vizuri sana.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka huu ndani ya awamu hii ya saba mwanzoni mapato kwa kweli yali-*pick* sana kila mmoja akasema kwa kweli *ZRB* imefanya kazi nzuri. Kwa hivyo, mimi naomba niwapongeze sana kwa hili.

Mhe. Spika, mimi baada ya kuundwa serikali hii ya awamu ya saba nilikuwa na wasi wasi na namna Mhe. Waziri na watendaji wake watakavyoweza, kuna Wizara kama ya Mifugo na Uvuvi ilikuwa haina bajeti nilitegemea labda tutalazimika kuletewa *supplementary budget* katika Baraza lako tukufu. Lakini namshukuru Mhe. Waziri na mtaji wake wameweza kufanya utaalamu wao pamoja na hali yote iliyokuwa lakini wizara hata wizara yangu haikukwama ambayo haikuwa na bajeti.

Kwa kweli namshukuru na wakati wowote ambapo tuliweza kuyumba basi wizara yake Mhe. Waziri na Katibu Mkuu na Mhasibu Mkuu wa Serikali walikuwa tayari kuipa msaada wizara yangu ili isiweze kukwama katika shughuli zake. Mhe. Spika, hili ni jambo ambalo lilihitaji maarifa makubwa na ujuzi na uzoefu katika kutekeleza mambo vyenginevyo tungelikwama, sio mchezo kwamba wizara iliyokuwa haikuwa na bajeti kwa karibu miezi minane,

lakini bado ikaweza kutekeleza shughuli zake bila ya matatizo sana. Mimi nashukuru sana kwa hilo.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo nataka nilisifu ni Benki ya Watu wa Zanzibar kwa muda mrefu tumekuwa na kilio cha kwamba wa Zanzibar walioko Dar es Salaam wanahitaji huduma ya benki yetu kwa sababu *PBZ* moja katika sifa yao ni uaminifu. Kwa hivyo, wafanyabiashara wetu walioko pale Dar es Salaam kwa kweli walikuwa na matatizo mengi, lakini *PBZ* imeweza kufungua tawi pale na mimi mwenyewe nimeshawahi kulitembelea kweli vijana wamejipanga vizuri, pana watendaji na inaonekana inafanya kazi vizuri.

Mhe. Spika, kwa sababu kwa kadiri ya shughuli nilivyoziona pale ni kwamba pana wateja wengi sana, mimi naomba niwapongeze sana na ikiwezekana basi wasiishie Dar es Salaam tuangalie Mikoa mengine ambayo imechangamka kibiashara basi wajaribu kufungua matawi ya benki, inaweza kusaidia sana.

Mhe. Spika, baada ya hilo naomba nizungumzie mambo mawili mengine. La kwanza naomba nimkumbushe Mhe. Waziri kwamba wizara yangu imepata kusaidiwa nafasi za masomo nje ya nchi baada ya bajeti. Mhe. Spika, baada ya kutayarisha bajeti yangu kuna nchi zimetusaidia nafasi za masomo kwanza China imetupa nafasi 30 mwezi huu, lakini tunatarajia pia mwezi wa April watatupa nyengine 30. Kwa hivyo, bahati mbaya mimi nilipopata hizo nafasi ni kwamba matayarisho ya bajeti yangu yalikuwa yameshapita, lakini naomba nimkumbushe Mhe. Waziri kwamba tumekubaliana yakitokea mambo kama haya basi wizara yake itakuwa tayari kusaidia jambo hili ili kuona kwamba wanafunzi wale wanawezeshwa kupata safari za nje kwenda katika nchi ambazo wanakwenda.

Kwa hivyo, naomba hili katika matumizi yake ya safari za nje ajue kwamba hawa 30 ambao wataondoka mwezi wa Augus kuna chochote lazima waandaliwe, masuala ya visa na mambo mengine, na chochote mfukoni na wale 30 wa mwezi wa April tukijaaliwa pia wanahitaji kuhudumiwa na wizara yake.

Mhe. Spika, jambo jengine ni Mfuko wa Baraza, mfuko huu umekuwa ukifanya kazi nzuri, mimi nauopongeza sana na katika maeneo mbali mbali wamekuwa wakijitahidi kusaidia. Kwa hivyo, Waziri wa Asiyekuwa na Wizara Maalum Mhe. Haji Faki Shaali alizungumzia barabara ile ya Shidi. Mhe. Spika, ni kweli na mimi nilikuwepo na mimi naomba nilisisitize hilo kuwa barabara ya kwanza, lakini barabara ya pili naomba kama alivyokwishazungumza na watendaji wake barabara iliyopo Kizimbani katika eneo la Kiwanda cha Mbao. Hii kama itakuwa ya pili au ya tatu au ya nne lakini naomba nayo iangaliwe

namna ya kushughulikiwa. Mhe. Spika, mimi kwa kweli nilikuwa nataka kutia baraka katika bajeti hii na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Gando naunga mkono hoja ya bajeti hii.

Mhe. Spika: Mhe. Mwanasheria Mkuu nikuombe radhi kidogo ameniomba mjumbe mmoja nimwite yeye halafu baadae nikuombe uchangie na wewe.

Mhe. Ali Mzee Ali: Bismilahi rahmani rahim Mhe. Spika, naomba radhi sana kukiingilia kati kati wakati umeshafanya maamuzi, lakini kwa kuwa leo tunahitimisha na nilichangia Wizara ya Elimu lakini sijaona raha kwa sababu wewe hujakuwepo kwenye kiti. Kwa hivyo, sababu iliyonifanya nichangie sasa hivi kwa sababu upo kwenye kiti. Mhe. Spika, naomba unistahamilie.

Mhe. Spika, kwanza sijapata nafasi ya kukupongeza nilikuwa nje kwa muda wa miezi minane. Mhe. Spika, nakupongeza kwa dhati na kwa kazi ambayo nilikuwa naisikiliza Baraza lako tukufu namna ulivyokuwa unaliendesha Baraza la mwanzo lenye mfuko wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Mhe. Spika, una kila sifa na unastahiki kuwa Spika wa kwanza kwenye Baraza hili la Umoja wa Kitaifa. (*Makofi*).

Mhe. Spika, mwaka 1990 wewe ulikuwa Mwakilishi wa Jimbo la Makunduchi, wakati huo wewe ulikuwa Mjumbe wa Tume ya Nyalali ya vyama vingi kama Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo, mwaka 1995 ukawa Spika wa kwanza kuongoza Baraza lenye mfumo wa vyama vingi, mwaka 2000, 2005, 2010 umekuwa Spika wa kwanza kuongoza Baraza la Wawakilishi lenye mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Hakuna mtu mwengine Zanzibar hii ambaye analingana na wewe labda kwa wakati wa mbele. Kwa hivyo, Mhe. Spika, hongera sana.

Mhe. Spika, wewe ni muumini umezungumza siku ile kwenye semina pale na ninayo hansard yako hapa namna gani ulivyokuwa unaumwa wakati Baraza hili namna mambo yalivyokwenda ukafika hadi ukaona labda nikioa Pemba mambo yatakuwa sawa, na mambo hayajasaidia. Mhe. Spika, haya mambo ya kuoa hata Kwame Nkuruma alikwenda kuoa Misri ili kujenga *Pan Africanism* pengine kuoa nayo inaweza kusaidia, umesemwa mimi na wewe vikaratasi vimetawanywa lakini leo Baraza lako hili tukufu ndio hii hali yake sasa hivi liko katika hali ya utulivu na amani.

Mhe. Spika, vile vile nataka nichukue nafasi hii mimi binafsi kuwashukuru Wawakilishi wote kwa miezi niliyokuwa nje namna walivyokuwa wanachangia, namna walivyokuwa wanaendesha mambo haya kwa kweli wamefungua uso wetu mimi na wewe. Mhe. Spika, redio Colon ilikuuliza

unauwa demokrasi nitafanya vipi serikali haina upinzani. Mhe. Spika, sisi tumekwenda Uingereza, mimi, Mhe. Abubakar Khamis Bakary, Mhe. Haji Omar Kheir, Mhe. Zakiya Omar Juma, Mhe. Ali Abdalla Ali na Mhe. Nassor Ahmed Mazrui Waingereza wametwambia mnauwa demokrasi itakuwaje? Nimemsikia mtu anasema mfumo huu hauko duniani, mfumo huu hauko Uingereza wala hauko Ujerumani. Huu ni mfumo wa Kificho tu lakini tukawaambia mtaona.

Mhe. Spika, juzi Mfalme wa Nigeria anamwambia Makamo wa Kwanza wa Rais, watu wao waje wasome Zanzibar namna gani tumeweza, huyo ni mtu wa Ghana. Ghana ndiyo waliotupatanisha sisi mwaka 1958 *Afro Shirazi* na Hizbu, leo Ghana wanasema waje Zanzibar. Mhe. Spika, Mabalozi mbali mbali wametupongeza sasa hivi ukenda kwenye *internet* watu wanalisifu Baraza la Wawakilishi namna wanavyozungumza, na hivi ndivyo inavyotakiwa kwenye *grade you* kwa sababu kuna upinzani, tunakosoa, tunatengeneza, tunaweka na kadhalika.

Mhe. Spika, kwa hivyo nakupongeza sana namna Baraza unavyoliendesha na nawapongeza Waheshimiwa Wajumbe wanavyochangia, wanapokosoa hivi ndivyo inavyotakiwa. Mhe. Spika, lakini mwisho wake tunafanya maamuzi ya pamoja kwa sababu sisi sote huko mbele wanaitwa *front* na huku nyuma wanaitwa *backbenchers* hakuna upinzani, tunaweza kusema kila baada ya miaka miwili tubadilishane wa huku waje huku inawezekana wala sio tabu.

Sasa Mhe. Spika, niliona niende kwenye hoja. Ndugu Omar Yussuf ni Waziri wa 14 au 15. Waziri wa Fedha wa mwanzo Serikali ya Mapinduzi ni Mhe. Hasnuu Makame, Mwenyezi Mungu amrehemu, ndio wa mwanzo, wengi wamekuwa mawaziri wa fedha lakini Mzee Abeir Karume alifika pahala akasema yeye sasa atakuwa Waziri wa Fedha mwenyewe, kaendeleza mambo yamekwenda vizuri, baada ya kuuwawa muda mrefu mwaka 2000 Rais Karume akasema na mimi nitakuwa Waziri wa Fedha nitakuwa na WAziri wa Nchi Fedha alimchagua ndugu Suleiman Othman Nyanag baadae Ndugu Mwinyihaji Makame na Dkt Shein na yeye kafanya hivyo hivyo.

Kwa hivyo, Ndugu Omar Yussuf ni Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Ndugu Omar ni mzoefu amekuwa Mtakwimu Mkuu, amekuwa Katibu Mkuu Mipango waziri wake Mhe. Ali Juma Shamuhuna, amekuwa Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Kiongozi, ameingia Siasa ameshinda jimbo, amekwenda Bara amekuwa Naibu Waziri wa Ulinzi, amekuwa Naibu Waziri wa Fedha, karudi nyumbani kateuliwa Jimbo letu hili la Ukulu. Mimi nampongeza. Lakini nilisema Mhe. Spika, siku ile hawa *front* hawa ni wapya, wamebeba majukumu ya Awamu ya Sita wanayoyaweza watayajibu

wasioyaweza tutakwendanayo mbele, lakini huko mbele tumekwenda watakuwa na yao ndio haya sasa hivi. Sasa mimi Mhe. Spika, kwanza nataka kuzungumza kuhusu *Peoples Bank.* Ni benki yetu ambayo ilifika pahala hali yake ikawa mbaya sana, lakini ni Ndugu Omar Yussuf akiwa Katibu Mkuu ndiye aliyepewa kazi ya ku-*reform* hii hali ya *Peoples Bank.* Leo yeye na wenzake ndio kazi waliyoifanya hiyo na *Peoples Bank* sasa ni benki ya kuaminika. Wamesema sijui Mhe. Ali Mzee barua, sijui nini, aah, lakini tunakwenda kukopa, tutakwenda ni benki ya kuaminika, ni benki ambayo inaaminika katika Afrika sasa. Kwa hivyo, tuendelee kuitumia na tuisaidie.

Jengine Mhe. Spika, Usimamizi wa Mitaji ya Umma. Watu wamesema sana hapa, mitaji ya umma sheria yake tumepitisha hapa, mimi nazungumza Mhe. Waziri aliwahi kufanya kikao mimi ni mwenyekiti Mhe. Spika, wa Shirika la Meli.

Mhe. Spaika, mwaka 2003 tuliunda Tume hapa wakati Mhe. Abubakar anamtoa jasho Mhe. Adam Mwakanjuki mpaka Mwakanjuki akaapa, *Wallahi Billahi* akashika msahafu kasahau kabisa kama ni mkiristo. Akasema hapana tusiunde tume, Kamati ya Mawasiliano nendeni Mombasa mkachunguze Shirika la Meli. Mhe. Abubakar yule pale, tulikwenda na Mhe. Said Ali Mbarouk, Mhe. Machano Othman Said, Mhe. Hafsa Said, kamati teule ya Baraza tulikwenda kule.

Mwaka 2008 Mhe. Machano ndiye Waziri wa Mawasiliano anayeshughulika na Shirika la Meli aliyekwenda mwaka 2003 kuchunguza. Sijakaa sawa nasikia Ali Mzee mwenyekiti, aah! Watu wakaandika itakuwaje? Lakini tumefika pale tumekuta matatizo yapo, leo kaulizwa habari za Meli ya MV. Mapinduzi. Mashirika yote Shirika la Bima, Shirika la Utalii, Shirika la Magari, *Peoples Bank*, Shirika la Meli yote haya ni mashirika ni mali ya serikali, haya sio mashirika binafsi ya uhuru ni mali ya serikali mwenyewe ni Wizara ya Fedha. Kila bajeti hapa anasema Mhe. Machano tutanunua meli, Mwakanjuki tutanunua meli, tutanunua meli vipi, wa kununua meli ni serikali. Tulipoingia pale tuliikuta M.V. Mapinduzi tangu mwaka 2003 imelala inakula tu, mimi nilipoingia nilifanya uamuzi mgumu tukasema hii meli ina nini? Nikaambiwa hii meli inataka kuuzwa lakini tatizo jina, dola milioni moja zipo tayari *survey* akachaguliwa, nikasema kwani Mhe. Machano kwa nini hatuiuzi? Akasema unajuwa tatizo jina MV. Mapinduzi itakuwaje tuuze.

Mimi Mhe. Spika, nikafanya maamuzi ya ujasiri nikenda kwa Rais mimi na Kapteni Sururu bila ya Mhe. Machano tukamchukua na yule *expert* tukenda pale tukamwambia Mzee hii meli itatia hasara inaoza, watu wanataka kuinunua, akasema atainunua nani? Nikamwambia yuko mtu tayari ripoti hii hapa,

akasema basi kama ni hivyo, lakini naona tatizo jina Mapinduzi, nikamwambia Mzee si tatizo hilo, tuuze tununue meli nyengine tuite Mapinduzi Daima akasema sawa, kama utauza Mapinduzi halafu unuue nyengine uite Mapinduzi Daima sawa, ikakubaliwa ile meli iuzwe. Mawaziri wote wale wa Awamu ya Sita tulikwenda Baraza la Mapinduzi sisi tukazungumza pale ikakubaliwa meli iuzwe, akasimama mtu wa Wizra ya Fedha akasema nani atauza, sisi tutauza, Maalum Haroun Suleiman yule sijui katoka, akasema iuzwe Meli ya Mapinduzi na Maendeleo. Baraza la Mapinduzi likakubali meli iuzwe, wakasimama watu wa fedha Mhe. Dkt,. Mwinyihaji wakasema Shirika haliwezi kuuza meli si yao na kuna sheria ya uuzaji.

Kwa hivyo, Wizara ya Fedha ndio iuze itatoa tenda. Sisi tukasema haja yetu iuzwe tu, meli ikatangazwa lakini ikawa inakwenda inauzwa, haiuzwi, mwisho wake akapatikana mtu wa kuinunua ile meli. Kuna kampuni Mhe. Spika, inaitwa **Ahorora** kwa dola 450,000 barua akaleta Waziri wa Fedha wa wakati huo Dkt. Mwinyihaji Makame akasema serikali imeuza meli, imemuuzia **Ahorora** kwa fedha hizi. Fedha hizi zitawekwa kwenye account maalum ya kuanza kununua meli. Barua ipo kila kitu kipo, tukakaa, tukenda ikawa bado yule mtu anasema kesho, keshokutwa meli inataka kuzama Mheshimiwa.

Baadae tukapata barua nyengine, Waziri wa Mawasiliano akapata mteja akampeleka Wizra ya Fedha wakazungumza na Waziri na akasema kuna bodi ikatoe idhini yake. Sisi tukasema hapana, sisi tunamjua yule wa mwanzo huyu sisi hatumjui, lakini nyinyi nyamazeni ikenda bahati mbaya naye mteja yule hakupatikana akapatikana mwengine akauziwa kwa dola 410,000/-, akalipa meli akaichukua kenda nayo nje huko meli ikazama *Innalilahi Wainnarajiun* ikaishia hapo. Sasa hiyo ndio hadithi ya M.V. Mapinduzi na fedha zake Wizara ya Fesha ndio wenye mali ndio wakununua.

M.V. Maendeleo ina miaka 30 mbovu tunalazimisha lakini waziri kasema iuzwe kwenye bajeti yake. Waziri wa Fedha ichukue meli iuze ina matatizo, mali yako ile. Lakini Mhe. Spika, Zanzibar ni kisiwa haiwezekani tusiwe na meli, haiwezekani, ikiwa meli kasema Maalim Seif inunuliwe aseme, ikiwa kasema Ali Mzee aseme, ikwa kasema nani lakini meli lazima ununuliwe, kwa sababu hiki ni kisiwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, wala si jambo jipya serikali hapa Zanzibar kuanzia mwaka elfu moja na tano (1005) serikal ina meli zake na meli ndio iliyomuokoa Jemshid, ingekuwa si meli yake tungekuwa naye sasa hivi hapa. Kwa hivyo, serikali lazima iwe na meli na serikali meli yake si biashara ni *service* baina ya Unguja na Pemba kupakia karafuu, mbata peleka wapi ni *service* muda wote huo. Shirika la Meli liundwe kwa *service*, kwa *decree* sio kwa sheria baadae ndio

sheria ya Mitaji ya Umma. Lakini Mhe. Spika, ili kuweka ushahidi kamili kuwa serikali imo kwenye meli ni kwamba hapo zamani kulikuwa na Meli ya S.S. Badra meli iliyotengenezwa Calcutta Meli ya Serikali ya Zanzibar iliundwa mwaka 1905 ilikuwepo hapa, S. S. Qupid mwaka 1912 ilikuwepo hapa, S.S. Drag Meli ya serikali nayo mwaka 1930 ilikuwepo, Alhadhara ilikuwepo baadae ikauzwa, Al-Sayyid ilikuwepo, tumeingia kwenye M.V. Mapinduzi tumezikuta sisi hizi meli za Khalifa na Salama hapa, kama wapo watu wa miaka 60 wanakumbuka meli hizo za serikali, baadae jina tukabadilisha tukaita Afrika na Jamhuri.

Baadae Serikali ya Mapinduzi ikaamua kununua Meli ya M.V. Mapinduzi mwaka 1974, mwaka 1980 tukanunua Meli ya M.V. Maendeleo, leo zote ziko hatarini. Mhe. Waziri wa Fedha aidha tupe sisi tuziuze au wewe mwenyewe, lakini wewe ndiye mwenyewe nunua meli.

Wakati wa kampeni Rais wa Zanzibar Pemba mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati iliyochaguliwa na Chama chetu cha Mapinduzi, Mjumbe wa Kamati ya Kampeni, sio nilichupia nilichaguliwa na chama chetu kwa Dkt. Ali Mohamed Shein. Aliniita nimpe taarifa za kununua meli nikampa Pemba akazungumza Micheweni kuwa tutanunua meli. Alitoa ahadi, tutaigeuza hali ya maisha Pemba Micheweni na Dkt Shein amefanya kazi kweli kweli ni muungwana.

Mhe. Spika, Dkt. Ali Mohamed Shein katika kampeni zake aliahidi, chama pia kiliahidi. Yeye alisema hivi, “CCM si chama cha wababaishaji”. Akasema tena tarehe 2/10/2010 “Nitaendesha nchi kwa mujibu wa Katiba”. Mhe. Hamza Hassan Juma alisema hapa. Akasema tena, “Niko tayari kufanya kazi na upinzani ndio njia muwafaka kuimarisha amani na umoja”. Akaesma tena, “Wana CCM waombeni kura wapinzani”. Kampeni za kisayansi, kitanda kwa kitanda. Akasema tena, “Nitaongoza kwa dira ya sayansi na teknolojia”, alisema Tumbe/Konde. Mwisho alimalizia kwa kusema, “Sitowavumilia wenye kuchezea amani”, alisema tarehe 22 Chokocho.

Mhe. Spika, tumefanya miafaka mingi tangu 1958, kwa Chief Anyauku, Baraza la Wawakilishi Mhe. Haji Mkema na Mloo akasaini, mwaka 2003 *IPC* Barazani kwako pia tukala haluwa, pilau, lakini yote ilikufa haijawezekana. Lakini Baraza lako tukufu chini ya uongozi wako ilikuja Hoja Binafsi humu ndani, nasema hayo kwa sababu wengine wapya kina Mhe. Abubakar Khamis Bakari, tuzungumze namna ya kuendesha nchi yetu.

Huko nyuma Rais Kikwete alisema anakerwa na Zanzibar watu kuwa hawasaidiani, hawapendani, zikaundwa tume zile zikenda Mhe. Juma Duni yupo alikuwa mjumbe, Ismail Jussa mjumbe na wengine hapa hawapo,

wakakubaliana hawa waunde Serikali shirikishi, tukasema hapana sisi CCM tukasema kiyama mimi nilikuwa mjumbe. Hatuwezi kuunda Serikali Shirikishi, twende kwa wananchi tukawaulize wanatakaje? *(Makofi)*

Mhe. Spika, tukabishana Mhe. Abubakar akaleta hoja yake, Baraza lako tukufu tukakubaliana twende kwa wananchi tukawaulize, aidha wananchi au Baraza kwa sababu Baraza lisipoamua wananchi wakaamue. Tukawapelekea wananchi tarehe 31, Jumapili kesho kutwa ni mwaka mmoja kamili tangu Wananchi wa Zanzibar kuchagua Mfumo wa Serikali ya Mapinduzi yenye Mfumo wa Umoja wa Kitaifa. Tuko salama na amani, tumefanya kampeni za uchaguzi tumemaliza serikali ikaundwa. Dkt. Shein ni muumini angeweza kuapa siku ile pale kwa katiba hii halafu asitekeleze, lakini ameapa anatekeleza, anaendelea kutekeleza na msikivu. Kwa hivyo, hali ya wananchi wetu ni sawa hivi sasa, tunakwenda vizuri, sasa niliona nitoe dibaji hii pamoja na haya mambo ya M.V. Mapinduzi na mambo ya Benki.

La mwisho kabisa Wizara ya Fedha kazi yake kusimamia uchumi na sasa hivi Mhe. Haji Faki Shaali alipokuwa akichangia mwaka jana alisema, irudishwe, ipangwe sijui na fedha, na ikaombwa dua arudi na karudi kawa waziri, siku hizi hata hanipitii. Lakini Mhe. Spika, Wizara ya Fedha ni uchumi, Baraza lako tukufu alisema Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi mwaka 14/01/1980 kuwa Baraza la Wawakilishi ni ngome. Narudia tena Baraza la Wawakilishi ni ngome, ngome ikikuangukia ukivunjika ukiipiga konde utaumia wewe. Nimefahamika? Hii ni ngome. Sasa ngome yako ilitoa azimio kasema mwanasheria mambo mengi yamezungumzwa lakini Baraza halijatoa maazimio. Baraza lilitoa maazimio ya uchumi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, niruhusu ninukuu kidogo. Muungano, “Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni ubia wa nchi mbili huru zilizoamua kuungana zikitegemea ushirikiano utakaoleta maendeleo zaidi kwa wananchi wa pande zote mbili”. Mpo? “Kwa mnasaba huo Muungano huu una dhima kubwa ya kuhakikisha kuwa kila upande unawezeshwa, kutekeleza dhamiri hiyo kwa wananchi wake”.

Mwaka jana kulikuwa na mjadala mkubwa ndani ya Baraza la Wawakilishi kuhusu rasilimali ya mafuta na gesi asilia uliotaka suala hilo lisiwe la Muungano na liondoshwe kutoka orodha ya mambo ya Muungano, ili kila upande wa Muungano huu ushughulikie wenyewe suala hilo kama ilivyo hivi sasa kwa mafuta na gesi asilia, dhahabu, almasi na madini mengine yote kwa Tanzania Bara. Pendekezo hilo liliungwa mkono karibuni na wananchi wote wa Zanzibar, hili pendekezo hili la Baraza la Wawakilishi liliungwa mkono na wananchi wote wa Zanzibar. Nini waliunga mkono?

Pendekezo hilo liliungwa mkono na karibu wananchi wote wa Zanzibar ililenga zaidi katika mambo muhimu matatu. La kwanza, kulinda na kuimarisha uchumi na ustawi wa jamii wa Wazanzibari, umuhimu wa kusimamia masuala ya utawala na uendeshaji wake, ulazimu wa usimamizi wa utunzaji wa mazingira katika maeneo husika ya ardhi na bahari ya Zanzibar. Kwa vile Muungano wetu umetokana na ridhaa ya wananchi wa pande mbili kupitia serikali zao lakini pia ni Muungano wenye utaratibu mzuri wa kurekebisha mambo kwa faida ya wadau.

Napenda kumpongeza Rais Kikwete kwa maelezo yake ambayo kimsingi yanakubaliana na mapendekezo ya Wananchi wa Zanzibar juu ya uwezekano wa kuliondoa suala la mafuta na gesi asilia katika orodha ya mambo ya Muungano ili Wazanzibari wenyewe waendelee kusimamia hatma ya uchumi wao kwa kutumia rasilimali zao wenyewe, ikiwemo mafuta na gesi. Bila shaka hatua hiyo italeta faraja kubwa kwa Zanziabar itayoongeza nguvu na heshima za Muungano wetu kinyume na wanavyofiiiria wale wasiojuwa maana ya Muungano. Wakati huo huo utaratibu wa kujadili kero za Muungano kupitia huko zitapitiwa pitiwa. Ndio haya maneno yalisemwa na Rais Mstaafu pale Uwanja wa Pemba. *(Makofi)*

Baraza lilimaliza suala hili, juzi limekuja tena lakini sasa tunasema huu uamuzi wa Baraza haujadiliwi wala hizi hazimo kwenye kero, suala hili sasa Mhe. Hamza Hassan anasema wao barua wameandika ndugu Waziri wa Fedha mlifuatilie suala hili Baraza hili liambiwe hakuna tena mjadala wala sitaki kutukanwa kwenye vikaratasi aah, nayasema maneno hapa mjadala hakuna umekwisha. Madhumuni yake ni kuchukua vitu vyetu hali yetu mbaya ya uchumi. *(Makofi)*

Sasa haya mambo ya *ZRB* kulipa mara mbili au tatu haya iko siku tutayazungumza. Wengine wanasema wafukuzwe mambo yanakwenda kwa utaratibu kwa sheria. Kwa hivyo, niliona Mhe. Spika, niseme hayo. Nafikiri kwa dibaji hiyo fupi mimi nasema wakati umefika tushikamane, tuendeshe nchi yetu tena vijana hao wapo, vijana wasikemewe wanafanya haki yao ya kidemokrasi.

Mhe. Spika, ninayo kaseti yako umezungumza *Radio Colon* na juzi Mhe. Ismail Jussa ametupongeza kutwambia watu wanasifu, watu wanasifu wanasikiliza. Maalim Seif Sharif anasema hili Baraza safi tena kamtaja mtu wake mmoja anasema huyo anauliza maswali ndivyo ilivyo hapana pengine. Ingekuwa tuna upinzani huku na huku lakini sasa hakuna.

Mhe. Spika, mimi nilikaa juu ya kiti chako nikafanya maamuzi, alisema Mhe. Haji Faki Shaali mchele mbovu, ghala imevunjwa, ripoti ya Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi imeandikwa usalama wa taifa nikasema hapana, thibitisha, akaema sithibitishi, nikamwambia thibitisha, siku ya pili yake ukaja mwenyewe pale ukasema nimepata barua kwa Mhe. Haji Faki anasema Mwenyekiti alikosea ikawa mzozo pale, ghasia na yeye Mhe. Spika, apelekwe maadili nikaesma hapana, niache nipelekwe mimi maadili kwa sababu mimi ndiye niliyekaa juu ya kiti kwa niaba ya Spika.

Tumekwenda kwa maadili tulikuwa na Mhe. Salmin Awadh, Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu, Mhe. Thuwaybah E. Kisasi na upande wa wapinzani kulikuwa na Mhe. Abubakari Khamis Bakary, Mhe. Haji Faki Shaali. Maadili yale barua wakaniletea niende Malindi nikasema wala siendi popote, ripoti ikatoka. CCM watano wasema Mwenyekiti hajakosea *CUF* wanasema amekosea. Leo ukipeleka maadili pahala haitokuwa hivyo patakuwa pana misimamo watatizama maadili *time* imebadilika na humu nyote mnataka kila jambo na uzuri wake ndio ubaya wake.

Sasa Mhe. Spika, niliona niseme hayo na Mhe. Waziri hayo niliokwambia nakuomba sana, unayoweza kuyatekeleza yatekeleze, unajibu mambo mengi ya mika mingi ndio kazi, lakini hili la Serikali kuwa na meli nimeeleza vizuri sana. Tunapakia majeshi, tunapakia mizigo yetu kukiwa na Sherehe za Mapinduzi Pemba katika zile boti za watu si sawa, wengine si raia wa meli zao, tunapakia majeshi wetu, serikali iwe na meli tena haraka sana kwa misingi hiyo. *(Makofi)*

Kwa hayo Mhe. Spika, mimi naona naunga mkono umoja huu haya mambo yanavyokwenda. Mimi nafikiri Mhe. Waziri atakuja kueleza haya mambo yangu ya meli na mengine tena hapo tutajua hali inavyokwenda. Mhe. Spika, Ahsante sana.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ili nichangie na mimi katika bajeti hii ya Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kazi nzito na ngumu. Kwa kweli Mhe. Spika, Wizara ya Fedha ina kazi ngumu na kwa sababu ni Wizara ya Fedha watu wote wanaitizama kwa maendeleo na kwa ufanisi wa nchi yetu hii.

Mhe. Spika, kwanza nianze na Shirika la Bima. Shirika hili ni shirika ambalo linatoa huduma muhimu sana kwa maendeleo ya uchumi na hifadhi ya jamii. Lakini Mhe. Spika, kwanza nijitambulishe kuwa ni Mjumbe wa Kamati ya *PAC* nikiwa kama Makamo Mwenyekiti wa kamati hiyo

Nimeona namna gani Shirika la Bima linamudu bima zake za mpito ambazo ni *liquilities position and working capital*. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu iliyopita ni kwamba inamudu kujiendesha.

Mhe. Spika, hali ambayo inasikitisha sasa hivi ni kwamba shirika hili kule mwanzo ambako tumesehelea tawi lake kumetokezea upotevu wa pesa karibuni milioni 12,084,900/=. Kwa hivyo, juu ya kuwa ina uwezo wa kumudu hii lakini upotevu kama huu kwa kweli tutafikia pahala ambapo shirika hilo litakwama kiuendeshaji.

Mhe. Spika, shirika hili linategemea faida au hasara kutokana na hali ya mapato halisi na gharama za malalamiko. Kwa hivyo, zikitokea hizi gharama za malalamiko ikiwa *income* ni ndogo kwa kweli kutaonesha matatizo na upotevu kama huu kusema kweli itakuwa ni mtihani kwao. Kutokana na kesi hii mpaka sasa hivi kule huyu mhusika ni kwamba mpaka sasa hivi yupo nje kwa dhamana na pesa kama hizi zimeshapotea. Kwa kweli hili ni tatizo tena kubwa.

Mimi nasema kulikuwa hakuna *internal control* kwa sababu pesa hizi walikuwa wanazipokea na halafu wanampa Mhasibu badala ya kutia mfuko huu zinatokea mfuko huu. Kwa hivyo, suala hili kwanza kwa upande wa Bima mjipange vizuri sana katika *internal control* ili ufanisi na yale matatizo ya kuibiwa pesa yaweze kuondoka.

Mhe. Spika, vile vile nirudie tena kwa Wizara ya Fedha niseme hii ni wizara yangu na leo nikisema kwamba ni Mwakilishi lakini Mwakilishi ni koti ambalo nalivaa kwa muda. Nitakaporejea tena kule wizara hii ndio wizara yangu na Mhasibu Mkuu wa Serikali atawajibika kunipokea. Kwa hivyo, nikitoka hapa ni lazima nitetee mapema kuhusu maslahi ya wafanyakazi.

Mhe. Spika, maslahi ya wafanyakazi bado, ingawaje ni ongezeko la mshahara ambalo wataongezewa wafanyakazi wa chini lakini hebu tutazame na tujiulize hili swali ambalo nimeshalisemea mara mbili au tatu. Maslahi kutokana na huu upandaji wa maisha kwa kweli mfanyakazi wa chini sasa hivi hata ukimpa hiyo shilingi 125,000 kwa kweli haisaidii. Kwa sababu mtu wa chini kwa siku sasa hivi anatumia si chini ya shilingi 20,000, hebu tumpangie huyu kwa muda wa siku 30 anatumia kiasi gani. Kwa hivyo Mhe. Spika, juu ya kuwa wizara hii ni wizara yangu na naipenda sana kwa sababu na mimi ni mdau katika wizara na nina imani kwamba na wao mpaka kutoka hapa watanipokea kwa nguvu zote.

Mhe. Spika, suala jengine niende Idara ya Upigaji Chapa. Mhe. Spika, hii ni idara ambayo serikali inaitumia na katika moja nikisema kwamba Wizara ya Fedha ina jukumu kwanza la kusimamia mapato na hivi vianzio vya mapato.

Hii ni idara moja Mhe. Waziri nimwambie kwamba nayo inakusanya mapato mengi tu. Kwa hivyo hii idara kutokana na hali ya kuona kwamba mashirika na idara nyingi ambazo zinakwepwa sana na hii ni moja ambayo kazi zetu kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi karibuni tu hivi tumefuta madeni ambayo yalikuwa wakati umeshakuwa mkubwa na sasa hivi yapo nafikiri kwenye *pipeline* kwamba haya madeni yaachwe kabisa.

Sasa tukisema tunazidi kukwepa nina hakika kwamba hivi sasa itakuwa serikali yote inawategemea wao wa kuchapisha hizi wizara. Nina hakika hata maposho kwa sababu watu wanafanya kazi mpaka saa nane za usiku kwa kuviandaa vitabu hivi, kwa hivyo nina hakika kwamba yale maslahi yao pia na wao wapewe kwa wakati ili na wapate ile *moral* ya kufanya kazi.

Mhe. Spika, niseme na mimi kama wenzangu waliopita kwa kweli asubuhi nilikuwa nimetaabanika kidogo lakini sasa hivi nasema kwamba napitisha bajeti hii kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Amani kwa asilimia 99.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, baada ya kukushukuru kwa kunipa fursa hii naomba na mimi niungane na wenzangu kuwapongeza na kuwashukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake. Kwa kweli kuongoza Wizara ya Fedha wazungu wanasema unahitaji *nerve of skills*, yaani uwe na kifua kweli kweli, uwe na kichwa kweli kweli na mabega uwe nayo ya kweli kweli. Kwa hivyo, kwa dhati kabisa naomba nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake na mimi nawapongeza kwa sababu najua yeye kaanza lakini tuna tamaa kwamba tunakokwenda ni kuzuri zaidi kwa sababu wanao uwezo wa kukutengeneza. *(Makofi)*

Mhe. Spika, la pili naomba sahibu yangu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk pamoja na Mhe. Hamza Hassan Juma walikuwa na wasi wasi wakasema wametoa hoja kwamba labda Mwanasheria Mkuu atatoa hoja za kisiasa au majibu ya kisiasa. Mhe. Spika, mimi naomba niwahakikishie kwamba siwezi kutoa hoja za kisiasa kwa sababu kwanza si mjuzi. Mimi nina wasia wa baba yetu alisema jambo ukitaka kulifanya jiulize ama uwe na jadi nalo au uwe na elimu nalo, kama huna jadi nalo wala elimu nalo basi hilo jambo usilifanye. Sasa uanasheria nina elimu nao na nina jadi nao pia, siasa hapa nadhani Mhe. Mshimba, Mhe. Hamza na wengine wakishakunifunza labda huko mbele lakini sio leo.

Lakini Mhe. Spika, ni kawaida mwanasheria unapotoa kauli au unapotoa maelezo wakati mwengine yanakuwa kama ya daktari, maana daktari ukipata mgonjwa ana kitu anachokipenda ukimwambia ni mwiko asikifanye mtagombana na atasema huyu daktari hafai hata kidogo. Mtu anapenda sukari

ukamwambie asile sukari, au napenda chumvi ukamwambie asile chumvi ingawa kwa faida yake mwenyewe. Sasa hilo si jambo la ajabu ndio kama haya, mwanasheria utasema jambo kwamba hili ni kinyume na sheria, lakini mtu akilipenda lazima akuone mbaya na lazima akupe jina kwamba umetoa hoja au jibu la kisiasa.

Mhe. Spika, jambo jengine la pili kuna mambo mawili yote naomba niyaseme nikiri kuwa ni kwa upya wangu ambayo nimeyaona hapa katika hoja hii yamejitokeza sana. La kwanza ni hoja hizi ambazo zimeshajadiliwa, zimeshatolewa maelekezo ndani ya mkutano huu huu wa Baraza, naona nyingi zimerejeshwa tena na ametakiwa Mhe. Waziri azitolee maelezo tena.

Mhe. Spika, hoja nyingi hizi zilizotolewa suala la kiwanja, suala la Kiwanda cha Mahonda, ni hoja ambazo zilipojadiliwa ndani ya Baraza hili kwa kweli zililipatia sifa sana hili Baraza. Kwa sababu waliotoa hoja hizi walizitoa kwa umakini na huko nje watu wakawasifu kweli kweli jinsi walivyoweza kuibana serikali mpaka ikatoa maelezo. Lakini nayo serikali pia ikapata sifa kwa kutoa maelezo, mpaka jana mazungumzo baada ya habari nasikiliza unasifiwa umakini huo wa Baraza, sio wa Mawaziri peke yake, wala sio wa Wawakilishi peke yake. Lakini zilizosababisha sifa hizi ni hizi hoja ambazo naona leo zimerudi tena.

Sasa mimi wasi wasi wangu tu mdogo kwamba hili Baraza limeshapata sifa kubwa kwa hoja hizi. Mhe. Spika, nachelea isije ikawa ni ile sifa za Hababeli, maana Hababeli aliona mwezi tena ule wa sikukuu watu wakamsifu kweli kweli kwamba bwana mwezi ule umetuhangaisha kauona Hababeli. Baada ya nusu saa sifa zilipoanza kupungua akasema na ule pale mwengine. Sasa Mhe. Spika, ikawa zile sifa zote alizopata zikaporomoka kwa hiyo kusema na ule pale mwezi mwengine. *(Kicheko)*

Sasa na mimi naomba kwa hizi hoja kwa sababu kwanza kwa kanuni zetu hoja ambayo imeshajadiliwa utaniongoza, ndio nasema hili nalisema kwa upya wangu, sidhani kama inapaswa tena ije ijadiliwe, itolewe maamuzi, itolewe maelekezo mengine tena katika mkutano huu huu ambao ulilijadili.

Mhe. Spika, jambo jengine la tatu ambalo naomba pia niliseme kwa upya wangu labda ni suala la kuleta naona kwamba kumekuwa na *change* ya kusema uletwe mkataba huu na huu imeorodheshwa hapa. Hoja hii nayo pia imeshatolewa na ikajadiliwa na muongozo ukatoka. Lakini Mhe. Hija Hassan Hija yeye anasema kwa kutumia kifungu cha 9 cha Sheria yetu Nam. 4 ya mwaka 2007, basi kaorodhesha mikataba mingi kwamba iletwe hapa mbele ya Baraza kwa sababu ana haki kama Mjumbe.

Mhe. Spika, nadhani kwenye Sheria ile ya Kinga, Haki na Fursa za Wajumbe pengine sikuwa mwalimu mzuri lakini nilikuwa mmoja ninayesomesha sana somo hili kwamba kuna kinga na fursa za Mjumbe mmoja mmoja na kinga na fursa za Baraza zima. Sasa kifungu cha 9 kinazungumzia haki za Mjumbe mmoja mmoja kama Mjumbe unapokuwa.

Lakini suala la kuleta *document* maana ukishakuzileta nyaraka kwanza zina utaratibu wake wa kuzileta, ukishakuleta document mtu ana haki ya kuhoji ndio au sio, una haki ya kumuita pengine aliyeitengeneza hiyo *document*. Sasa nadhani kwenye Baraza hapa huwa hizo *document* haziletwi au hakuna utaratibu wa kuzileta kwa sababu hazipati kufanyiwa kazi. Mikataba, ushahidi wa maandishi na mpaka kwenda kutembelea *site* hiyo ni Baraza lakini linapokuwa katika utaratibu mwengine wa kamati ama wa Kamati Teule au Kamati za Kudumu.

Sasa huko mna haki ya kusema hata kama kuna gari ina mzozo imenunuliwa iletwe muione au mkaione ilipo. Maana tukianza hizi *document* ziletwe hapa katika utaratibu huu wa Baraza sisi tutakapokuwa na mzozo wa gari ukasema iletwe sijui itakuwaje kama itaingia humu ndani au tutaahirisha tutaiangalie hapo nje. Sasa hili nadhani ni vyema tukaelewana. Baraza ni kweli sheria imelipa uwezo wa kudai hizi nyaraka, hati na vitu vyengine mbali mbali ambavyo inavichunguza lakini kwa utaratibu wake.

Mhe. Spika, hakuna jambo zuri kuliko utaratibu, maana utaratibu ndio unaohalalisha. Mhe. Spika, kama kuna ibada nzuri basi ni sala, ndio utaambiwa itakwenda kuhesabiwa sala kwanza halafu ndio yaangaliwe mengine. Lakini huwezi kusali alfajiri rakaa nne na uzuri wake, lakini alfajiri rakaa nne utatia nia labda usahau. Sasa mimi naomba hizi taratibu zetu ndio zitakazohalalisha mambo yetu ni vizuri kuzifuata.

Mhe. Spika, eneo jengine alizungumza Mhe. Ismail Jussa Ladhu na namshukuru sana kuhusu *instrument* za kiuchumi. Mimi nakubaliana nae kwamba kwa kweli moja katika tatizo tulilonalo katika mfumo wa Muungano wetu ni mgawanyo wa hizi *instrument* za kiuchumi. Mimi hilo nimekuwa nikilisema siku zote na sioni haya kulisema popote.

Kwa mfano, unaposema *income tax* mimi siijui nchi ambayo ya kisiwa inaweza kuendelea kwa kuwa na mfumo wa kodi ya mapato sawa sawa na Bara tuseme. Kwa hivyo, alilolisema mimi nakubaliana nae kuna haja kama huko tunakokwenda eneo la kuliangalia na kulitazama namna gani masuala haya ya kiuchumi tukaweza kuwa na fursa katika kuyaangalia na kuyawezesha Zanzibar kuyatumia kwa ajili ya maendeleo yake ya kiuchumi.

Lakini Mhe. Spika, kuna moja ambalo nilisema labda nilitolee ufafanuzi tu suala la *stock and change.* Anasema kwamba *stock and change* kwa nini ni moja au iko Bara tu na kwamba kampuni ya Zanzibar ukitaka kwenda kuwa *listed* pale lazima ukabatizwe kwanza Tanzania Bara hilo ni kweli. Lakini makampuni ya Tanzania Bara ingekuwa sisi ndio tumeanzisha *stock and change,* kampuni ya Tanzania Bara ikitaka kuja hapa Zanzibar nayo ingehitaji ifanye hivyo hivyo kwa sababu uchumi wetu wa makampuni ni tofauti. Kuna sheria mbili tofauti za makampuni na masuala ya *capital market* yamezaliwa kutokana na sheria za makampuni sasa hivi tu yamekuwa *regulated* vizuri. Lakini ukiangalia ni kwamba yametokana na sheria hizi za makampuni.

Moja kwa nini lazima ubatizwe ni kwa sababu ili uingie kwenye *stock and change and stock market* kuna *retirement* za *disclosure,* kuna *retirement* za *qualification* za *directors,* kuna *regulations* nyingi ambazo bahati mbaya kwenye sheria yetu ya makampuni hapa hazimo *retirement* hizo. Sisi bado tunatumia sheria yetu ime-*base* na sheria ya Uingereza ya mwaka 1945. Waingereza wenyewe wameshaiacha zamani lakini sasa hivi kuna juhudi najua za kuifanyia marekebisho makubwa ili iwe ya kisasa kama kwa wenzetu.

Kwa hivyo, kwa sasa hivi kwa hili ni lazima litaendelea kwa sababu dunia nzima hata ukitaka kufanya *cross meeting* basi ni lazima kuna masharti uyapate ya pale pahala au ile nchi ambayo inasimamia makampuni. Lazima kampuni yako uendeshaji wake, *standard* zake zilingane na sheria ya makampuni ya ile nchi ili upate kuwa *regulated* kwa sababu pale sasa unachukua fedha za watu. Unapokwenda kwenye *capital market* maana yake ni kwamba unawaambia watu leteni pesa zenu tutumie sisi tunajua namna ya kutumia mtapata faida ndio hilo tu.

Wala sisi Zanzibar hatuzuii kuanzisha hizi *capital market* lakini kwa *nature* ya uchumi wetu Zanzibar hapana *public company* hata moja. Kwa hivyo, ni mambo ambayo tuimarishe kiuchumi ili na sisi tufike pahala tuweze kuanzisha hizi *public company* ili tuweze kuanzisha hizi *capital market.* Lakini ni jambo hatuhitaji uamuzi wa mtu mwengine yeyote isipokuwa tunahitaji kujiimarisha sisi katika uchumi tuweze kufika hatua ambayo wenzetu wamefika.

Mhe. Spika, jengine ni kuhusu suala la *BoT* Tume ya Pamoja ya Fedha. Hili namna lilivyozungumzwa linazungumzwa kama kwamba ni kosa la Serikali ya Zanzibar bado haijakuwa makini, haijachukua juhudi za kutosha katika kufuatilia suala la Tume ya Pamoja ya Fedha. Mhe. Spika, Tume ya Pamoja ya Fedha imeshakuja ikakutana na Wajumbe wa Kamati za Baraza hili mara mbili, Wajumbe wale tena sio wa Zanzibar, Wajumbe wale kutoka Tanzania Bara wameeleza jinsi gani Serikali ya Zanzibar ilivyokuwa *serious* katika kufuatilia

mambo ya *BoT*. Wameeleza kikwazo ambacho wanakipata kutoka kwa wenzetu Serikali ya Muungano. Serikali imeletewa ripoti au mapendekezo mbali mbali imeweka *order* na *consultant* kuja kuifanyia kazi ikajadili mbele ya Baraza la Mapinduzi ikasubiri wenzetu waweze na wao kutoa mapendekezo yao.

Mhe. Spika, *BoT* zaidi ya mara tatu mpaka juzi tu wametaka kuja kuuona uongozi hapa wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuanzia Rais, Makamo wa Kwanza wa Rais, Makamo wa Pili wa Rais na wamepata *access* ya kuonana nao, mwaka juzi walikuja wakaonana nao vile vile. Lakini *BoT* hii kwa upande wa Tanzania Bara mwisho wameishia kwa Makamo wa Rais. Sasa mimi napata shida tunapoona kwamba kama labda Serikali ya Zanzibar ndio inayoona tatizo la jambo hili na kwa kweli imefanya kazi kubwa sana imekuwa *serious* katika hili.

Mhe. Spika, mimi nadhani wakati sasa sio wa kuilaumu Serikali, ni wakati Baraza liisaidie Serikali katika hili. Nasema Baraza liisaidie Serikali kwa sababu gani. Kwa sababu hili Baraza lina Wawakilishi watano wa Bunge wanaingia Bungeni na kule ndio inakopitishwa Bajeti ya Serikali ya Muungano. Sasa ikiwa wale Wabunge wetu wa Baraza wasiilaumu Serikali, sisi tuwalaumu wao kwamba hawajaisaidia Serikali labda kwenye hili.

Kwa sababu ibara ya 133 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema wazi kwamba kutakuwa na Akaunti ya Pamoja ya Fedha na matumizi yote ya mambo ya Muungano fedha zake zitaingia mle na zitatumiwa kutoka mle kwenye Akaunti ya Pamoja ya Fedha. Sasa leo kama Akaunti ya Pamoja ya Fedha haiko, hivi ni Serikali ya Zanzibar ndio ya kuianzisha.

Sasa hiyo ni kazi ya Mbunge atusaidie aulize kwa nini na je, kuna uhalali hayo matumizi ya Bajeti ya Muungano kufanywa bila ya kutoka kwenye Akaunti ya Pamoja ya Fedha. Hayo ndio masuala rahisi ambayo Wabunge wetu Wawakilishi wangeweza kutusaidia tukaweza tukakwamuka labda kwenye jambo hili. Lakini wakiiuliza Serikali ya Zanzibar kwa kweli ni ya kuionea huruma kwa sababu imehangaika sana katika hili, imejitahidi, imekuwa *very receptive, very cooperative* kwenye hili. Kwa hivyo, mimi niombe kwamba kwenye jambo hili labda watusaidie.

Mhe. Spika, la mwisho ambalo alilizungumza Mhe. Mbarouk Wadi Mussa suala la kesi ya sio wastaafu waliostaafishwa, *retrench* wanasema. Wakati wa *restructure* ile ya *PBZ* ripoti zote za kitaalam zilionesha kwamba kunahitajika baadhi ya wafanyakazi wastaafishwe. Leo ndio maana tunasema *PBZ* inafanya vizuri ni kwa sababu maamuzi magumu hayo ilibidi yafanyike na taratibu

zikafuatwa za kuwastaafisha wakachukua chao. Baada ya kuchukua chao binadamu, baada ya kutumia zimekwisha wanasema aaaa bwana tazama utaratibu hapa haukufuatwa. Lakini tukishachukua tumeshatia mfukoni aliyelea na mke pengine na mtoto ameshapata kabisa hapo ndio ni haki yao kulalamika, siwezi kumzuia mtu kulalamika. Wakaenda Mahakamani, Mahakama Kuu ikatoa uamuzi, *PBZ* ikakata rufaa Mahakama ya Rufaa, uamuzi ukatoka *PBZ* wakashinda Mahakama ya Rufaa. Lakini ilipokuja kutolewa *decree* cha kushangaza mna maneno ndani ya ile *decree* ambayo hayamo kwenye hukumu yalikuwa yanaonesha kwamba wale wengine ndio wameshinda. Ndio maana *PBZ* wakapeleka ombi jengine, hata sio *PBZ.*

Kwa hivyo, *PBZ* walipokwenda wakaomba kwanza itolewe kumbukumbu sahihi ambayo ilikuwa inaonesha wazi kwamba wameshinda. Lakini wale wadau wakarudi tena Mahakama ya Rufaa wakafungua ombi kutaka Mahakama itoe ufafanuzi. Wamepeleka ombi namba 20 la mwaka 2011 na ombi hili litasikilizwa tarehe 23 Agosti mwaka huu. Kwa hivyo, nadhani tusilizungumze sana kwa sababu suala bado liko Mahakamani, kinachotafutwa ni ufafanuzi kashinda *PBZ* au wameshinda wafanyakazi.

Kwa hivyo, Mhe. Mbarouk Wadi Mussa namshukuru kweli alikuwa na pointi katika hili kwa sababu kweli kuna utatanishi huo. Lakini maelezo yake kwa ufupi ni hayo hapana *foul play* katika hili isipokuwa tunasubiri tarehe 23 Agosti itakuwa ndio fainali na mwenye haki atajulikana.

Mhe. Spika, mimi niseme katika maeneo hayo, baada ya kuzungumza hayo niunge mkono hoja na niwaombe wenzangu kwamba tumuunge mkono Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Naamini sote tunamuamini umahiri wake, uwezo wake wa kufanya kazi ili aanze kusia mapema. Tunasema asie mapema ili tuweze kuvuna mapema tusichelewe msimu. Mhe. Spika, nakushukuru, ahsante.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe wachangiaji wote ambao waliomba wamepata nafasi na wameshatoa michango yao. Niliwasiliana na Mhe. Waziri na amepata maoni ya Waheshimiwa Wajumbe wengi kwa hivyo sasa suala hili lije likamilishwe kesho kwa ajili ya kutoa majumuisho au ufafanuzi wa hoja mbali mbali. Basi tusitishe shughuli zetu kuanzia hapa na sasa niahirishe kikao hichi mpaka kesho tarehe 29/7/2011 saa 3:00 barabara za asubuhi.

(Saa 12:30 Baraza liliahirishwa mpaka
tarehe 29/7/2011 saa 3:00 asubuhi)